Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Kumi – Tarehe 24 Juni, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 84

**Barabara ya Kuunganisha Wilaya ya Sikonge na Urambo**

**MHE. JUMA S. NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara itokayo Tutuo – Mole – Usanganya – Izimbili hadi Urambo barabara fupi ya kuunganisha Wilaya za Sikonge na Urambo na kwa kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya barabara hiyo mara nyingi hazitoshelezi matengenezo yanayohitajika ili barabara hiyo iweze kupitika kwa majira yote:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuiongezea fedha barabara hiyo ili iweze kupata matengenezo ya kuiimarisha zaidi?

(b) Je, daraja lililopo Kitongoji cha Ibumba ambalo limeharibika sana kutokana na mvua za msimu uliopita, litatengewa fedha za kutosha ili kujenga daraja linaloweza kuhimili maji mengi ya Mto huo hasa nyakati za mvua nyingi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Swali hili ni zuri sana, nitakaporejea *back bencher* nami nitaweza kuliuliza kama hili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, matengenezo ya barabara ya kuunganisha Wilaya za Sikonge na Urambo yanafanywa kwa pamoja na Halmashauri za Sikonge na Urambo kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara *(Roads Fund*). Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge inafanya matengenezo kwenye sehemu ya Tutuo, Mole hadi Usanganya yenye urefu wa kilomita 27 ambapo katika sehemu hii ndipo daraja la Ibumba lilipo.

Halmashauri ya Wilaya ya Urambo inafanya matengenezo ya barabara hiyo kwa sehemu ya Usanganya - Izimbili hadi Usoke yenye urefu wa kilomita 46 ambapo barabara hii inaunga kwenye barabara ya Mkoa ya Tabora – Urambo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ilitenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya kawaida *(Routine Maintenance)* kwa barabara hiyo kiasi cha Sh. 13,940,000/=. Pia kwa mwaka 2008/2009, Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge imetengewa Sh. 13.91 kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara ya kilomita 27 na Sh. 4,590,000/= kwa ajili ya matengenezo ya maeneo korofi ya kilomita nane na Sh. 2,000,000/= kwa ajili ya matengenezo ya makalvati katika eneo la barabara lililopo upande wa Sikonge.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Halmashauri ya Wilaya kupitia Mfuko wa Barabara ilitenga Sh. 90,781,200/=, fedha hizo zimetoka katika Mpango wa Usafiri katika Halmashauri *(Local Government Transport Programme*), pia ilitenga Sh. 34.9m/= ili kufanya matengenezo ya maeneo korofi kutoka Usoke hadi daraja la Ibumba. Kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imeleta maombi ya Sh. 84m/=, lakini imetengewa Sh. 28m/= kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum ya kilomita nne kwa barabara ya Ibumba –Izimbili – Sikonge *Boarder*.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu daraja lililoko Kitongoji cha Ibumba, Halmashauri ya Wilaya Sikonge imetengewa Sh. 2,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa mistari mitatu ya kalvati yenye kipenyo cha sentimeta tisini ambalo litasaidia kupitisha na kuhimili maji yatakayopita kwenye daraja hilo.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha kupatikana kwa fedha za kutosha na usimamizi zaidi wa matengenezo ya barabara hii, likiwamo daraja la Ibumba, kikao cha Bodi ya Barabara, Mkoa wa Tabora kilichofanyika tarehe 27 Oktoba, 2007 kilipendekeza kuwa

barabara hii ya Tutuo – Mole – Usanganya – Izimbili hadi Usoke ipandishwe daraja ili iwe ya Mkoa hivyo iweze kuhudumiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*).

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mwaka jana Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ilipokuwa inatoka Urambo kwenda Sikonge ilipofika kwenye daraja hili ilikwama, ikarudi Urambo na ilibidi izunguke Tabora kwa kutumia siku nzima na kwa kuwa fedha alizozitaja Mheshimiwa Waziri ni ndogo kufuatana na maji mengi yanayopita hapo. Je, Serikali ipo tayari kuwakomboa watu wa Urambo na Sikonge kwa kutengeneza daraja hili? (*Makofi*)

**SPIKA:** Asubuhi ya leo imeanza vizuri sana. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama utakumbuka nami mwenyewe nilipita katika maeneo haya ingawa sikupita ile barabara ya *shortcut* bali nilipita kutoka Tabora kwenda Urambo na nilipofika Izimbili kilio cha wananchi kilikuwa ni hiyo barabara ya *shortcut* ya kutoka Sikonge hadi Urambo.

Tunafahamu hilo tatizo ni kubwa na ndiyo maana tunasema kwamba tukishirikiana na wenzetu wa *TANROAD* tutahakikisha kwamba barabara hii inaingia katika barabara ambazo zinahudumiwa na Mkoa ili iweze kupewa fedha nyingi zaidi lakini kwa sasa hivi tumeitengea fedha za kutosha ili angalau iweze kupitika. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa Spika kwamba, kwa kushirikiana na wenzetu wa *TANROAD* tutahakikisha kwamba barabara hii inapandishwa daraja. (*Makofi*)

Na. 85

**Ubovu wa Miundombinu – Kinondoni**

**MHE. ALI KHAMISI SEIF** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Msasani ni miongoni mwa watu wanaochangia kodi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kodi ya majengo kwenye Manispaa ya Kinondoni na kwa kuwa licha ya michango hiyo maeneo hayo yameachwa kuwa na miundombinu mibovu kwa mfano, kutokuwepo mifereji:-

Je, Serikali haioni kuwa haiwatendei haki wananchi hao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, wananchi wa Msasani ni miongoni mwa wananchi wanaochangia kodi mbalimbali kwenye Manispaa ya Kinondoni. Eneo la Msasani kwa uasili wake ni eneo tepevu (*swampy area)* ambalo maji ya mvua kutoka sehemu mbalimbali yalikuwa yakipita hapo kuelekea baharini na maji mengine yanayotuama na kuyeyuka kutokana na jua (*evaporation*).

Mheshimiwa Spika, baada ya maeneo hayo kuendelezwa kwa kupimwa viwanja, mifereji ya maji ya mvua ilijengwa katika barabara ya *Old* Bagamoyo. Kutokana na maeneo hayo kuendelea kuendelezwa wakati miundombinu ya mifereji ikibakia kuwa ileile ya awali, kwa sasa mifereji hiyo imezidiwa uwezo. Hali hii imesababishwa na ukubwa wa makalvati yaliyopo kutotosheleza wingi wa maji na makalvati hayo kuziba mara kwa mara kutokana na kujaa matope na taka ngumu.

Mheshimiwa Spika, katika mikakati ya uboreshaji wa miundombinu, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imekwishajenga mfereji wa maji ya mvua wenye urefu wa mita 585 ambao ulichangiwa na wawekezaji wa eneo hilo kwa kupitia mpango shirikishi.

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa kushirikiana na wakazi wa eneo la Msasani wanaendelea kujenga mfereji wa maji ya mvua wenye urefu wa mita 1,050 ambao utapunguza mafuriko kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imekamilisha kujenga mifereji yenye urefu wa mita mia nne eneo la *TIRDO* na Msasani Shule ya Msingi. Kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Halmashauri hiyo imeomba kiasi cha Sh. 2bn/= kwa ajili ya matengenezo ya barabara zake ikiwamo na mifereji. Kwa juhudi hizi zinazofanywa ni dhahiri kwamba Serikali inawathamini wananchi wote ikiwa ni pamoja na wale wa Manispaa ya Kinondoni.

**MHE. ALI KHAMISI SEIF:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani katika kuhakikisha kwamba barabara ya Msasani inapata huduma ili iweze kuwahudumia wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Msasani kama zilivyo barabara zingine itakuwa inapewa kipaumbele kulingana na uwezo wa fedha za Serikali. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba Manispaa ya Kinondoni kwa mwaka huu imeomba Sh. 2bn/= kwa ajili ya matengenezo ya barabara pamoja na mifereji. Kwa hiyo, barabara ya Msasani ni mojawapo kati ya hizo barabara ambazo zitapewa kipaumbele katika kutengenezwa.

Na. 86

**Mashindano ya Mpira wa Pete Kumuenzi Hayati Baba wa Taifa**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kumuenzi Hayati Baba wa Taifa Mwalimu J.K. Nyerere, Chama cha Taifa cha Mpira wa Pete (*Netball*) kilikuwa na utaratibu mzuri wa kuweka mashindano ya mpira huo kwenye Mji wa Dodoma kila mwaka jambo ambalo kwa kipindi kirefu sasa mashindano hayo hayajafanyika tena:-

(a) Je, kwa nini mashindano hayo hayafanyiki tena kwani imepita miaka miwili sasa?

(b) Je, kuna mpango gani wa kuirudisha michezo hiyo au imehamishiwa mkoa mwingine?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuberi, Mbunge wa Mkwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sababu ya msingi ya kutoendelea kufanyika kwa mashindano ya mpira wa Pete yenye lengo la kumuenzi Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere, ni kukosekana kwa fedha. Ili mashindano hayo yaweze kufanyika, kunahitajika fedha kwa ajili ya gharama mbalimbali za kuendeshea mashindano hayo.

Gharama hizo ni pamoja na usafiri wa ndani wakati timu zinapowasili, posho kwa marefa, wasimamizi, ununuzi wa vikombe, malazi na chakula kwa timu zinazotoka nje ya nchi kama vile Kenya, Uganda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafanya mazungumzo na waanzilishi wa mashindano haya ili kuweza kutafuta wafadhili watakaoweza kuyadhamini. Aidha, kituo cha mashindano hayo hakijabadilika ambacho ni Dodoma.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBERI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Vyama Vingi vya michezo vinalalamika kuhusu suala la fedha Je, Wizara haitengi Bajeti ya makusudi kuhusu michezo hii ambayo inachezwa hapa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kutegemea wadhamini mara nyingi sana baadhi ya michezo kwa sababu wadhamini wanaangalia maslahi na *interest* zao katika michezo. Je, Waziri haoni kutegemea wafadhili baadhi ya michezo inaweza kufa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatenga Bajeti kwa ajili ya michezo lakini kutokana na hali halisi na vipaumbele vya nchi ni kwamba, Bajeti ya suala zima la kuendeleza michezo ipo lakini haitoshelezi kwa michezo yote, akitazama hata kwenye jedwali ambalo tunalo Serikali inatenga karibu Sh.

90m/= kwa ajili ya michezo yote na michezo ipo zaidi ya thelathini na sita na michezo yote iwe na mashindano ndani na nje ya nchi, ndiyo maana tunahimiza Vyama vya Michezo nchini navyo viwe na jukumu la kutafuta fedha wao wenyewe na ndiyo maana wamechukua uongozi na ukiwa kiongozi maana yake lazima utafute mbinu za kuendeleza michezo yenyewe. Haipendezi uwe Mwenyekiti wa Chama fulani au uwe kwenye Kamati ya Utendaji ya Chama fulani na huna uwezo wa kutafuta hata senti moja utegemee Serikali ndiyo ifanye shughuli hiyo. Kwa hiyo, naomba nitoe wito kwa Vyama vyote vya Michezo nchini kwamba pamoja na mgao mdogo wanaopata Serikali na wao wenyewe wawe na juhudi za kutafuta fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, wafadhili ni miongoni mwa wananchi wa Tanzania ambao nao wana jukumu la kuendeleza michezo. Duniani kote michezo inaendeshwa na Serikali pamoja na watu binafsi na wafadhili mbalimbali. Kwa hiyo, tutaendelea kuwategemea wafadhili katika baadhi ya michezo na ningeomba pia nitoe wito kwamba wafadhili waendelee kujitokeza kusaidia michezo kama ambavyo Serengeti, *NMB* na mashirika mengine mbalimbali yanayosaidia katika kuendeleza michezo nchini.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wanawake wameonyesha umahiri mkubwa katika mchezo wa pete na kwa kuwa wanawake hao hao wameonyesha umahiri mkubwa katika mpira wa miguu mfano *Twiga Star*. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuhakikishia au kutueleza kuna mpango gani wa kuanzisha mpira wa miguu katika mikoa yote na kuweza kupata timu ya Taifa ya wanawake wachezaji wa mpira wa miguu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze kwa sababu yeye ni mfuatiliaji mzuri sana na kama mnavyofahamu katika Waheshimiwa Wabunge wachache wanaocheza *football* yeye ni mmojawapo na anafuatilia sana masuala ya mpira wa miguu. Nataka nimhakikishie kwamba timu yetu ya wanawake ya mpira wa miguu bado ipo na inaendelea kufanya mazoezi na pindi kutakapokuwa na mashindano naamini kabisa ikiingia kiwanjani itafanya vizuri kwa sababu inafanya mazoezi kwa program ambayo imeandaliwa na *TFF*.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la kuendeleza mchezo huu ni kwamba, *TFF* inayo Kamati Maalum ya Mpira wa Wanawake pale Makao Makuu na wana *program* maalum katika nchi nzima ya kuendeleza mchezo huu wa mpira wa miguu kwa wanawake kwa nchi nzima na *program* hii naamini itakaposambaa katika maeneo mengine tutaweza kupata wachezaji wa kuweza kuunda Timu ya Taifa nzuri. Sasa hivi *program* hiyo inaendelea na katika hii *system* ambayo Serikali imeanzisha ya kuanzisha michezo ya shule za msingi na huu pia tutauanzisha katika shule zote, vyuo vyote na taasisi zote ili tuweze kupata wachezaji wazuri kuanzia ngazi ya shule mpaka kwenye vijiji na kadhalika.

Na. 87

## Mgao wa Misaada ya FIFA kwa TFF na ZFA

**MHE. HAFIDHI ALI TAHIR** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa zaidi ya miaka 43 hivi sasa kumekuwa na utatanishi mkubwa juu ya maslahi, masomo, mikutano na vifaa vinavyotolewa na Shiriksho la mpira ulimwenguni (*FIFA*) kutumiwa na *TFF* bila ya ridhaa ya *ZFA*, ambavyo ni vyama viwili tofauti vya soka ndani ya Muungano lakini vinavyofanya kazi kwa kujitegemea na kusaidiwa na Serikali husika na kwa kuwa tarehe 21/6/2007 Waziri wa Michezo Tanzania Zanzibar alimwandikia barua Waziri wa Michezo wa Muungano kuhusu mgao wa msaada wa Dola za Kimarekani 250,000 zilizotolewa na *FIFA* kutokwenda *ZFA*:-

(a)Je, Serikali kupitia Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wa Muungano amechukua hatua gani juu ya jambo hilo?

(b)Je, Serikali inatarajia kuunda lini chombo kitakachosimamia masuala ya Kimataifa ya mpira wa miguu ili kuondoa utata huo wa muda mrefu na ukiritimba usio wa lazima?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakiri kupitia Bunge lako Tukufu kupokea barua kutoka kwa Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar kuhusiana na mgao wa msaada wa dola za Marekani 250,000 zilizotolewa na *FIFA* kutokwenda *ZFA*.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imefanya vikao kadhaa na Wizara ya Utamaduni na Michezo ya Zanzibar kuhusu masuala mbalimbali ya ushirikiano katika sekta ya Utamaduni na Michezo. Kufuatia vikao hivyo, Wizara hizi mbili zilitoa ushauri wa *TFF* na *ZFA* kukaa pamoja na kujadili juu ya Maendeleo ya Michezo, ukiwemo mpira wa miguu.

Aidha, Vyama hivi viwili viliagizwa kufanya mazungumzo ya pamoja ili kujadili pia juu ya mgao wa misaada inayotolewa na *FIFA* hasa tukizingatia kwamba sisi ni nchi moja Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgao wa msaada wa Dola za Marekani 250,000 ambazo zilitolewa na *FIFA* kutokwenda *ZFA*, ni kwamba kulingana na utaratibu wa matumizi ya fedha hizo, hazikupaswa kutolewa kama mgao.

Kwa mujibu wa matumizi ya fedha hizo, *TFF* ikishapokea, hutakiwa kabla ya kuzitumia kuwasilisha *FIFA* mchanganuo wa matumizi yake na *FIFA* baada ya kuridhika na mchanganuo huo huidhinisha matumizi hayo. Hivyo ndivyo kanuni na taratibu za *FIFA* zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Dola za Marekani 250,000 zilizopokelewa na *TFF* kutoka *FIFA* zilitumika kwa shughuli za maendeleo ya michezo wa mpira wa miguu kwa manufaa ya pande zote mbili, Zanzibar na Bara. Kulingana na matumizi ya dola hizo, shughuli zifuatazo zilihusika:-

1. Kozi mbalimbali za Utawalana Mipango.. ..... ..... ...... ....... $ 70,000
2. Michezo kwa Timu ya Taifaya Vijana...… … ... ..... $ 40,000
3. Maendeleo ya Kiufundi... … … …$ 35,000
4. Timu ya Taifa ya Wanawake... … $ 25,000
5. Madawa ya wachezaji... … … …$ 15,000
6. Mafunzo kwa marefa... … … … $ 25,000
7. Mashindano ya Timu ya Taifa... …$ 10,000
8. Matengenezo na ununuzi wa Vifaa vya Ofisi......................... $ 30,000

**JUMLA**... … … … … ...... **$ 250,000**

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kuunda chombo kitakachosimamia masuala ya Kimataifa zaidi ya vyombo vilivyopo kama vile *TOC* na kadhalika kwani haioni suala la *TFF* na *ZFA* ni la utata au kuna ukiritimba katika utekelezaji wa majukumu yake. *ZFA* inatambuliwa na *CECAFA* yaani Shirikisho la Mpira la Afrika Mashariki na Kati na inatambuliwa pia na *CAF* yaani Chama cha Mpira cha Afrika wakati *TFF* inatambuliwa na *CAF, CECAFA* na *FIFA*.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, sina budi kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu kajibu swali langu lakini baadaye nataka unisaidie mwongozo wako katika Fungu 46 ukurasa wa 28 wa Kanuni zetu kwa sababu baadhi ya kanuni zetu hazina meno ya kutafuna. Kifungu hiki kinasema maswali kujibiwa kwa ukamilifu. Hili suala halikujibiwa kwa ukamilifu. Hivi Waziri anachukuliwa hatua gani? Baada ya majibu hayo naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, ufafanuzi nausubiri. Pamoja na majibu aliyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo hayaridhishi wala hayakidhi haja, nimeuliza swali la mgao wa Dola 250,000 na nikasema kwamba kuna vifaa, masomo na mikutano, Mheshimiwa Waziri hakulijibu hili. Lakini pamoja na majibu aliyotoa katufafanulia matumizi ya Dola 250,000 zilizotolewa swali liko hapa. Je, anaweza kuliambia Bunge hii katika mgao huo utawala na mipango, Zanzibar wamefanyiwa nini? Anaweza kuliambia Bunge hili Maendeleo ya kiufundi, Zanzibar imefanyiwa nini na anaweza kuliambia Bunge hili matengenezo na ununuzi wa vifaa vya ofisi kitu gani kimepelekwa *ZFA*? Hilo swali la kwanza. (*Kicheko*)

La pili, wakati akijibu swali la pili, Mheshimiwa Waziri alisema kwamba Serikali haina nia ya kuunda chombo lakini wakati huo huo akatuambia kwamba *TOC* imeshaundwa, *TOC* ni Tanzania *Olympic Committee*, hiki ni chombo kinachoshirikisha Zanzibar na Bara katika mambo ya michezo ya riadha na mingine, Mwenyekiti wake anatoka Zanzibar anaitwa Gulam Abdallah, Katibu wake ni Filbert Bay. Je, *TFF* ambayo inawakilisha Tanzania kwa niaba ya Zanzibar nani anaongoza *TFF* kutoka Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimhakikishie kwamba nimejibu swali tena kwa kina bila wasiwasi wowote kwa sababu yeye alitaka kujua suala zima la mgao wa fedha wa Dola 250,000 zilizotolewa na *FIFA* na nimetoa mpaka mchanganuo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka nimhakikishie nimejibu swali kwa sababu fedha zinazotolewa na *FIFA* nimesema wazi si za mgao. Chama husika ambacho ni *TFF* kinatakiwa kinapohitaji fedha na hii ni kwa Vyama vyote dunia nzima wanapeleka maombi kwa kuandika mchanganuo au *project proposal*, wanapeleka *FIFA*, *FIFA* ndipo wanapoleta fedha. Kwa hiyo *TFF* wanafanya hivyo na wanapopeleka ndio huletewa fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, yeye anataka kujua kwamba, je, masomo, mafunzo yalikuwaje. Nimemweleza hapa na naomba nimpe *data* ili aweze kujua kwamba nimejibu kihalali. Zimefanyika kozi za utawala, kozi za utawala zilipofanyika *TFF* kwa ushirikiano wao na *ZFA* wameweza kuleta watu kumi na sita kuja kwenye kozi za Marefa. *TFF* wamefanya kozi ya mafunzo ya makocha wameleta makocha kumi kutoka Zanzibar. Hiyo yote inaonyesha kwamba zile fedha hazitumiki kwa ajili ya *TFF* peke yake, zinatumika kwa ajili ya *ZFA* na *TFF*. Tatizo lililopo hapa *TFF* ni Chama kinachoendeleza mpira Bara na *ZFA* ni Chama kinachoendeleza mpira Zanzibar na hivi si vya Muungano, kila watu wana Katiba yao na utaratibu wao lakini tatizo lililopo hapa *ZFA* na *TFF* hawapatani. (*Makofi*)

Sisi kama Wizara tumekutana mara nne, sio Wizara ya Muungano lakini kwa kuona kwamba sisi ni nchi moja, tunakutana, tunazungumza mambo yetu ya maendeleo ya michezo na ndiyo maana hata timu ya Taifa mnaiona ni ya mchanganyiko, kuna wachezaji wanne kutoka Zanzibar. Kocha wa timu ya Taifa Ali Bushir ni msaidizi kutoka Zanzibar, Daktari anatoka Zanzibar. Lingine la ziada marefa Makamisaa wote, pamoja na kwamba *TFF* ndiyo wanaopeleka *FIFA* lakini wanafanyiwa *cooper test* ya kinchi, wengine wanatoka Zanzibar na wengine wanatoka Bara. Kwa hiyo baadhi ya marefa wanaochezesha *FIFA* wengine wanatoka Zanzibar, wengine wanatoka Bara.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu Makamisaa akiwepo Mheshimiwa Hafidh Ali anatoka Zanzibar ambapo Hafidh Ali ni Mechi Kamishna wa michezo ya *FIFA* na *CAF* lakini jina lake limepelekwa na *TFF* huko *FIFA*. Kwa hiyo, kimsingi ni kwamba tuna ushirikiano wa hali ya juu na ndiyo maana sisi kama Serikali tunalaani kitendo cha *ZFA* juzi kusema wanavunja uhusiano na *TFF*. Hatuwezi kukubali, hii ni nchi moja lazima tushirikiane na tufanye mambo yote ya Muungano pamoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Hafidh umechokoza mwenyewe, umejibiwa kikamilifu. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 88

**Juhudi za Kupambana na Ugonjwa wa Maralia**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na juhudi kubwa za Serikali katika kupambana na maambukizi ya ugonjwa wa Malaria nchini:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa vyandarua vya bure vilivyo na dawa kwa mama yeyote anayejifungua hospitalini ili iwe kichocheo kwa akinamama wajawazito kwenda kujifungulia hospitali badala ya nyumbani?

(b) Je, ni sababu ipi iliyoifanya Serikali kufuta kitengo kilichokuwa kinamwaga dawa za kuulia mazalia ya mbu kwenye maeneo mbalimbali?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa kila mjamzito anatumia chandarua chenye dawa wakati wa ujauzito na hata baada ya kujifungua. Serikali ilianzisha Mpango wa Hati Punguzo mwezi Oktoba, 2004 ili kuhakikisha kuwa kila mjamzito anayehudhuria kliniki anapatiwa hati inayomwezesha kununua chandarua chenye dawa kwa bei nafuu. Huduma ya Hati Punguzo kwa wajawazito inapatikana nchi nzima kwenye Vituo vyote vinavyotoa huduma ya uzazi na mtoto.Bei ya vyandarua hivi ni kati ya shilingi 8,000 hadi 11,000 kufuatana na ukubwa na aina ya chandarua. Hati Punguzo anayopewa mama mjamzito ilikuwa inamtaka mama achangie shilingi 2,750 tu. Hata hivyo, kuanzia mwaka huu wa fedha mama mjamzito anachangia shilingi 500 tu. Ni nia na imani ya Serikali kwamba jinsi uwezo kifedha utakavyoongezeka hatimaye akinamama wajawazito watapewa vyandarua hivyo bure. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba utaratibu umewekwa wa kuwapatia vyandarua bila malipo ya mchango kinamama ambao hawana uwezo wa kulipa.

(c) heshimiwa Spika, Serikali haikufuta kitengo kilichokuwa kinamwaga dawa za kuulia mazalia ya mbu. Unyunyiziaji wa dawa ya kuua mbu kwa kutumia dawa ya *DDT* yalisitishwa katika miaka ya 1970, sababu kuwa ikiwa ni kutokuwepo udhibiti madhubuti wa matumizi ya dawa hii. Kumekuwapo na wasiwasi kwamba matumizi ya *DDT* yanaweza kuharibu mazingira na vilevile kwamba bila uangalizi makini wadudu wanaweza kupata usugu kwa dawa hii kwa urahisi.

Hivyo agizo la Shirika la Afya Duniani ni kwamba dawa hii ipulizwe kwenye kuta na dari ndani ya nyumba kwa kiwango (*concentration*) kilichoainishwa ambacho hakina madhara kwa binadamu. Aidha, kila mwananchi atambue wajibu wake kwamba ni lazima asafishe mifereji na kutoruhusu maji kutuwama katika eneo linalomhusu.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa ruksa hii. Naomba niulize swali moja tu la nyongeza, kutokana na majibu ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, jibu lake la msingi ni mwelekeo wa kutoa vyandarua hivyo bure. Lakini katika kujibu kwake amesema bei ya chandarua ilianzia shilingi 8,000, kikateremshwa bei mpaka shilingi 2,750 na mpaka kikafikia shilingi 500. Lakini wapo akinamama ambao wanaojifungua hawawezi kuilipa hata hiyo shilingi 500 na mtoto ndiye anayeathirika. Je, siyo wakati muafaka sasa Wizara pamoja na kuwa na maandalizi hayo ikatamka tu kwamba akinamama wanaojifungua wanapewa vyandarua hivyo bure? *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nisahihishe sikusema kwamba bei ya vyandarua ilikuwa shilingi 8,000, ikateremka mpaka shilingi 2,750 na mpaka sasa ni shilingi 500.

Mheshimiwa Spika, nimesema bei ya vyandarua katika soko kwa mfano mwanaume akienda kununua dukani ni shilingi 8,000 hadi 11,000. Mjamzito kuanzia mwaka 2004 alikuwa ananunua chandarua kwa shilingi 2,750 tu na ilikuwa inamwezesha kupata chandarua na uwezo wa Serikali ulivyoongezeka tukapunguza na sasa hivi ananunua chandarua kwa shilingi 500. Nadhani ukiangalia hiyo *trend* utaona nia ni kwamba wapatiwe vyandarua bure. Sasa hivyo vyandarua vinatolewa kwa akinamama wanapokwenda kujifungua au wanapokwenda kwenye kliniki. Na katika swali lake la msingi alisema wapewe ili kiwe kichocheo. Tungependa hicho kichocheo kianzie wanapokwenda kupima ujauzito ndiyo tunawapa. Itakuwa vigumu kujua nani yupo kijijini ambaye hajaenda kupima ujauzito na anajifungua itakuwa vigumu sana kuweza kumtambua na kumpa chandarua. Lakini akinamama wajawazito wanapokwenda kwenye Vituo vyetu na wakapima hapo ndipo wanapewa hiyo vocha na wanaweza kupata vyandarua kwa bei nafuu.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali ndogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, ndani ya nchi yetu malaria imekuwa ni tatizo sugu; na kwa kuwa Zanzibar tumefanikiwa kwa asilimia kubwa kutokomeza tatizo hili la maralia. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kukaa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuangalia ni taratibu gani zilizochukuliwa na Zanzibar za kutokomeza kwa asilimia kubwa tatizo hili la maralia ili zikatekelezwa Tanzania Bara? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa pande zote mbili zinahusiano wa karibu sana. Tunafuatilia kwa karibu nini kinatokea Zanzibar, na wao vilevile wanafuatilia nini kinatokea Tanzania Bara. Kwa hiyo, juhudi zote zilizofanyika mpaka ikawafikisha hapo tunazijua. Wametoa vyandarua bure.

Vilevile, wametumia dawa ya kupulizia inaitwa ikoni. Walipokamilisha hilo zoezi, hiyo dawa ilikuwa imebaki na sisi tukaichukua ndiyo tumekuwa tukiitumia Karagwe pamoja na Muleba. Kwa hiyo, tunajua nini kinatendeka na tunahusiana kwa karibu na nina imani yale yaliyotokea huko baada ya muda na sisi malaria itakuwa ni historia. *(Makofi)*

Na. 89

**Mapambano Dhidi ya UKIMWI**

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeamua kupambana na tatizo la maambuziki ya UKIMWI; na kuzuia unyanyapaa kwa watu wanaoishi na virusi hivyo; na kwa kuwa, Viongozi wa Dini na Siasa wana mchango mkubwa katika kuwashirikisha waumini na wananchi wao kukabiliana na changamoto hizo:-

Je, Serikali haioni kwamba, umefika wakati wa kuwawezesha Wabunge na kuwapatia vitendea kazi ili wasaidiane na Viongozi wa Dini ili kuharakisha kasi ya mpambano dhidi ya tatizo hilo Majimboni mwao?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdalla Khamis, Mbunge wa Magogoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya gonjwa la UKIMWI hapa nchini yanazingatia dhana ya ushirikishwaji wa wananchi, sekta na wadau mbalimbali katika ngazi zote. Wanaohusika ni kuanzia mtu mmoja mmoja, familia, Halmashauri, Serikali Kuu, Sekta zote, Wahisani , Mashirika na Asasi za Serikali na zisizo za Kiserikali na viongozi wa ngazi mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge pamoja na viongozi wengine ni wadau wakubwa katika mapambano ya UKIMWI. Kutokana na ukweli huo, Waheshimiwa Wabunge watarajiwa kushiriki kikamilifu katika mapambano hayo katika Majimbo yao na sehemu nyingine kwa kutumia zana na nafasi zilizopo.

Mheshimiwa Spika, afua muhimu yaani *intervention* kuliko zote katika pambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI ni kutoa elimu na ushawishi ili wananchi wabadili tabia na mienendo inayohusu ngono zembe. Hii inatokana na ukweli kwamba zaidi ya asilimia 80 ya maambukizi hapa nchini yanasababishwa na njia hiyo. Kwa nafasi aliyonayo Mheshimiwa Mbunge katika jamii, ushawishi kwa wananchi

waliomchagua una *impact* kubwa kwa kuwa walimwamini ndiyo maana wakamchagua. Vitendea kazi vilivyoombwa na Mheshimiwa Mbunge ni kumpatia ujuzi na elimu kuhusu suala nzima la mapambano dhidi ya UKIMWI. Hivyo tunawaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kujielimisha kuhusu ugonjwa huu pamoja na mikakati ya kuushinda ili waweze kujiamini yaani "*confident*" wakati wanawashawishi wapiga kura wao pamoja na kujibu maswali yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, kuna semina, kuna vipindi vya *Radio,* hapa Bungeni tuna Chama cha *TAPAC* na tuna Kamati ya Kudumu ya Bunge, zote hizo tuzitumie ili kuongeza uelewa wa mpambano huu na tuweze kujiamini tunapozungumza mbele ya wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba tuwe mstari wa mbele kushirikiana na Serikali na wadau wengine katika Majimbo yao katika kuhamasisha na kutekeleza afua za kudhibiti UKIMWI kwa kutumia rasilimali zilizopo.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, wafadhili wengi wa Mashirika ya Kimataifa wanapotusaidia katika Serikali ya Muungano; na kwa kuwa Tanzania ina Serikali mbili. Kwa upande wa Serikali ya Zanzibar. Je, Serikali ya Muungano ina utaratibu gani wa kusaidia moja kwa moja msaada huo ukafika Zanzibar unapotoka kwenye Taasisi za Kimataifa?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, Wahisani wanapotoa fedha za msaada wanaotoa kwa mradi ulioandikiwa. Kwa hiyo, unaandika mradi na kuonyesha hizo fedha unazihitaji kwa shughuli gani na wao ndipo wanapotoa. Wizara ya Afya ya Muungano inaangalia masuala ya upande moja, lakini kuna Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa upande wa Zanzibar. Hivi punde nimezungumzia habari za shughuli za kutokomeza malaria ambazo mradi uliandikwa na Zanzibar, *USAID* wakawasaidia.

Nadhani kulikuwa na wafadhili wengine, na hizo fedha na vile vyote walivyopewa vilikwenda Zanzibar, upande wa Tanzania Bara hatukupewa kwa sababu hatukuwepo katika yale maandiko.

Kwa hiyo, hakuna anayeleta fedha kwamba hizi fedha tunaleta kwa Serikali ya Tanzania, na itakavyotokea hivyo basi tutakaa na wenzetu tuangalie kwamba tuzigawe vipi? Lakini kwa sababu wanaleta kwa *specific activity* inabidi tuzitumie kwa hiyo *specific activity*.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa, tarehe 24 Julai, 2007 Mheshimiwa Rais alizindua kampeni ya upimaji wa hiari ya virusi vya UKIMWI na kuwezesha Watanzania zaidi ya milioni nne

na kuvunja rekodi dunia nzima kuweza kupima virusi vya UKIMWI katika muda mfupi? Kwa kuwa, siku hiyo ni muhimu sana. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ili kuenzi juhudi zilizofanywa na Mheshimiwa Rais, siku hiyo itengwe maalum kama siku ya UKIMWI ya Tanzania na kufanya wananchi wengi waendelee kutoa elimu ya UKIMWI na upimaji na kuoanisha na siku ya tarehe 1 Desemba, ambayo ni siku ya UKIMWI ya Kimataifa, tuwe na siku hiyo ambayo itakuwa siku ya UKIMWI ya Tanzania?

**SPIKA:** Swali la msingi lilikuwa ni maradhi ya Maralia.

**WABUNGE FULANI:** Ilikuwa ni UKIMWI.

**SPIKA:** Ohoo ilikuwa ni UKIMWI ehee.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Lo! Samahani sana nilipitiwa kidogo. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na ni mwanaharakati. Naomba nilichukue wazo hilo, linazungumzika, na sisi kama Serikali tutaliangalia kuona utekelezaji wake.

Na. 90

**Makato ya Kodi kwa Wafanyakazi**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Watanzania wanaofanya kazi rasmi hukatwa kodi moja kwa moja kutoka kwenye mishahara yao kila mwezi; na kwa kuwa, '*payslip*' huonyesha makato hayo ambayo hutofautiana kulingana na kiwango cha mshahara wa mfanyakazi:-

Je, kwa nini kila mfanyakazi asipewe *TIN* namba itakayomtambulisha kuwa ni mlipa kodi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzisha namba ya utambulisho wa mlipakodi (*Taxpayer Identification Number (*TIN*)* ni kwa ajili ya kuwatambua walipakodi nchini pamoja na shughuli zao, na namba ya mlipa kodi hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya

Kodi ya Mapato. Wafanyakazi wanatambuliwa kutokana na namba wanazopewa waajiri wao.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

(a)Miaka yote wafanyakazi wanalipa kodi kupitia mishahara yao kila mwezi. Kwa nini zoezi hilo la kuwatambua halijafanyika mpaka leo au swali langu ndiyo limeishtua Serikali kwamba kuna umuhimu wa kufanya hivyo?

(b) Je, ni lini zoezi la kuwatambua na kupatiwa hizo *Tax Identification Number* litafanyika, kwa sababu hajatupa *timeframe*?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wafanyakazi katika Sekta Rasmi ambao wanalipwa mishahara mwisho wa mwezi hawapewi *TIN* kwa sababu wale waajiri ndiyo walioandikishwa kama walipakodi, na katika kuandikishwa kule kila mwezi wanatakiwa wapeleke *returns* ambazo zinaonyesha orodha ya wafanyakazi wao. Kwa hiyo, kwa kweli hakuna haja ya kuwaandikisha wao mmoja mmoja. Isipokuwa Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania inaendelea na usajili wa wafanyakazi na wafanyabiashara kwenye Sekta isiyo rasmi ili hatimaye tufike mahali ambapo kila Mtanzania anayefanya kazi ama anayefanya biashara analipa kodi.

Na. 91

**Mpango wa Utoaji Ruzuku ya Mbolea Mikoani**

**MHE. JENISTA J. MHANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu sana Serikali imeendelea kutoa ruzuku kwa ajili ya pembejeo ya mbolea; na kwa kuwa, imeonekana kuwa ruzuku hiyo bado haijawanufaisha wakulima wengi vijijini:-

(a)Je, Serikali inatambua vikwazo vinavyosababisha kutofanikiwa kwa mpango huo wa ruzuku ya mbolea na hasa kwa Mkoa wa Ruvuma na Jimbo la Peramiho na ni hatua zipi zilizochukuliwa kuondoa vikwazo hivyo?

(b)Je, kuna mifano halisi ya mafanikio kwenye Jimbo la Peramiho katika kutatua vikwazo hivyo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Utaratibu uliotumiwa kusambaza mbolea ya ruzuku katika misimu mitatu iliyopita Mkoani Ruvuma na katika Mikoa mingine, ilikutana na vikwazo vifuatavyo:-

Licha ya mbolea kufikishwa katika maghala yaliyoteuliwa katika Mikoa mbalimbali ukiwemo Mkoa wa Ruvuma, palijitokeza udhaifu wa usimamizi wa Kamati za Pembejeo katika ngazi ya Wilaya katika kusimamia na kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima kwa wakati.

Aidha, mawakala walioteuliwa kufikisha mbolea hiyo vijijini baadhi yao hawakuwa na uwezo wa kifedha wa kuwawezesha kununua na kusafirisha mbolea hadi vijijini. Mbali na udhaifu wa kifedha, baadhi ya Mawakala walificha mbolea ya ruzuku, kwa nia ya kuiuza kwa bei kubwa kutokana na kuwepo bei mbili katika soko moja, yaani bei ya mbolea ya ruzuku, na bei ya soko. Ili kupambana na vikwazo hivyo, hatua kadhaa zilichukuliwa Mkoani Ruvuma ili kurekebisha kasoro kama ifuatavyo:-

Kila kata ilitakiwa na hivyo kuteua wakala mmoja aliyeteuliwa na Baraza la Maendeleo la Kata na kuingia mkataba na Wilaya. Hatua hii ilisaidia kufikisha kiasi cha mbolea licha ya kuwa mbolea yenyewe ya ruzuku haikuwa ya kutosheleza mahitaji. Hatua hizi, zilisaidia kufikisha na kuwauzia mbolea kwa bei iliyopangwa na Kamati ya Wilaya. Mafanikio makubwa zaidi yalipatikana pale *SACCOS* zilipokuwa zimepewa uwakala.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na matatizo hayo, Serikali inakusudia kubadilisha mfumo wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima kuanzia msimu ujao wa kilimo. Ruzuku itakwenda moja kwa moja kwa mkulima, kwa njia ya vocha kwa wakulima watakaoteulilwa na Serikali ya kijiji, badala ya utaratibu wa zamani ambapo ruzuku ilikwenda kwa makampuni yaliyosafirisha mbolea.

Mawakala watakaotoa huduma hizi chini ya utaratibu huu, wamepewa mafunzo na pia wataunganishwa na Benki ya *NMB* ili kuwezesha kupata mikopo ili kuondoa udhaifu uliojitokeza, huko nyuma. Maelezo zaidi kuhusu mfumo huu mpya utaelezwa kwa kirefu na kwa kina katika hotuba yangu nitakayoiwasilisha hapa Bungeni hivi karibuni.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa asilimia 80 ya wananchi wa Jimbo la Peramiho ni wakulima, na ni wakulima wakubwa wanaotegemewa na Taifa katika kuzalisha chakula na hasa chakula cha hifadhi. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuniambia katika huo mfumo wake wa sasa wa vocha ni vigezo gani vitatumika katika kuwateua wakulima wanaostahili kupata hiyo ruzuku na wasiostahili kupata hiyo ruzuku, angalau aniambie vigezo vitatu tu ili nianze kufahamu hilo?

La pili, lakini vilevile kwa kuwa; katika majibu ya msingi amekiri kabisa kwamba *SACCOS* zilifanya kazi nzuri sana ya kusambaza mbolea katika mfumo huo wa ruzuku.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuna umuhimu sasa Serikali kusikiliza matakwa ya wakulima ya kutumia *SACCOS* zao kama ndiyo Mawakala wa kusambaza mbolea hiyo ya ruzuku na siyo kuendelee kufuata tu mipango ambayo haitokani hasa na matakwa ya wakulima hao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Mbunge hataki kusubiri ufafanuzi wa hotuba yako baadaye anataka jibu. Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, la kwanza, vigezo gani vitatumika ni kwamba mkulima huyo lazima atambuliwe na kijiji chake kwamba ni mkulima, anayo ardhi, kwa sababu kijijini kuna watu wengine ambao wanaishi pale lakini hawana ardhi, kwa hiyo si wakulima.

Hii tunafanya hivyo, kwa sababu lazima vocha ile iandikwe kwa jina la mkulima, na mkulima huyo sifa yake ni kwamba anayo ardhi lakini hana uwezo wa kununua mbolea. Hiyo ndiyo sifa kubwa ambayo inaiwezesha Serikali kum-*support*. Hilo ndilo sifa kubwa kwa kweli awe mkulima hana uwezo. Kwa hiyo, tunamsaidia ili uwezo wake uongezeke kwa kuweza kupata mbolea na aweze kuzalisha zaidi na kuondokana na umaskini, na vilevile kuchangia katika kuzalisha chakula kwa ajili ya watanzania wote.

La pili, tunatilia mkazo *SACCOS* kuwa Wakala, na kwa kweli mahali ambapo *SACCOS* ipo tunaitilia mkazo ijiorodhesha ili na yenyewe iwe Wakala, iingie kwenye mafunzo na iwezeshwe kupata mikopo ili iweze kununua hiyo mbolea na kuifikisha kwa wakulima. Sisi Wizara yetu inatu-*promote* Ushirika na *SACCOS* ni Ushirika. Kwa mahali pale ambapo Ushirika unafaa kufanya kazi hiyo tunatilia mkazo zaidi Ushirika kuliko vinginevyo.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, tatizo la kutokuwa na mbolea ya kutosha Mkoani Ruvuma sasa limekuwa ni mbolea isiyokuwa na viwango. Mwaka jana msimu uliopita baadhi ya Kampuni siyo *TFC* zilituuzia mbolea isiyokuwa na kiwango, na baadhi ya wakulima hasa wa Wilaya ya Namtumbo walilalamikia hilo, na Serikali ya Mkoa ilichukua hatua ya kuifanyia utafiti. Je, Serikali Kuu inalifahamu hilo, na inachukua hatua gani ili lisitokee tena kupelekewa mbolea isiyokuwa na viwango?

**SPIKA:** La! Pole sana. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulipokea malalamiko aliyoyaeleza na tulikielekeza Kituo cha Uyole cha

Utafiti kuchukua sehemu ya mbolea iliyolalamikiwa kuipima na kutoa ushahidi kama kweli ilikuwa haina viwango.

Matokeo ya utafiti tuliyoyapata yalidhihirisha kwamba mbolea ile ilikuwa na viwango. Kwa hiyo, tulipata tabu kuweza kujua msingi hasa wa malalamiko ilikuwa ni nini? Lakini tunaendelea kufanya utafiti kwa sababu utafiti si kitu kinachochukua siku moja ili kujua hasa sasa aina gani ya mbolea inayofaa kwa Mkoa wa Ruvuma.

Maelezo tuliyoyapata hivi karibuni yanasema watu wa Ruvuma wangependelea zaidi kutumia aina ya mbolea ya Kani, na sisi tunafikiria kuiweka Kani katika mfumo wa ruzuku ili iweze kutumika katika Mkoa huo. *(Makofi)*

Na. 92

**Kujenga Jengo la Mahakama**

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mahakama ni moja ya Mihimili mitatu ya nchi, na kwa kuwa, Mahakama haina jengo zuri ikilinganishwa na Mihimili mingine yaani Serikali na Bunge:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga jengo linalolingana na hadhi ya Mhimili wa Mahakama?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Mahakama ya Tanzania kama Mhimili mwingine wa nchi haina jengo zuri ikilinganishwa na Mihimili mingine yaani Serikali na Bunge. Serikali imechukua hatua za awali za kuanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama. Kiwanja kimepatikana tarehe 19 Oktoba, 2007 Dar es Salaam karibu na Hoteli ya Holiday Inn. Aidha, fedha zimepatikana chini ya Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria (*Legal Sector Reform Programme)* na ujenzi wa jengo la kudumu la Mahakama ya Rufani Tanzania, utaanza wakati wowote kuanzia sasa.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

La kwanza, kwa kuwa, lengo la Serikali ni kuhamishia Makao Makuu Dodoma kwa nini sasa Jengo la Makao Makuu ya Mahakama lijengwe Dar es Salaam? *(Makofi)*

La pili, kwa kuwa, Mahakamani ya Rufaani ni jambo la Muungano. Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Ofisi ndogo kule Zanzibar kama ilivyokuwa Ofisi ya Bunge?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, la kwanza, tunajenga Makao Makuu ya Mahakama Dar es Salaam si kwa sababu hatutambui kwamba Makao Makuu ya nchi yetu ni Dodoma.

Lakini si lazima kila kitu kijengwa Dodoma, tungechagua Arusha vilevile ingewezakana tu,. Hata hivyo, mjadala wa kuhamia Dodoma kama mlivyomsikia jana Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiyo unaanza.

Kwa hiyo, tuache mjadala huo uendelee pengine tutapata maamuzi tofauti. La pili, suala la kujenga Ofisi Ndogo Zanzibar linazungumzika, nafikiri nitashauriana na Mahakama tuone kama uwezekano huo utakuwepo. Nashukuru sana.

**MHE. HAMAD R. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja ndogo la nyongeza. Je, Serikali inataka kutuambia kwamba ile Sera ya kuhamia Dodoma inakuwa *revised* sasa na kwamba tunataka kuijadili tena upya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Swali hili linatokana na maelezo yako. Kwa hiyo, ninaliruhusu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, Sera ya kuhamia Dodoma msimamo wa Serikali upo pale pale, bado Serikali itahamia Dodoma.

Kwa hiyo, sidhani kama sera hiyo imebadilika. Nafikiri kinachojaribu kuzungumzwa hapa ni utekelezaji wake tu lakini uamuzi ni ule ule.

Na. 93

**Hitaji la Makambi ya Barabara**

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Mkutano wa Nane wa Bunge, Wabunge wengi walitoa mawazo ya kurudisha Makambi ya barabara kama njia mojawapo ya kuzisimamia barabara zetu kwa makini zaidi hususan zile za udongo na changarawe:-

(a) Je, kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi katika kutekeleza jambo hili?

(b) Kama Serikali haina kigugumizi; je, ni Kambi ngapi zimeanzishwa au zitaanzishwa katika mwaka wa fedha 2008/09?

(c) Kwa kuwa, katika Kijiji cha Mngeta Wilayani Kilombero kuna miundombinu yote inayohitajika (barabara ya Ifakara-Mlimba-Taweta); je, Serikali itakuwa tayari kumweleza Mkandarasi atakayepewa barabara hiyo kuweka Kambi Mngeta kwa kuwa ni katikati ya barabara ya Ifakara-Mlimba?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mbunge wa Kilombero lenye sehemu (a), (b) na (c) pamoja na masahihisho kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliokuwepo huko nyuma wa Serikali kuwa na Makambi ya kusimamia barabara ulitumika wakati huo ambapo ujenzi, matengenezo na usimamizi wa barabara ulikuwa unatekelezwa na Serikali yenyewe. Baada ya mabadiliko ya Sera za Ujenzi wa barabara nchini, Serikali ilijiondoa kwenye jukumu la moja kwa moja la utekelezaji wa ujenzi na matengenezo ya barabara na hivyo kubakiwa na jukumu la usimamizi tu. Jukumu hilo la usimamizi linahusisha tathmini ya ujenzi na matengenezo yanayotakiwa kufanyika, uandaaji wa nyaraka za zabuni, utangazaji na utoaji wa zabuni (*award of contracts*) na kusimamia wakandarasi kuhakikisha wanatekeleza kazi ipasavyo kulingana na mikataba yao. Kutokana na mabadiliko hayo, jukumu la ujenzi na matengenezo ya barabara liliachiwa makandarasi wa kuajiriwa na Serikali na hivyo kuifanya Serikali kutokuwa na haja ya watumishi wa kudumu waliokuwa kwenye Makambi hayo.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na hali hiyo, Serikali iliamua kuyafunga makambi hayo na hivi sasa Serikali haina mpango wowote wa kuyajenga Makambi hayo pamoja na mawazo mazuri yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikiwakabidhi wananchi wanaoomba Makambi yanayojengwa na Makandarasi kwenye barabara wanazozijenga kwa matumizi mengine ya kijamii kama vile shule na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara ya Ifakara-Mlimba hadi Tawete yatakapokamilika mkandarasi atakayepatikana kuijenga barabara hiyo atashauriwa na Serikali awasiliane na uongozi wa Kijiji cha Mngeta ili kubaini eneo la muafaka na kujenga kambi ambayo inaweza kutumiwa na wanakijiji baada ya ujenzi wa barabara hiyo kukamilika.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza katika Bunge hili tunakuwa tunapitisha bajeti kwa ujenzi wa barabara kwa viwango viwili yaani barabara ya changarawe na barabara ya lami. Je, Wizara ya Miundombinu sasa itakuwa tayari kupitisha kuongeza kiwango kingine cha barabara ya udongo badala ya viwango hivi viwili? Kwa sababu kinachotokea kule ni kutengeneza barabara za udongo.

Pili, je ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kuanza kujenga barabara ya Ifakara hadi Mahenge kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidi katika Bunge la bajeti la mwaka 2006?

**NAIBU WAZIRI MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Sera ya Ujenzi ya barabara katika viwango viwili vya changarawe na lami napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara za changarawe, lami pamoja na za udongo zote zinatumika hapa nchini.

Kwa hiyo, katika suala la kuidhinisha makadirio niseme tu kwamba makadirio tunayopitisha hapa Bungeni yanaelekezwa kwenye kujenga barabara hasa ikikumbuka kwamba kwa mfano asilimia 30 inayopelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya ambako ndiko kwenye barabara nyingi za udongo fedha hizi zinatumika kuhudumia barabara za udongo. Kwa hiyo uidhinishaji wa bajeti unahusu ujenzi wa barabara zote za changarawe, lami pamoja na udongo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara ya Kidatu kwa kiwango cha lami. Naomba tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira kwamba wiki ijayo tutawasilisha hotuba yetu ya bajeti hapa Bungeni tutafafanua barabara mbalimbali zitakazokuwa zipo tayari kujengwa kutegemea na uwezo wa Serikali na fedha tutakazoidhinishiwa katika kipindi hiki cha bajeti.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali ndio umepita kidogo na maswali yamekwisha. Matangazo nitaanza na wageni.

Kwa heshima na taadhima kubwa naomba niwatambulishe Wazee wetu, Waasisi wa Chama cha Mapinduzi. Kwanza nitawasumbua kidogo wazee kwa utaratibu mnatakiwa ukitajwa kama una uwezo basi usimame labda kama hujisikii vizuri. Lakini nadhani mna afya njema. Mzee Pancras Ndejembi, Mwenyekiti wa Wenyeviti Wastaafu wa CCM. Yule pale. Ahsante mzee tunashukuru sana kwa kazi yako naona bado unapiga tai na koti vizuri, suti safi sana, ahsante sana. (*Makofi)*

Wa pili ni mzee Hassan Nassor Moyo. Karibu sana mzee, tunakushukuru sana sana na tunawashukuru kwa kuja kufuatilia shughuli zetu za Bunge hapa. Wa tatu ni meja Jenerali Mstaafu Said Natepe. Bwana askari ni askari tu, tazama mzee

alivyosimama vizuri kabisa wima kabisa. Karibu sana Jenerali Mstaafu Natepe. *(Makofi)*

Wa nne ni Mzee Nnko Mwenyekiti Mstaafu wa CCM Arusha. Naona ana udhuru kidogo lakini tutampa salamu zake. Wazee wetu tunawashukuruni sana na bado tunaendelea kuenzi kazi kubwa sana mliyoifanya na hata kuwepo kwa ukumbi huu ni matokeo ya matunda ya kazi yenu. Ahsante sana. (*Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Gosbert Blandes ni mkewe Golora Blandes naomba asimame. Yule pale. Karibu sana. Wanawe Comfort Blandes na Boniface Blandes wote wakiwa ni wanafunzi wa Sekondari. Karibu sana na nyie mnaosoma tunawatakia mafanikio katika masomo yenu.

Wageni wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini ni wazee 17 ambao walitembea kwa miguu toka Musoma mpaka Butiama na kupokelewa na Rais mnamo Februari, 1968. Naomba wasimame wazee wa Musoma. Ohoo wale pale loo!!! Ahsante sana. (*Makofi)*

Tunawashukuru kwa kitendo chenu hicho na pia kwa kuja kushuhudia shughuli za Bunge. Miongoni mwao 4 walitembea kwa mguu mwaka 1967 toka Musoma mpaka Dar es Salaam, ningeomba wale 4 waliokwenda Dar es Salaam kutoka Musoma kwa miguu maana yake walitembea na Baba wa Taifa. Ohoo wazee alalalalah!!!!!

Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Musoma Mjini kwa kutuletea hisia za kihistoria za jambo kubwa kama hili. Ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 50 kutoka Shule ya Jamhuri Sekondari na walimu mkono wangu wa kushoto nadhani. Naomba msimame walimu na wanafunzi Jamhuri Sekondari Dodoma. Ahsante sana. Tunaomba mfanye vyema katika masomo na walimu muendelee kuwalea watoto wetu. Ahsante.

Mheshimiwa Fatma Maghimbi ametembelewa na wajukuu zake wawili Nasri Habib sijui yuko wapi Nasri? Yule pale mkono wa kushoto. Ahsante sana na Karima Abood. Karima yule pale ahsante sana karibuni sana. Mkionaona mambo haya mnaweza mwisho mkafuata nyayo za bibi si jambo baya.

Kwanza niwakumbushe tu kwamba tuna nyongeza ya Orodha ya Shughuli za Leo nalo ni kauli ya Waziri ambayo ni ya Waziri wa Fedha na Uchumi. Kwa hiyo, nitakapomaliza matangazo tutaendelea na hilo. Nilikuwa nawakumbusha hili ili muelewe wale ambao hamjapata imetawanywa sasa hivi *Supplementary Order Paper*.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini anahitaji wajumbe wake wote wa Kamati ya Nishati na Madini mkutane saa 5.00 asubuhi ukumbi Na. 227 jengo la Utawala.

Mheshimiwa Abdisalaam Khatib, Mwenyekiti Kamati ya Viwanda na Biashara anawahitaji wajumbe wote wa Kamati ya Viwanda na Biashara mkutane leo saa 5.00 asubuhi ukumbi Na. 231. *(Makofi)*

Mheshimiwa Anne Makinda, Naibu Spika kwa nafasi yake kama Mwenyekiti wa Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote *(TWPG)* anaomba leo saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Msekwa Wabunge wote wanawake mkutane hapo kwa kikao kifupi lakini muhimu sana.

Watu wamechelewa hapa kuna wageni wengine hawakusahaulika hawakuorodheshwa tu ndio wameleta sasa hivi kutoka Kanisa la Biblia wanaitwa *EMMAUS* ningeomba wasimame wale wa kutoka Kanisa la Biblia. Wale pale karibuni sana, ahsante sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mwenyekiti wa *APNAC* Tanzania anaomba leo saa 5.45 wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji ya *APNAC* wanaharakati wa kupambana na rushwa mtakutana na Waheshimiwa Wabunge wageni wetu kutoka Denmark saa 5.45 leo chumba namba 219.

Kwa hiyo, Kamati ya Utendaji ya *APNAC* saa 5.45 chumba namba 219 kwa kukutana na Wabunge kutoka nchi ya Denmark.

Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi anaomba wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi mkutano saa 5.00 katika ukumbi Na. 428.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Takwimu za Hotuba ya Waziri wa Fedha Bajeti 2008/2009

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, wakati wa mjadala wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2008/2009 hapa Bungeni tarehe 16 mpaka 20 Juni, 2008 baadhi ya vyombo vya habari hususan baadhi ya magazeti yaliandika habari za maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu bajeti ambazo zinahitaji ufafanuzi ili kutoa picha sahihi ili wananchi na wadau wengine wa Bajeti za Serikali wapate ufahamu wa kweli wa mambo yaliyokuwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza linalohitaji ufafanuzi ni kuhusu habari zilizoandikwa na magazeti kadhaa kwamba takwimu za bajeti zimetofautiana na hata wengine kudiriki kuiambia Serikali ijiuzulu kwa kuwasilisha Bungeni bajeti isiyokamilifu. Mahali pa kuanzia katika kutoa ufafanuzi kuhusu jambo hili ni kukumbusha kwamba bajeti ya Serikali ya mwaka 2008/2009 ilipitishwa na Bunge lako Tukufu tarehe 20 Juni, 2008 kwa zaidi ya theluthi mbili ya Wabunge. Aidha, hakuna Mbunge hata mmoja aliyepiga kura ya hapana bali wachache hawakutaka kupiga kura ya ama “Ndio au Hapana”.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kura ya Wabunge ni kielelezo tosha kwamba bajeti iliyowasilishwa na Serikali Bungeni ilikuwa sahihi na kwamba maswali yaliyoulizwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu takwimu ni sawa na maelezo ya Serikali pia yalikuwa sahihi na hasa baada ya Kamati ya Fedha na Uchumi kujadili na kuridhia takwimu hizo.

Mheshimiwa Spika, maelezo zaidi kuhusu jambo hili ni kama ifuatavyo. Mapendekezo ya bajeti ya Serikali yanaainishwa katika hotuba ya bajeti na katika vitabu vya bajeti 4, kitabu cha kwanza hadi cha 4. Aidha, kwa upande wa mapato kuna Muswada wa Sheria ya Fedha ambao ni sehemu ya bajeti.

Baada ya Serikali kuwasilisha mapendekezo yake ya mwaka Bunge linajadili na kutoa ushauri na mapendekezo mbalimbali ambayo ni pamoja na kupendekeza marekebisho kadhaa katika bajeti iliyowasilishwa na Serikali. Hatimaye Bunge linapitisha Mpango wa Bajeti pamoja na *Finance Act* na *Appropriation Act* ambazo zinaidhinishwa mwisho wa shughuli za Bunge la Bajeti.

Kwa hivyo vitabu vyote vya bajeti vinavyowasilishwa Bungeni vinafanyiwa marekebisho yanayostahili yanayopendekezwa na Waheshimiwa Wabunge na hatimaye zinatolewa nakala mpya ambazo zina takwimu za makadirio ya mapato na matumizi yaliyoidhinishwa na Bunge, utaratibu huu ni wa kawaida na unafanyika miaka yote.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya hakuna maajabu kuona kwamba takwimu za bajeti za Serikali zinarekebishwa wakati wa Bunge la kujadili bajeti hili ni jambo la kawaida. Marekebisho yanafanyika hasa katika makadirio ya mapato na Serikali na hili ndilo linalotokea ambalo baadhi ya magazeti yameliandikia kwa kirefu. Serikali inarudia tena kusema kwamba hakuna takwimu za bajeti ambazo hazikuwa sahihi na bajeti iliyoidhinishwa ndiyo iliyowasilishwa hapa Bungeni na kusomwa na Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya mapato ya Serikali hasa mapato ya ndani ni vingi. Kwa mfano mwaka wa fedha 2008/2009 baada ya kitabu cha kwanza kupelekwa kwa Mpiga Chapa zilipatikana taarifa mpya kuhusu makadirio ya mapato ya mauzo ya hisa asilimia 21 za Serikali katika *NBM.*

Awali tulipewa makadirio ya shilingi 42 bilioni kisha yakarekebishwa na kufikia shilingi 58 bilioni na zikapanda tena siku za mwisho yakawa shilingi 60 bilioni. Kwa kuwa taarifa ya mwisho ilikuja baada ya vitabu vya bajeti kupelekwa kwa Mpiga Chapa na baada ya hotuba ya Bajeti kuandikwa na kuchapishwa kiasi hiki cha shilingi 60 bilioni hakikuonyeshwa bali kimeingizwa katika masahihisho yaliyoitwa *addendum.*

Mheshimiwa Spika, fedha zinazotokana na msamaha wa madeni ya IMF yaani *MDRI* hazikuwa zimejumuishwa katika orodha ya misaada na mikopo ya nje katika kitabu cha kwanza, lakini zilikuwa katika hotuba yangu ya bajeti.

Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walitaka ufafanuzi kuhusu fedha za ndani za matumizi ya maendeleo ya shilingi bilioni 938. Kwa ufafanuzi fedha za ndani kwa ajili ya matumizi ya maendeleo zinajumuisha vyanzo vikuu vifuatavyo. Moja misaada ya bajeti *General Budget Support.* Pili fedha za ubinafsishaji, tatu albaki kutoka kwenye bajeti ya kawaida na nne msamaha wa deni la *IMF MDRI. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo ni kwamba misaada ya bajeti yaani *GBS* inahesabiwa kuwa ni sehemu ya fedha za ndani kwa sababu fedha za *GBS* zinaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na zinachanganywa na mapato yetu wenyewe hivyo zinahesabiwa kama fedha za ndani. Zikichangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali hazina tena tofauti na zile zilizokusanywa na *TRA* na vyombo vingine vya ndani.

Msamaha wa madeni pia unahesabika kama fedha za ndani kwa ajili ya bajeti ya maendeleo kwa kuwa deni likifutwa maana yake Serikali inaokoa fedha ambazo ingetumia kulipa deni hilo lililofutwa. Hivyo basi kiasi cha deni lililofutwa linahesabiwa kama fedha za ndani kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

Serikali inatumaini kwamba maelezo haya yatasaidia katika kuwataarifu wananchi kwamba bajeti ya Serikali ya Mwaka 2008/2009 haikuwa na tatizo la msingi la takwimu kiasi la kulifanya liwe jambo kubwa linaloweza kutoa picha tofauti kwa jamii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda pia kutoa ufafanuzi kuhusu maelezo iliyoyatoa Bungeni tarehe 20 Juni, 2008 wakati nikijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhitimisha mjadala wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, nilisema kwamba akaunti ya *EPA* ilitokana na akaunti ya Wafanyabiashara wa Tanzania zilizokuwa katika iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara ambao katika miaka ya 1980 walikopa kutoka nje ya nchi malighafi za viwanda, vipuri na zana zingine za uzalishaji kwa njia ya *suppliers credit.*

Wengi wa wafanyabiashara hao walilipia madeni yao kwa shilingi ya Tanzania kupitia akaunti zao katika iliyokuwa *NBC* lakini Benki hiyo ilishindwa kuwalipa wadai wa nje kwa kukosa fedha za kigeni ambazo zilikuwa adimu hapa nchini wakati huo.

*NBC* ilipoanza kurekebishwa mwanzoni mwa miaka ya 1990 iliamuliwa kwamba akaunti hizo zihamishiwe Benki Kuu na ikafunguliwa akaunti Benki Kuu iliyoitwa *External Payments Arears* kwa kifupi *EPA.*

Benki Kuu ilipewa jukumu la madaraka ya kuhakiki madai ya Kampuni za Nje zilizokuwa zinaidai Kampuni za Tanzania kupitia NBC ili iweze kubaini zile ambazo zilistahili kulipwa.

Kwa hivyo ni wazi kwamba fedha hizo zilizokuwa kwenye akaunti ambazo zilihamishiwa Benki Kuu kutoka *NBC* ya zamani hazikuwa fedha za Serikali. Narudia hazikuwa fedha za Serikali bali ni za Makampuni hayo binafsi na Benki Kuu ilikuwa wakala tu wa kuyahakiki madeni hayo.

Kwa maelezo haya hakuna mantiki ya kuhoji kwa nini fedha za EPA hazikuwekwa kwenye bajeti ya Serikali kwa sababu hazikuwa fedha za Serikali. Hii ndiyo historia haitafutika na huo ndio ukweli. Waliopata fedha hizo kwa njia zisizo halali hawana uhusiano wowote na wale waliokuwa wanaidai *NBC*. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nikihitimisha hotuba yangu nilisema yafutayo nanukuu. "Kuhusu *EPA* ningependa kukumbusha kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania aliteua Kamati Maalum iliyojumuisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama Mwenyekiti, *Inspector General* wa Polisi na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU.

Kamati hiyo imepewa muda wa miezi 6 kukamilisha kazi iliyopewa. Kamati itawasilisha taarifa yake kwa Rais ambaye ataamua hatua za kuchukuliwa".

Mheshimiwa Spika, kwa maneno haya mimi sikutamka kwamba waliohusika na fedha za *EPA* hawatachukuliwa hatua bali hatua zitachukuliwa baada ya Mheshimiwa Rais kupokea taarifa ya Kamati Maalum na kuagiza utekelezaji wake.

Kwa hivyo hakuna mahali popote ambapo mimi kama Waziri wa Fedha na Uchumi nililiongopea Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi huo. Waheshimiwa Wabunge kulikuwa na matangazo ambayo nimeletewa nadhani kutokana na karatasi nyingine kuja sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa *LAAC* Dr. Slaa anasema sasa hivi ni Mkutano ule na wale wageni kutoka Denmark ambao wamepangiwa ratiba kumbe na Kamati mbalimbali. Kwa hiyo, wametoka sasa hivi wale wote wa Kamati ya *LAAC* ambao bado wamo ukumbini hapa wanaombwa wakakutane na wale wageni.

La pili, lilikuja mapema sana ili nilighafirika. Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya Nje, Ulinzi na Usalama wakutane saa 5.00 hii katika ukumbi namba 432 jengo la Utawala. Inaelekea leo tutabaki wachache sana maana yake mikutano mingi ni saa 5.00 lakini ndiyo kazi za Bunge zinavyokwenda.

## Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2008/2009 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama alivyokwishatangaza jana Mheshimiwa Naibu Spika, orodha hii ni kielelezo tu cha jinsi majina yalivyokuja. Lakini kiti tunaruhusiwa kupanga ili kuzingatia mjadala ambao una uwiano unaozingatia uwakilishi tulivyo humu, jinsia, upinzani na kadhalika na hata rika mara nyingine. Kwa hiyo usione umerukwa ukasema tunakuonea hapana, ni namna ya utaratibu.

Wa tatu wanaoanza kwanza ni Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mbunge wa Rombo, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mbunge wa Buchosa, nitaje na wa nne ni Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mbunge Viti Maalum. Nitaanza na Mheshimiwa Basil Mramba. *(Makofi)*

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ili niweze kuchangia hotuba nzuri sana ya jana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naanza kwa kusema kwamba naiunga mkono hotuba hiyo ambayo kwa maoni yangu ilikuwa nzuri, *balanced* na yenye mambo mengi ya kutafakari na kuzingatia. *(Makofi)*

Ningependa nianze na suala la barabara. Niseme kwamba kwanza niishukuru Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba katika Wilaya yangu ya Rombo ametaja kilomita 32 ambazo zimetengenezwa kwa kiwango cha lami na vipande vingine vya barabara zinaendelea kutengenezwa. Wananchi wa Rombo wamenituma niishukuru sana Serikali kwa kuendelea kuitengeneza barabara hiyo hasa kwa kuiwezesha Wilaya ya

Rombo kuunganishwa na nchi ya Kenya ambayo ndiyo ilikuwa mojawapo ya madhumuni na kwamba muda si mrefu itawezekana kwenda Nairobi kupitia Tarakea, tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa mjadala wa Wizara ya Fedha, mjadala wa Bajeti tulisikia vilio vya Wabunge wengi wengi hasa wa Magharibi mwa Tanzania kuhusiana na barabara. Mimi ningesema naunga mkono vilio hivyo kwamba wakati umefika kwa Magharibi ya Tanzania kuwa na barabara za kuaminika.

Kwa kweli sio sahihi kusema kwamba tuwaonee huruma kuna baadhi ya Wabunge waliokuwa wanasema unajua na Waziri Mkuu yuko huko. Kwa hiyo, tuwaonee huruma tuone namna ya kumsaidia! Hapana, wanastahili barabara, sio kuonewa huruma, wanastahili. *(Makofi)*

Naelewa tatizo la fedha, nalielewa sana, lakini kuna njia nyingi za kupata fedha. Tukisubiri akina *Millenium Challenge* au fedha zetu za ndani itafika mwaka 2020 kabla ya barabara hizo zilizotajwa za Magharibi ya Tanzania hazijatengenezwa.

Kwa hiyo lazima tutafute njia nyingine za dharura za kutengeneza barabara hizo ikiwa ni pamoja na ile ya kuanzia Mto wa Mbu kuelekea Mkoa wa Mara Mugumu ambayo pia nayo ni barabara muhimu lakini haina fedha.

Mheshimiwa Spika, nilibahatika kuhudhuria Mkutano ule wa wa China na nchi za Kiafrika mwaka jana. Wachina wamesema njooni tuna fedha za kusaidia miundombinu huko kwenu kwa utaratibu wa mikopo nafuu sana.

Mimi napendekeza kwamba kwa njia ya dharura tuwekeze kwenye barabara zetu, baadhi ya viwanja vya ndege ili tuweze kutumia mikopo hiyo nafuuu ya Kichina.

Mheshimiwa Spika, ziko fedha Benki ya Dunia, ingawa najua wale wanachukua muda lakini zipo. Zipo fedha kwenye nchi nyingine kama tukizungumza nao vizuri ambazo zingeweza zikatumika kidharura kupata njia mbadala ya mapato.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni miaka mitatu au minne sasa, hapa ndani tunazungumza habari za *BOT (Build Operate and Transfer).* Tunazungumza tu, hata mimi kwenye bajeti yangu moja nilisema tutatumia utaratibu wa *BOT*, hatujafanya, tunazungumza tu.

Mheshimiwa Spika, Sheria tuliyoipitisha hapa mwaka jana, ile Sheria ya Barabara, ina kipengele kinachoruhusu kutengeneza barabara kwa utaratibu wa *BOT*. Kwa hiyo, hakuna tatizo la Kisheria, tatizo ni uamuzi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba barabara zote zile ambazo, wale tuliohudhuria ile semina ya juzi Jumamosi, zilitamkwa barabara fulani; zile na nyingine

za namna hiyo, tuzitafutie watu binafsi wa kuzitengeneza kwa utaratibu wa *BOT* na njia kama hizo za kibiashara, nusu kibiashara na nusu ubia hata Serikali inaweza ikaingia ubia.

Mheshimiwa Spika, lakini natoa tahadhari, tusitengeneze barabara hizo kubwa bila kuzingatia bandari. Haitakuwa jambo la maana kutengeneza barabara kama hatutengenezi bandari.

Mheshimiwa Spika, najua inawezekana pia tukapata watu binafsi wa kutusaidia kutengeneza bandari ya Mtwara, Tanga na Dar es Salaam ili tukaondokana na tatizo hili la bandari maana hata ukifuatilia majadiliano yaliyopo hapa, mambo ya *TICTS,* ni hili hili tu la bandari finyu! Ukishakuwa na bandari finyu na vitu vingine vinakuwa finyu, kwa hiyo, unapata matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napendekeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, badala ya kusubiri uonewe huruma, afadhali ulivalie njuga jambo hili la barabara ambazo zimebaki. Tuzitengeneze kwa utaratibu maalum ili nchi hii iweze kuwa moja, tusipofanya hivyo, utatokea mpasuko.

Mheshimiwa Spika, (b) yake…

**SPIKA:** Kabla hujaliacha hilo, nilivutiwa sana uliposema barabara za Magharibi, hii si pamoja na barabara Manyoni –Itigi –Tabora –Urambo mpaka Kigoma, si ndiyo hivyo?

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Spika, nazungumzia barabara ya Manyoni – Itigi –Tabora –Malagarasi mpaka Kigoma. Nazungumzia barabara ya Tunduma – Sumbawanga, sasa ina mfadhili lakini tuanzie Sumbawanga - Mpanda – Uvinza - Kigoma kuelekea Kasulu Kibondo. Nazungumzia barabara hii ya Makuyuni - Mugumu na barabara nyingine za hapa katikati ya nchi kwa mfano ile ambayo ilikuwa inazungumziwa ya kuunganisha Wilaya ya Sikonge na Mkoa wa Mbeya, barabara hii ni muhimu!

**SPIKA:** Sana sana. *(Makofi)*

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Nazungumzia zote hizo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mimi nawapenda Wabunge wa namna hii, si kuvutia kwao tu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Spika, nazungumzia zote hizo na nipo tayari kuungana na mtu yeyote atakayenihitaji katika kupiga debe na kutafuta wafadhili wa barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, ukishazungumza hivyo, ni sawasawa na Mbunge mmoja aliyesema, unaweza ukavaa suruali bila viatu kwa maana kama hatuna barabara za vijijini hata hizi za lami ni bure. Kwa sababu ni lazima magari yaweze kuingia sasa mpaka kwenye Kata, mpaka kwenye Kitongoji kuchukua mahindi, viazi na mbogamboga na bidhaa nyingine na vilevile kupeleka vitu kama bidhaa za ujenzi, mabati, saruji; lazima ziweze kuingia huko ndani. Kwa sasa hivi hatuna mpango wa Kitaifa wa barabara za vijijini, hatuna na hii nafikiri ndiyo ingekuwa kazi moja nzuri ya TAMISEMI, tungeweza tukasema kila Kitongoji kiwe na barabara ya Kitongoji, inachimbwa na kusimamiwa na Kitongoji. Kila Kijiji kila Kata na kila Tarafa. Hatuna utaratibu wa namna hiyo kama tunavyosema shule za Kata! Kwa hiyo, napendekeza kwamba Waziri Mkuu aangalie uwezekano kwa kupitia TAMISEMI wa kuwa na mpango wa Kitaifa wa barabara za toka Kitongoji mpaka Wilaya mpaka Taifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, anayetaka kuelewa ninachozungumza, namwalika Wilayani Rombo. Mimi naishi kijijini, ndani kabisa, nina barabara nne za kuingia kwenye mji wangu kaskazini, kusini, magharibi na mashariki ya kitongoji ikiunganishwa na ya kijiji na ya Kata. Nataka kusema mtu yeyote ambaye anataka kuliewa suala hili, aje Rombo tumwonyeshe jinsi unavyoweza kuzunguka Wilaya ile kilomita nyingi wakati wowote hata wakati wa mvua kwa sababu tuna utaratibu, ulianza miaka ya 1950, si leo, kwa sasa, kila kitongoji kina barabara.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye *SACCOS*. Mimi ni mzoefu sana wa kuunda *SACCOS. SACCOS* ni ushirika na kuna kitu kingine kinachoitwa Vikundi. Kwa hiyo, bado hatujaweka utaratibu mzuri wa vikundi, tumeweka utaratibu wa *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wangu, hasa wa kule Mbeya na Rombo ni kwamba kuna watu ambao hawataki ushirika kwa maana ya *SACCOS* kwa sababu mbalimbali, hatuna muda wa kueleza hapa lakini wapo kwenye vikundi. Tafsiri ya Kisheria ya Kikundi ni nini? Hatuna!

Mheshimiwa Spika, nimeona Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake amesema kwamba anafanya utaratibu wa kuangalia namna ya kuimarisha vikundi hivi vya vijijini, napendekeza kwamba tusizingatie tu hizi *SACCOS* bali tuzingatie vikundi na tuweke utaratibu wa kisheria wa kusimamia vikundi hivi. Sasa hivi hakuna utaratibu wa Kisheria; *SACCOS*, ni za Afisa Ushirika lakini matatizo ya Maafisa Ushirika ndiyo yale yale tunayozungumza hapa na mimi nimesikia yakizungumzwa, si kila Wilaya ina Maafisa Ushirika lakini Halmashauri lazima iwe ni msimamizi mkuu kwa njia yoyote ile wa vikundi vilivyo ndani ya Halmashauri ile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika hilo mimi nasema tena kwa mara ya pili , mtu yeyote anayetaka ushauri kwangu namna ya kuunda vikundi hivi, nipo tayari. Nilianza Mbeya, nimefanya Rombo na kule kuna mifano ya kuigwa ya vikundi ambavyo si vya ushirika ambavyo vinashamiri na vinaendelea vizuri sana. Tunahitaji *Regulatory Framework* (Utaratibu wa Kisheria na Kiutawala) wa vikundi kama hivi kama tunataka baadaye viweze kushamiri sana.

Mheshimiwa Spika, nilianzisha vitu vinavyoitwa Benki Kata, si Ushirika na sasa nasikia kuna kitu kingine kinaitwa VIKOBA, ni aina fulani ya Ushirika vijijini. Tukizungumza habari ya maendeleo ya kifedha vijijini bila vikundi hivi, bila Benki Kata hizi, bila *SACCOS*, tutakuwa tunaishi kwa matumaini tu bila matokeo. Kwa hiyo, naomba jambo hili lishughulikiwe. Mimi ni mzoefu na nipo tayari kushauri ili kusudi tuweze kuwa na kitu ambacho kinaeleweka.

Mheshimiwa Spika, katika fedha hizi za JK, kama tunavyoziita, nimesikitika sana kwamba *SIDO* hawakutambuliwa kama mojawapo wa chombo muhimu kinachoweza kukopesha wazalishaji. Shirika hili la kuhudumia viwanda vidogo vidogo, lipo mpaka vijijini, lipo mpaka Wilayani na Mkoani na lina rekodi nzuri ya kukopeshwa na kurejesha. Hawa wangejumuishwa kama zile Benki za Maendeleo za Wilaya, hawa pia wangehesabiwa na kupewa fedha zile za JK, ili waweze kukopesha wajasiriamali wenye viwanda na shughuli ndogondogo za uzalishaji huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, miaka yote hii toka uhuru, sisi Rombo, hatujui Redio Tanzania wala *TBC* kwa sababu hatuisikii. Sisi tunategemea sana Redio ya Kenya na siku nyingine tunategemea hata Redio ya Sauti ya Zanzibar lakini *TBC*, hakuna.

Mheshimiwa Spika, wakati mmoja walituambia kwamba baada ya kuweka mitambo kule Arusha sasa na Rombo tutasikia. Mimi nataka kutoa ushahidi, kwa sasa hivi tunaipata *TBC* kupitia Redio Sauti ya Injili inayotegeshea *TBC* wakati wa habari na baada ya hapo wanazima na *TBC* kwetu inazimwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu utukumbuke katika mpango wake huu alioueleza wa kupeleka usikivu zaidi vijijini kwamba Wilaya nzima ya Rombo yenye watu 300,000, hatuna uhusiano kabisa wa kihabari na kadhalika na Redio Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba nimefarijika sana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na naomba Wabunge wenzangu tuiunge mkono lakini tusisitize pale ambapo tunafikiri kuna mapengo ambayo tunaweza tukayajaza. Ahsante sana,

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi hii na mimi nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini nianze kwa kuiunga mkono. Nimpongeze sana kwa sababu maelezo yaliyomo ndani yanajitosheleza.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuomba wataalamu wetu, Katibu Mkuu, Bwana Vicent Mrisho, mama Tarishi na Wakurugenzi wengine, nina uhakika hao ndiyo nguzo kuu ya utendaji kazi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu inasimamia pia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Serikali za Mitaa ziko kule

mpaka vijijini, maamuzi yenu yawe sahihi lakini pia tuwahishe yale maamuzi kwa sababu tatizo letu ni kufanya maamuzi. Kuanzia sasa ni vizuri zaidi tufanye maamuzi ya haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba nipongeze vyombo vya habari, kwa kazi nzuri vilivyofanya kwa Mkutano wa Leon Sullivan, kule Arusha. TV/Redio zilihamasisha, sisi Watanzania tuliona kila kitu kilichokuwa kinaendelea kule. Kwa hiyo, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la maji. Mwaka 2006, tulijiwekea utaratibu ambao ulikuwa unaitwa Programu ya Kitaifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Mradi huu au mpango huu ulikuwa unavihusisha vijiji kumi kwa kila Wilaya, nina uhakika hata Urambo imo. Sasa mpango huu mpaka sasa hivi umesimama, je, hatma yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, najua Mheshimiwa Mwandosya, ni Waziri makini, nina uhakika kwa sababu wataalamu wameshafanya upembuzi katika Wilaya 96 ambazo ndizo zimepitishwa na nina uhakika Wilaya ya Kwimba pamoja na Urambo, zimo. Sasa ni vizuri zaidi Mheshimiwa Waziri mhusika wa Maji na Umwagiliaji, akatoa tamko kwamba mradi huu utaanza lini kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi humu ndani kila wakisimama wanaulizia mpango huu.

Mheshimiwa Spika, najua Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, ni Serikali sikivu, ni vizuri sasa ikatoa taarifa kwamba mpango huu wa vijiji kumi kwa kila Wilaya, utatekelezwa mwezi fulani au mwaka fulani ili Serikali yetu ionekane ni makini zaidi lakini lisiwe ni suala la kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, tumepunguza asilimia tatu kwenye bajeti ya maji, sina uhakika kwa sababu mpaka mwaka 2010, tunaambiwa kwamba maji vijijini yanatakiwa yafike asilimia 65 na asilimia 90 kwa mijini, sasa kama punguzo ndiyo hilo, sijui kama tutafika.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala zima la barabara. Mkoa wetu wa Mwanza tuna ule mradi wa *PM*, Mara. Mradi huu ni mzuri sana na utasaidia sana kuboresha barabara zetu. Lakini ninaomba kutoa ombi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, aturuhusu kwa sababu zipo barabara nyingine ambazo haziko kwenye mpango huu lakini upo utaratibu ambao ni lazima Mzabuni apewe. Tunachoomba sisi kwa sababu Mkandarasi huyu yupo jirani na utaratibu wa zabuni una mlolongo mrefu, tungeshukuru zaidi kama ingewezekana Wakandarasi ambao wapo sasa badala ya kutafuta Mkandarasi mwingine ambaye yupo nje basi uturuhusu tumtumie huyu Mkandarasi atutengenezee barabara yetu kwa pesa ambazo ni kidogo kuliko kutangaza miezi mitatu au minne inachukua muda mrefu kidogo. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili ulione.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la msongamano wa magari, mimi nianze na mizani. Utashangaa ukitoka Dar es Salaa ukifika Kibaha unakuta kuna mizani, ukitoka Kibaha unafika Chalinze, unakuta kuna mizani, ukitoka Chalinze kama unakwenda

Morogoro basi Mikese kuna mizani, ukitoka Mikese kama unakuja Dodoma unakuta kuna mizani. Sasa huu ni ucheleweshaji wa maendeleo wa nchi yetu, kama kila sehemu kuna mizani, kwa nini tusiangalie sehemu moja au mbili tukaweka mizani?

Mheshimiwa Spika, lakini si hilo tu, mizani hii iko barabarani, kwa nini hii mizani isichepuke. Sisi utaratibu wetu ni kwamba mpaka mabasi nayo ni lazima yapimwe, mimi sijaona duniani kote, ni Tanzania tu lakini mabasi yanapimwa kwa sababu gani? Hata Mheshimiwa Rais alipotembelea Wizara ya Miundombinu, Machi, 2006, suala hili aliliuliza kwamba hivi ni lazima mizani ikae barabarani? Lakini hii mizani yote, inasaidia nini? Kwa nini msiangalie suala hili vizuri zaidi ili kupunguza matatizo yaliyopo?

Mheshimiwa Spika, lingine, najua pesa zitatoka lakini niombe barabara yangu ya kutoka Sumve – Fulu itengenezwe lakini pia daraja la Mto Simiu, litengenezwe. Nina uhakika pesa zipo na Mheshimiwa Waziri mhusika atalisemea hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende sekta ya umeme, naishukuru Serikali kwa kukamilisha umeme katika eneo la Mji wa Sumve. Hivi sasa nafikiri umeme unaendelea kujengwa katika eneo la Marya. Bahati nzuri Mkuu wa Mkoa alitembelea lakini pia aliyekuwa Mkuu wa Mkoa, Mwalimu wangu, Mheshimiwa Njolay, namkaribisha aje aone maendeleo yale aliyoyaacha, kwa kweli tunasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati wa semina ya Sheria ya Umeme, ulisema mambo mawili. Ulisema kwamba umeme ni gurudumu la kusukuma maendeleo ya nchi. Pili, umeme ni nyenzo muhimu ya maendeleo. Naomba sana umeme Marya uharakishwe kwa sababu moja, kipo kituo cha reli pale kinasubiri umeme, lipo Gereza linasubiri umeme, kuna Chuo cha Maendeleo ya Jamii wanasubiri umeme, kuna Kiwanda cha Kuchambulia Pamba, wanasubiri umeme, kuna Kiwanda cha Mikokoteni, wanasubiri umeme, kuna Chuo cha Michezo Afrika Mashariki na Kati, wanasubiri umeme pamoja na wananchi wa eneo la Marya wanasubiri umeme. Naomba umeme Marya uharakishwe kama ambavyo Wizara iliahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala bora. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Madiwani posho pamoja na usafiri wao, watapata. Lakini tulikuja kwako tukakueleza kwamba Kata ya Mabomba, ina vijiji vitatu Kiserikali lakini ina vijiji vitano Kichama. Tunaomba vijiji hivyo vigawanywe ili kuwapunguzia adha watu wetu kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Vijiji hivyo tunavyoomba vigawanywe ni vya Mwabomba, Chava, Mgogo, Mulula na Mwangika. Nitashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu suala hili liko Ofisini kwako na bahati nzuri wakati tulipokuja kukutembelea nyumbani kwako kipindi kile, Mwenyekiti wangu wa *Council*, hili alilizungumzia. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili nalo alitazame.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kwa sababu hali ya hewa siyo nzuri, njaa ipo hasa Wilaya ya Kwimba na niwaombe kupitia Bunge lako Tukufu wananchi wangu wa Jimbo la Sumve na Wilaya ya Kwimba kwa ujumla kwamba watunze na watumie chakula chao vizuri kwa sababu hali ya hewa siyo nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya afya, ninaomba gari la wagonjwa katika kituo chetu cha Marya.

Mheshimiwa Spika, sekta ya elimu, upo upungufu wa Walimu hasa katika shule za sekondari. Sekondari ya Wasichana ya Sumve na hili nimeshamwomba Mheshimiwa Waziri siku nyingi, najua matatizo ya Walimu yaliyopo ni wachache lakini naomba na kushauri kwamba basi Walimu hao wapatikane.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nizungumzie kidogo yale yaliyozungumzwa ndani humu jana, suala la Kiwanda cha Karatasi, Mgolole. Nitoe taarifa fupi tu kwamba baada ya kubinafsishwa, baada ya kukaa miaka kama 10 hivi, sasa kimeajiri wafanyakazi 600, kina vibarua 1000. Mwaka 2007, waliuza tani za karasi 27,000 na kuingiza dola za Kimarekani 15,000 milioni. Mwaka 2008, wanatarajia kuuza tani 33,000 na wataingiza nchini dola za Kimarekani 22,000, asilimia 20 ya karatasi zinazotengenezwa Mgolole, zinafanya kazi hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaposema kwamba kiwanda hiki hakina thamani, kwa kweli nafikiri ni vizuri tukaenda, tukajiridhisha zaidi. Mimi nashauri wenzangu kabla ya kusema, wafanye utafiti.

Mheshimiwa Spika, lingine, tumelaumiwa sana lakini mimi nasema ikitokea Padri akazini, hivi unalihukumu Kanisa kwamba limezini? La hasha! Haiwezekani! Lakini ikitokea Muislam akasema uongo au Sheikh kasema uongo utasema Msikiti umesema uongo? Hapana! Kwa hiyo, sisi kama wana CCM, tunao utaratibu wetu, mambo ya Richmond na *EPA,* Mheshimiwa wetu ameyachukulia uzito wa hali ya juu, ni vizuri zaidi wenzetu mkafanya subira.

Mheshimiwa Spika, inashangaza hata ile Kamati ya Madini, iliyoundwa na Mheshimiwa Rais, taarifa yake haijatolewa rasmi lakini inasikika humu, haileti starehe lakini pia haipendezi.

Mheshimiwa Spika, nakushuru sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndassa na ninamwita sasa Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo na atafutiwa na Mheshimiwa Savelina Mwijage na wakati huo huo Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, ajiandae.

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kwanza, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuwa mchangiaji katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Vilevile namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuandaa hotuba ambayo ni nzuri, ya kufurahisha na itawasaidia Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, vilevile nachukua nafasi hii kwa sababu kila mtu ana uhuru wa kusema maneno yake hapa, kumshukuru sana Waziri wetu Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kazi nzuri aliyoifanya alipokuwa hapa Bungeni na amelitumikia Taifa hili vya kutosha. Hii ni haki yangu ya msingi, nina wajibu wa kumshukuru pale alipofanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nachukua nafasi hii kumpongeza Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri kwa kushauriana na Waziri wetu Mkuu na kuifanya hotuba hii ikawa nzuri na nawashukuru watendaji wote katika Ofisi hiyo ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, sina budi kuwashukuru wananchi wangu wapendwa kabisa wa Buchosa, walioniweka madarakani tangu mwaka 2000 hadi leo pamoja na mambo yote na nitaendelea kuwatumikia zaidi ya miaka mingine inayokuja, kama Mungu akiniweka hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kumshukuru kwa namna ya pekee, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza, kwa ziara yake nzuri aliyoifanya kwenye Jimbo langu la Buchosa. Alipofika pale alikuta barabara yetu ikiwa mbaya na haipitiki ya kutoka Sengerema - Nyakalilo - Kaunda. Lakini alitoa maneno mazuri na baadaye ilianza kutengenezwa mara moja. Ninawahakikishia wananchi wangu wa Buchosa, kwamba barabara yetu Mkandarasi atakaa barabarani hapo akiitengeneza kwa miaka mitano mfululizo bila kutoka na Mkandarasi aliyeteuliwa ni *Nyanza Road*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mambo ya barabara kwa Buchosa, tiba ipo na ndiyo maana hata nafikiri Wizara ya Miundombinu hawawezi tena kuionyesha hapa kwa sababu tunazo pesa zilizotengwa kwa ajili ya barabara yangu ya Buchosa. Nawashukuru sana watu wa Wizara ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge tangu mwaka 2000 lakini kila Bunge ninajifunza na linakuwa na matukio yake. Bunge la mwaka 2000, tulikuwa tunasikia tu huko nje, leo kuna mabomu na wananchi wanakuwa na masikio ya kusikiliza. Bunge hili nimekuwa kimya kwa muda, nimesikiliza vya kutosha, mambo yamekuwa yakijirudiarudia. Leo mtu akizungumza hapa kesho kutwa atataka azungumze lilelile, tunawafundisha nini Watanzania? Kila siku Watanzania wataacha kufanya shughuli zao kusikiliza habari za *EPA*, kesho Richmond, kesho kutwa Kagoda, siku inayofuata *Meremeta*, *TANGOLD*, Mwananchi, *Deep Green* mara Kiwira na *ANBEN*! Leo unamwingilia Rais Mstaafu kwa kazi yake nzuri aliyoifanya ya kuiletea nchi hii maendeleo! Leo Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, anatukanwa ovyo ovyo, tena anatukanwa wakati mwingine na watu ambao ni wana-CCM! Mimi nasema kwa kupitia Bunge hili, ambaye ameona kwamba Rais wetu Mstaafu hakufanya kazi nzuri, karibu asilimia 90 ya Watanzania watamlaani na wanazidi kulaani kauli mbaya za namna hii.

Mheshimiwa Spika, naomba Watanzania wote hasa Wabunge, tujielekeze kwenye mambo ya msingi ya kufanya kwamba wewe umetoka kwenye Jimbo lako na unalitetea

Jimbo lako ili upate maendeleo na vilevile unatetea mambo ya Serikali yako. Mimi nasema nikiwa kama Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, sitaidharau Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi na sitaikejeli yaani Bunge linataka kugeuzwa liwe kama Bunge la majungu, kila siku ni haya!

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lowassa hapa aliamua tu akaacha nafasi yake ya Uwazi, kwani anakosa, liko wapi? Leo umekuwa mjadala wa kila siku, ameacha kisiasa na hata mimi ningekuwa Waziri Mkuu pale, nikiona kuna tatizo, nitaacha mwenyewe lakini nimeacha kwa ajili ya manufaa tu ya nchi yangu.

Mheshimiwa Spika, hizi Benki nyingine zinazotoatoa siri za pesa za mtu na zenyewe nafikiri zichunguzwe pamoja na kwamba zinatoa taarifa zinaweka kwenye magazeti akaunti za watu! Chenge alikwenda kubomoa nyumba ya nani akawa na hizo pesa? Tungeambiwa hapa, Chenge alibomoa nyumba, akavunja kufuli, akaiba mahali, ndiyo ningeambiwa kwamba kuna kosa hapa. Kama ni mambo mengine, ni lazima Serikali ifanye kazi kwa manufaa ya Watanzania. Kama mtu anakosa twende naye taratibu, lichunguzwe huko maana tunaposimama hapa Bungeni, tunalolisema, wananchi wanaamini.

Mheshimiwa Spika, leo Bunge litabaki, mara Chenge amekuwa mchawi, kesho Chitalilo atakuwa mchawi, kesho kutwa Spika utakuwa mchawi na kesho kutwa nani atakuwa mchawi?

**SPIKA:** Mheshimiwa, hebu rudi kwenye hoja, unaongea hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO:** Ahsante na niko kwenye hoja…

**SPIKA:** Wewe una uhuru kama wenzio walivyo na uhuru kusema wanayosema.

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO:** Haya, nashukuru. Nashukuru kwa kunirudisha hapo lakini nilikuwa sijaenda mbali sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nirejee, nilikuwa najaribu kuzungumza ya wenzangu waliokwishazungumza. Ninaomba nijirejeshe kwa kusema kwamba ajali Tanzania imekuwa ni tatizo sugu, ni kutokana na barabara kuwa moja tu. Tunatengeneza barabara kama ni ya kutoka Dar es salaam, barabara hiyo hiyo ifike Mwanza. Gari inayotoka Mwanza na inayotoka Dar es salaam, waje wakutane pale, madereva wapishane, hii nayo inasababisha ajali kuwa nyingi Tanzania. Naomba Wizara ya Miundombinu ijaribu kuwaza kwamba kama barabara ipo tayari ya kwenda Mwanza, itengeneze barabara nyingine, gari inayotoka Mwanza iwe na barabara yake na gari inayotoka Dar es salaam, iwe na barabara yake. Kwa hiyo, ninaomba suala hili litiliwe maanani.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine, *TRA* nao wamekuwa ni tatizo kwa watu wanaofanya biashara kutoka nje. Ukileta pale biashara yako au ukileta kontena lako bandarini, wao wanakisia wanavyotaka. Ukiwaambia kitu hiki nimenunua labda dola 10,000, wao wanafanya mara tatu mpaka mara tano. Nchi yetu inatakiwa ikusanye kodi ambayo ni halali lakini kukusanya kodi ambayo siyo halali, hata kwa Mungu, ni makosa.

Mheshimiwa Spika, nilifikia hatua siku moja nikawaambia watu wa *TRA*, kama wanabisha kitu hiki hakikununuliwa kwa dola 20,000, nimlipie mtu wa *TRA*, twende mpaka hapo kiliponunuliwa, *either* China au Japan, akaone mwenyewe na mwenyewe ununue kwa dola hiyo. Wanasema hiyo ni mara tatu au ni mara mbili!

Mheshimiwa Spika, wanapoangalia kwenye mitandao, wanaangalia labda kitu fulani, labda gari fulani ni la dola kadhaa, hawajui kama kunaku-*negotiate*, mkapunguziana bei, hiyo *TRA* hawana! Huo ni uonevu kwa wafanyabiashara. Mimi ninaomba jambo hili, watu wa *TRA* waangalie sana kwamba kuna makosa ambayo wanayafanya la kutowasikiliza wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye jambo la uchumi, Tanzania tusipoangalia, hatutakwenda mbele sana kwa sababu moja, uchumi wetu mimi labda ningeufananisha na China kwamba wao mambo ya uchumi na siasa hawachanganyi pamoja. Tungeangalia eneo moja kama ni Dodoma, ndiyo tuje tuzungumze mambo ya siasa hapa, tukifika huko kwenye sehemu za kazi, tuzungumzie mambo ya uchumi, itakuwa vizuri zaidi. Huo ni ushauri wangu tu. Ninyi ambao mmebobea kwenye mambo ya uchumi, mtaliona kwa upana zaidi.

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala moja nalo ni suala la umeme. Suala la umeme, ni suala ambalo kila Mtanzania, awe anatoka kijijini kama kule Buchosa, naye anataka mwanga. Sehemu nyingi sana, inapofika hata saa moja, watu wanaingia kulala badala ya kujisomea au kufanya shughuli nyingine, ni kwa sababu kuna giza.

Mheshimiwa Spika, nimeshangaa kwenye hii hotuba, Mheshimiwa Waziri labda utanifafanulia wakati wa kuhitimisha, kuna mahali hapa, ukurasa wa 34, nimeangalia katika ule mpango wa Rais Bush, hakuna sehemu ambayo inatamka kwamba Mwanza iko katika ule mpango wa kupata umeme. Kwa hiyo, nitapenda nipate *clarification* ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, umeme kule kwangu Buchosa, ni muhimu na unatakiwa kuanzia pale Kata ya Nyanzenda, Nyakasungwa, Yakalilo, Bukokwa, Kalebezo, Nyehunge, Kafunzo, Bupandwa hadi Kaunda. *Centre* hizi ni *centre* kubwa na Jimbo langu ndio Jimbo ambalo hata chakula kwa Mkoa wa Mwanza unategemea kule, nina Ziwa kule, nina msitu mkubwa, Buhindi *Forest*. Kwa hiyo, ni Jimbo ambalo linajitegemea kwa mambo mengi, kupatiwa umeme ni lazima. Lakini nashukuru kwamba tayari Mheshimiwa Waziri Ngeleja amenihakikishia kwamba iko ila walisahau kuiweka tu hapa lakini, nitapenda itoke wazi hapa.

Mheshimiwa Spika, nakuja upande wa barabara. Upande wa barabara, nimeshasema tangu mwanzo kwamba sitapenda kuongelea mambo ya barabara, lakini ni vema tuimarishe vile vile barabara za vijijini ndani kabisa, sio tu barabara za Wilaya, barabara za Mkoa, sijui na nini, tuzidi kuimarisha barabara za vitongoji kwa vitongoji au kijiji kwa kijiji.

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika hotuba ya Waziri Mkuu, kilichonifurahisha zaidi ni kile Kivuko cha Nyakalilo – Kome, kile kipya. Hicho sitaki kuzungumza kwa sababu hata wananchi walisikia wakati unasoma hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini, vile vile ninaomba tu kuipongeza Wizara kwamba imekuwa ikinisikiliza mara kwa mara ninapokuja ofisini kwao na ninapoonana hata na Waziri mara kwa mara, ndiyo maana imewekwa hapa, kwa hiyo nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, lakini, ninaomba sasa Wizara wakati huu tunasubiri hicho kivuko kipya, hiki kingine ambacho kinafanyiwa matengenezo pale Mwanza, kitengenezwe haraka. Niliambiwa mwezi wa nane kitaanza kazi, naomba Waziri ulifuatilie hili suala ili kuhakikisha watu wako kule Mwanza wanapata usafiri.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu sasa ni kubwa na Wilaya ya Sengerema ina watu takribani 500,000, Jimbo langu lina watu karibu laki mbili na kitu, hakuna sababu ya kuinyima kuwa Wilaya. Kuna *centre* kubwa kama Nyaunge pale, inajitosheleza kabisa kuwa Wilaya na bahati nzuri hata juzi juzi Halmashauri yangu imepanga kujenga Hospitali ambayo ni kubwa kabisa ambayo itasadia wananchi wangu wengi pale. Kwa hiyo, ninaomba hili wazo pamoja na kwamba litaanzia kule, lakini huku ni vema nikaliweka wazi Waziri Mkuu akawa nalo kwenye kumbukumbu zake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni ulinzi, ninaomba ulinzi, kila mara nimekuwa nikipiga kelele hapa, Jimboni kwangu kule kwenye Ziwa, Wavuvi ni wengi na wana mali zao nyingi lakini, ulinzi umekuwa ni hafifu, wanavamiwa na kuuwawa na kunyang'anywa mali zao. Ninaomba ulinzi sasa wa kudumu kabisa katika Visiwa vya Zilakula, Maisome, Chembaya, Mchangani, Swaswa, Iyezu, Gembele na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, ulinzi ni jambo ambalo ni la maana sana. Kumekuwa na uvamizi wa kila mara, sina haja ya kusema hapa kila siku lakini kila mara kwa nini nilalamike kwamba kwangu kule kuna matatizo? Ninaomba sasa Serikali inisikilize.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano, kwa sasa kwa kiasi kikubwa, mawasiliano Buchosa, si mabaya sana lakini, bado kuna tatizo. Ninayashukuru makampuni ya *Celtel, Vodacom, Tigo* yamekuwa yakitusikiliza kwa shida zetu na yameweza kujitahidi *at least* kuweka minara. Lakini, ninaomba sasa minara mingine iweze kupelekwa kwenye Visiwa kama Zilakula pamoja na Kisiwa cha Kome. Nilishazungumza na watu wa *Celtel*, sasa ni wakati wao wa kutimiza tu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba michango yangu yote, niliyoizungumza hapa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, aweze kunisaidia ili watu wangu wa Buchosa waendelee kuwa na imani na mimi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sitaki kupoteza muda wako mrefu, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa hapa na nikaweza kuchangia bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa bajeti yake kwa kuwafikiria Madiwani wetu, siku nyingi, ni kilio kikubwa hapa, Wabunge wote tunalilia Madiwani lakini tunaomba kama alivyoandaa iweze kutekelezeka, siyo iwe ahadi, ahadi mpaka tukafika 2010 bado hawajapata huo mpango.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mikakati mizuri tu, ina mipango mizuri lakini kutekelezeka inakuwa ni shida. Kuna pesa zinatengwa kwenda kwenye Wizara, kwa mfano, Wizara ya Maji, tumetembelea Bwawa la Manchila lenye miaka 31, ukihesabu pesa za Serikali zilizotumika pale ni pesa nyingi sana tu, mimi nilisikitika kweli, nikasema afadhali wangezileta Bukoba zikatengeneza Uwanja wa Ndege, kuliko kutoa pesa mara kwa mara, mradi wenyewe hauonekani, wanachokifanya hakionekani. Naomba pesa zikiwa zinatolewa kwenye Wizara yoyote, kuwe na ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuona kama zinafanya kile kilicholengwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na tatizo la Mkoa wetu wa Kagera. Nitausemea huu Mkoa na mara kwa mara nikisimama hapa inakuwa wimbo, sisi tumeshakuwa kwenye Kisiwa, hatujulikani kama tuko Tanzania ya wapi. Kwa sasa hivi hatuna hata usafiri wa ndege, meli yenyewe ni ya kusuasua. Tumeahidiwa meli sasa huu ni mwaka wa kumi, sijui tunafikiriwa mpaka lini! Wanasema uchumi umekua, naona uchumi umekua sehemu nyingine, siyo Kagera.

Mheshimiwa Spika, vijana wanaanzisha miradi yao, huko huko Kagera, wanakamatwa, wanapigwa, wananyang’anywa mali zao, sijui ni Tanzania ya wapi, hawa vijana watapata maendeleo kutoka wapi? Ajira yenyewe iliyoahidiwa na Serikali haionekani, wenyewe wanajianzishia ajira, ndiyo hivyo, ajira yenyewe inaharibiwa. Kwa mfano, kama vijana wa pikipiki na baiskeli, zimekamatwa baiskeli zina miaka kama saba ziko kwenye Kituo cha Polisi, ni mali ya Mtanzania hiyo, kweli Serikali haioni aibu kumtesa Mtanzania kiasi hicho?

Mheshimiwa Spika, ninakwenda kwenye barabara, kuna barabara ya kutoka Kagoma - Lusaunga, Mkandarasi alinyang'anywa, sijui Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninakwenda kwenye barabara ya kutoka Kyaka – Mlongo na kutoka Mlushaka - Kabanga, haionekani katika bajeti zote zinazosomwa hapa, mimi sijui kama hii bajeti itatusaidia sisi watu wa Kagera. Naomba Waziri akiwa anajumuisha, atueleze kama tuko kwenye mpango wake au hatupo.

Mheshimiwa Spika, narudi kwa Maaskari. Niliomba hapa Serikali iwasaidie Maaskari Polisi, sehemu ya kutoka Lushaka kwenda mpaka Kimisi, angalau wajenge kambi ndogo kuliko watu kuteseka mara kwa mara wanatekwa pale, wanakamatwa, wanauwa na Askari wa *escort* ni mmoja tu, hawezi akasaidia kitu. Niliomba lakini sijasikia mpango wowote wa kuwasaidia wale watu angalau kuwapa usafiri wa kuwasaidia kufanya *patrol* za mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwenye mambo ya mazungumzo ya Zanzibar. Kwa kweli mazungumzo haya, namwomba Rais, wale ambao ni washauri wake, asiwasikilize, wanamdanganya. Yeye mwenyewe, aingie akiwa yeye, kuliko kuwasikiliza washauri, wanampotezea muda wake na kuendelea kutokuwa na imani na watu wa Zanzibar na uongozi uliopo madarakani.

Mheshimiwa Spika, narudi kwenye kujenga Zahanati. Sisi Mkoa wa Kagera, sana sana mambo ya michango, wananchi wamechangia sekondari kwa kusuasua. Watu wa Kagera mazao yao ilikuwa ni kahawa. Mtu akiuza kahawa yake, anapata pesa ya kuweza kuchangia maendeleo ya Mkoa wake lakini, ndiyo hivyo, katika kuongoza kote, sisikii watu wanasema kuhusu kahawa, sisikii wanasema kuhusu kilimo. Kilimo chenyewe hata wakijitahidi kulima kama Mkoa wetu, walime nini? Barabara hakuna kusema angalau watalima kitu chao ili kiweze kusafirishwa vizuri. Watu wanatoka Uganda, wananunua mali kwetu, faida inakwenda kwao badala ya sisi wenyewe, tungekuwa na uwanja mzuri wa ndege haya yangewezekana. Ndege zinakuja, kama Uganda, ndege zinafika zinachukua ndizi, zinachukua michicha, zinachukua matunda, lakini sisi Kagera utalima nini, watu wameshakata tamaa ya maisha, ni kwa sababu huo Mkoa umesahaulika.

Mheshimiwa Spika, narudi kwenye Halmashauri na Manispaa. Sisi Wabunge wa Viti Maalum wote hatuthaminiki hata kidogo, aliongea Mheshimiwa Chilolo jana, ni hivyo hivyo na Kagera.

Mheshimiwa Spika, juzi hapa Rais alikuwa anakuja Kagera, sisi hatukupata muda, Mheshimiwa Mushashu alipata muda wa kuweza kuzunguka na Mheshimiwa Rais akiwa hathaminiki kabisa, alikosa hata sehemu ya kulala, hata gari lake walilizuia asiende kwenye msafara. Mimi nitaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa anajibu, aweze kutuambia ni Sheria gani inayozuia Wabunge wa Viti Maalum kuingia kwenye Kamati

ya Fedha na Uchumi? Kama kuna kipengele hicho, nilimwambia Mkurugenzi, niandikie barua basi nijue ni kipengele gani kinatuzuia sisi, ni kwa sababu wanajua Mbunge tuliye naye hasa kama pale Bukoba Mjini ni Mheshimiwa Kagasheki, anakuwa wakati mwingine yeye hayupo pale, wanafanya maamuzi yao, wanafanya wanavyotaka, kama ni pesa wanagawana wenyewe.

Mheshimiwa Spika, utasikia kwamba, Meya na Makamu Meya wanasafiri ili wamalize zile pesa, zile pesa hazijulikani zinafanya nini. Wanasafiri kwenda wapi na wananchi wapo wanalia na njaa, vijana hawana hata kitu chochote cha kuwasaidia? Zile pesa badala ya kuzichukua angalau zikafanya kitu cha maana, wenyewe wanasafiri, wanakwenda London, sijui wanasindikiza Kwaya, sijui wanasindiiza nini, ni kwa sababu sisi Wabunge, wawakiklishi hatupo! Nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aweze kunisaidia, tufanyeje ili tuweze kuwa tunaingia kwenye Manispaa?

Mheshimiwa Spika, nitarudi kwenye hospitali. Hospitali tunayo nzuri tu, lakini Madaktari ni shida, mpaka uende Bugando ndio unapata ma-*specialists*. Madaktari tulionao pale ni ma-*Medical Assistants*, ndio wako pale, lakini Madaktari hamna! Tuna vifaa vya *X-Ray*, hatuna mpimaji!

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli auangalie kwa macho ya huruma Mkoa wa Kagera. Sasa hivi wakinipigia simu, wakaniambia unahitajika nyumbani, nitakosa mahali pa kupitia kwa sababu ndege hamna, kila kitu hamna, mpaka nizunguke na gari kupitia hapa, mafuta yenyewe unayasikia bei inazidi kupanda, watu wanasema mafuta yamepunguzwa, sasa hivi Kagera ni shilingi 2000/= lita moja. Sasa nikiondoka hapa kwenda Kagera nitachukua mafuta lita ngapi ya kwenda na kurudi kuja hapa Dodoma? Naomba tuliangalie hili suala la mafuta.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuongelea, ni kuhusu hawa vijana wa pikipiki na baiskeli. Mara kwa mara, kipindi kilichopita, walisema Muswada wa Sheria utapitishwa ili kuwaruhusu hao vijana waweze kujitegemea kwa kuwa na kipato chao. Naomba sana nijue ni nini kinachozuia au kwa kuwa Kagera ndio wanaendesha? Kwa sababu unakwenda sehemu nyingine unakuta wanaendesha baiskeli, wanapakia watu, wanapata kipato chao bila kumwomba mtu yeyote mtaji wala kusema wameunda *SACCOS* wakapata baiskeli na pikipiki, ni uchumi wao wenyewe. Kwa nini Serikali inawatupa kiasi hicho?

Mheshimiwa Spika, narudi kwenye shule. Shule ziko nyingi tu, wamejitahidi wamejenga sekondari, Madiwani wamejitahidi wamechangisha hata kama tunawasahau lakini nashukuru kama nilivyotangulia kusema Mheshimiwa Waziri ameshasema, naomba haraka haraka kabla hatujaondoka hapa tupate maamuzi ni lini wanaweza kusaidiwa. Wamejitahidi kuchangisha shule lakini imefika mahali hawa Watendaji wa Mitaa kwa njaa yao, hawawezeshwi kuweza kupata chochote, fedha wanakusanya, wanakaa wenyewe, wanagawana pembeni lakini siwalaumu kwa sababu Serikali

imewasahau. Wale Watendaji wanafanya kazi kubwa sana. Naiomba Serikali iwaangalie sana watu hawa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nimesema mara ya kwanza, nitarudia tena kwa hawa Maaskari hawa *Field Force*, ukifika pale utasikitika, nitaomba nichangie tena kwa Waziri wa Ulinzi. Maaskari wale ukiangalia wanapolala Mheshimiwa ni pa kusikitisha. Naomba Serikali, vifungu vyote vya fedha vinapita hapa lakini sijaona kama Kagera itakuwemo kwa ajili ya Maaskari wa Kagera na si Kagera peke yake naona ni sehemu nyingi sana. Unakuta wako kwenye mabati, ni masikitiko kwani wanatufanyia kazi kubwa sana. Ikitokea majambazi Kimisi, umeshawapigia simu, wameshakwenda kule, familia ameiachaje, anaishije, hana hata usafiri na kadhalika, naomba sana wawasaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sitaacha kuongelea mwekezaji huyu aliyetufukuza, nitamwongelea sana. Nilisimama hapa nikasema kwamba huyo mwekezaji anachoma sindano wanyama wetu, anawasafirisha kuwapeleka kwao na kwao kule ameshakuwa na mbuga inaitwa Serengeti. Nitaomba Serikali ifuatilie sana, siku ile nilijaribu kuongea hapa wakasema kwamba nisubiri kuchangia kwa Waziri Mkuu au kwenye Wizara husika. Sasa nalia mbele ya Waziri, kweli tukiamua kuwaachia kiasi hicho, tunakwenda wapi? Anapeleka wanyama wetu kiasi hicho, kama anafanya kitendo kama hicho, naomba Mheshimiwa Waziri hili suala lifuatiliwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ile ile alipo kuna sehemu inajulikana ina madini, anazuia hata watu kwenda kule. Mtu amekuja kuwekeza ameshakuwa Mtanzania kabisa, sasa tukifanya hivyo, tutakuwa tunaendelea kupoteza mali nyingi.

Mheshimiwa Spika, wenyewe hawa wawekezaji wakishaingia hapa wanapata wafanyakazi, wanaendelea kufanya kazi lakini kuwalipa kwenyewe ni shida. Soronera pale, wafanyakazi tulikuta wanalia, mimi na Mheshimiwa Kirigini tulirudi nyuma kwenda kuwahoji. Mpaka sasa hivi hawajalipwa, wanapewe nauli ya kuondoka pale kwenda makwao, hawapewi chochote. Kweli angekuwa ni Mzungu tumfanyie hivyo, kama unavyoona, wanakuja hapa, tunawabania hapa, unamwambia kwamba umefika hapa labda umemleta mwenyewe kwamba nitakulipa mshahara, nitakupa nauli, unachukua nauli peke yake unamwambia nenda, ataondoka, si atakupiga risasi?

Mheshimiwa Spika, naomba tusiwe tunaleta wawekezaji hapa wanatuendesha, iwe mwisho. Mikataba yao iletwe hapa, itungwe Sheria ya mfanyakazi na mwekezaji siyo kujichukulia madaraka kama wanavyofanya. Wewe Mzungu mwenyewe anaingia hapa, anakuja kutuzuia tusiingie kwenye hoteli, yeye ni nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudi kwenye barabara ya Mugumu - Serengeti. Ni masikitiko makubwa, tulitembea pale karibu masaa matano kufika kwenye bwawa la Manchila, tumefika pale tumekuta wana utaratibu wa ajabu. Kwenye bwawa lile

kulikuwa na wakazi wanaishi pale, wale wakazi walishalipwa lakini bado ile Wizara wanaundaunda vikundi wanawalipa, Serikali inazidi kutoa fedha, hizo fedha zinazolipwa kila siku wakazi wa pale kwa nini zisimalizie lile bwawa?

Mheshimiwa Spika, tumeangalia nyumba zilizojengwa kwa shilingi milioni 70, ukiziangalia nyumba zenyewe, utasikitika.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri, fedha zikiwa zinatolewa kwenye mradi wowote, kuwe pia na usimamizi kama ni Mbunge wa Jimbo lile, kama ni Madiwani au kama ni Wenyeviti wawe wanafuatilia wenyewe.

Mheshimiwa Spika, suala langu la mwisho, naomba nizungumzie suala la Zanzibar, jamani namwomba Rais, hawa washauri wake si washauri, wanampoteza.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na hatimaye leo nimepata nafasi ya kushiriki tena katika bajeti hii, ni bajeti ya tatu tangu niingie katika Bunge lako Tukufu.

Baada ya shukrani hizo, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya na anayofanya siku zote tangu alipoteuliwa, lakini pia kwa maandalizi mazuri ya bajeti hii ya hotuba ambayo tunaijadili sasa hivi, kwa kweli kazi ni nzuri. Nawashukuru pia wasaidizi wake wote nisingependa kuwataja majina, ninaamini Mungu atawabariki katika utendaji wao wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, napenda kumpongeza Mkuu wetu wa Mkoa, Bregedia Dr. Balele, kwa kazi nzuri ambazo amefanya hasa katika usimamizi wa shughuli za maendeleo katika Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kupitia jedwali hili lililotoka kwa Waziri Mkuu katika orodha ya majedwali, katika watoto waliofaulu kwenda shule za sekondari, wamekwenda kwa asilimia 100, hiyo ni kazi nzuri. Kwa hiyo, ninaamini wakiendelea hivyo, kwa kushirikiana na wadogo zako pamoja na sisi Wabunge, iko siku Mkoa wa Shinyanga utakuwa katika hatua nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niingie kwenye bajeti. Nataka nizungumze suala la MKUKUTA kama vile ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini nitaainisha kipengele kimoja baada ya kingine juu ya suala la uwezeshwaji watu kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, suala hili limeelezwa na hata katika bajeti iliyopita lilizungumziwa, hata hivyo, Mheshimiwa Rais, aliamua kutoa fedha za wajasiriamali maarufu kwa jina la JK. Kweli fedha hizi zimekuwa zikisaidia sana lakini baadhi ya

maeneo kuna matatizo ya upatikanaji wa fedha hizi kutokana na kukosekana kwa taasisi za kifedha katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Bukombe, hatuna benki. Muda mrefu sana nimekuwa nikizungumzia suala la benki na mwaka jana tarehe 23/8/2007, Mheshimiwa Rais alipokuwa Bukombe, watu wa *NMB* walimwahidi wakasema ifikapo Oktoba 2007, tutafungua tawi pale lakini mpaka leo, tawi halipo. Tunasaidiwa sana na *NMB* na *CRDB* iliyopo Kahama umbali wa Kilomita 100 lakini sheria zao zinataka zikopeshe umbali usiozidi kilomita 20. Ninaomba sana Serikali itusaidie kwa sababu uendeshaji wa Halmashauri unakuwa ni mgumu sana, hawawezi wakakaa na *hard cash* lazima fedha ziwekwe benki na lazima kila siku wajaze mafuta kwenda Kahama kilomita 100, kwenda na kurudi kilomita 200. Tunaomba mtusaidie, ikiwezekana mtujulishe ili wananchi wa Bukombe wajue hatma ya benki yao ni nini? Hawa *NMB* waliahidi watafungua au basi ndiyo imeshindikana?

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika hili tunapokosa benki mzunguko wa fedha kiuchumi, unakuwa ni mgumu kwa sababu fedha zinakuwa mikononi mwa watu na ndiyo pengine hata ujambazi katika Wilaya ya Bukombe ni mkubwa. Tunashukuru imefanyika *operation* ya Kamanda Tossi na wakati inafanyika kule bado matukio mengine yanaendelea ndani ya *operation.* Kwa hiyo, tunafikiri ni kwa sababu hatuna benki na Wilaya ya Bukombe ni Wilaya ambayo ni nzuri kiuchumi, tunaomba sana mtusaidie.

Mheshimiwa Spika, niende sekta ya maji, katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, wenzangu wamezungumza na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameeleza kwamba mpaka sasa hivi, tumefikia asilimia 55.7 na asilimia 73 maji vijijini na mjini lakini Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni asilimia 65 kwa 90 kwa Vijijini na Mjini. Wilaya ya Bukombe mpaka sasa ninavyoongea tuna asilimia 35 ya watu wanaopata maji safi na salama. Kwa hali hii, inawezekana tusifikie lengo. Tunaomba sana tuangalie, asilimia 35 ya watu 525,746, ina maana ni watu 184,011, ndiyo wanapata maji safi na salama. Kwa hiyo, tunapata shida, tunaomba mtusaidie.

Mheshimiwa Spika, uko mradi wa Ziwa Victoria, tunaishukuru Serikali kwa sababu umeukamilisha lakini mradi huu, najua awamu ya pili ilikuwa imekubalika kuhudumia watu milioni moja waliomo Bukombe, tunaomba sana muendelee kulifanyia kazi suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la mfumo wa stakabadhi ya mazao. Ni mfumo mzuri sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameeleza kwenye ukurasa wa 27 wa hotuba yake lakini tumeona jinsi watu wanaolima mazao ya korosho walivyofaidika na mfumo huu. Nimejitahidi sana pamoja na Watendaji wangu katika Wilaya yetu ya Bukombe, tukahamasisha wananchi wetu, safari hii zao la pamba wauze kupitia mfumo wa stakabadhi ya mazao. Tukaanzisha utaratibu huu tukaweka *SACCOS*, zimepitia taratibu zake zote, tunajua bei ya pamba haijapanda ukilianganisha na mwaka jana, sasa hivi wananunua shilingi 400 mwaka jana ilikuwa shilingi 500, lakini msimu

umefunguliwa, hivi vyama vilivyotakiwa kununua pamba kupitia mfumo wa stakabadhi ya mazao, vimekosa fedha, wananchi mpaka sasa ninavyozungumza, naamini wananisikiliza, baadhi yao mazao yao yako majumbani wanasubiri waje wauze kwa mfumo huu. Katika hili nitaomba Waziri Mkuu anisaidie sana, haya mabenki yawape fedha wanunue pamba. Wasiponunua pamba katika mfumo huu, tunapata wakati mgumu sana.

Mheshimiwa Spika, hii najua na hata Mkuu wa Mkoa anajua, wakati tunaanza kuhamasisha hili, tumeshirikiana sana lakini leo *SACCOS* zile ambazo zinatakiwa zipate fedha bado zinahangaika sana. Hata asubuhi wamenipigia wakiniuliza, Mheshimiwa Mbunge, tufanyeje? Wao wanajua kimbilio lao ni Mbunge na mimi leo nasema kimbilio langu ni Waziri Mkuu, naomba uwasaidie, pamba iko nyumbani, wanatakiwa wanunue na waiuze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la utawala bora, leo ni mara ya tatu nikisimama katika Bunge hili kuchangia bajeti ya Waziri Mkuu, nikiongelea suala la kutenga maeneo ya utawala. Wilaya ya Bukombe ina kilomita za mraba 10482, Wilaya ya Bukombe ina vitongoji 488, ina vijiji 120, ina Kata 14, ina Tarafa tatu, ina Jimbo moja na *growth rate* yetu, ni asilimia 7.4, ni hatari kweli lakini Kitaifa wakati Waziri wa Fedha na Uchumi, anasema *growth rate* ya nchi sasa ni asilimia 2.9, tena anasema ni hatari sana, ni changamoto, sasa hebu oneni Bukombe tuna asilimia na 7.4, changamoto kali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana hili mtusaidie. Waswahili husema binadamu hufariki, mataifa huanguka, lakini fikra hudumu. Mimi ninaamini maneno niliyoyasema tangu mwaka 2006 katika bajeti mpaka leo yanaendelea kudumu. Wananchi wangu wanasikia. Tunaomba mtusaidie tupate kutenga maeneo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, akiwa pale TAMISEMI, amesaidia sana baadhi ya Wilaya. Alisajili vijiji, akaongeza vijiji na ninaamini hili nalo haliwezi likawa ni shida. Ninaomba tuweke kipaumbele, kila Mbunge analalamikia suala hili lakini hebu tuone ukubwa wa maeneo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kuangalia kwenye kitabu cha makisio ya idadi ya watu katika Majimbo ya Uchaguzi, ukioanisha, ukikuta Wilaya ina watu 400,000 ina Wabunge wawili au ina Wabunge tatu lakini Bukombe ina watu 525,746, ina Mbunge mmoja. Hata hivyo, ninashukuru tu kwa sababu wananchi wangu wananipa ushirikiano mkubwa na ninafanya kazi kweli, kama punda ili tuone jinsi ya kutekeleza Ilani hii.

Mheshimiwa Spika, katika kila kipaumbele, kunakuwa na mambo ambayo umesema, mimi nimeeleza sana katika mambo ambayo ninatakiwa niyatekeleze sasa hivi ni pamoja na hili lakini pia watendaji wetu wa ngazi za Kata wanapata shida sana katika kusimamia kwa sababu maeneo yao ni makubwa mno.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana mtusaidie na mwaka kesho tuna uchaguzi, vipo vitongoji ambavyo nashindwa kujua nini kimetokea na Madiwani wangu wameshindwa kufika kwa sababu aliviahidi, ni kweli vina sifa na mimi nilisema vinasifa lakini nashindwa kufika kwa sababu nitakapofika pale kabla ya kufanya chochote wanakuuliza je, tumepata Kijiji?

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, anapohitimisha suala hili anisaidie ili nikimaliza Bunge, nikatembelee vitongoji vyangu hivyo kwa sababu nitakuwa na *confidence* kutoka kwako.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Kaka yangu, Ndugu Kishenyi na Watendaji wake wote kwa sababu baada ya kuona ukubwa wa maeneo haya, ni kweli amejitahidi kutumia vyanzo vyetu, tukaweza kununua pikipiki za Madiwani wote, pikipiki za Watendaji wa Kata, kwa kweli tunahitaji kusifiwa na nina kila sababu ya kumsifia ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, ninakumbuka siku moja, Naibu Waziri ambaye ni Waziri wa TAMISEMI, alijibu swali langu hapa akasema kwamba mna uwezo wa kufanya hivyo na mimi nikaenda kukaa na Mkurugenzi wangu, tutakubaliana. Kwa hiyo sina budi kumpongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea suala la uundwaji wa Mkoa. Wilaya ya Bukombe kutoka Makao Makuu ya Mkoa ni kilomita 225, tunaomba ikiwezekana Mkoa mpya unaojumuisha Wilaya ya Chato, Geita na Bukombe, uundwe na hili ninaamini Mkuu wangu wa Mkoa ataniunga mkono kwa sababu tupo mbali sana na Makao Makuu ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la mgawanyo wa rasilimali. Katika kitabu cha orodha ya majedwali, ninaomba sana Serikali, muangalie mnapogawa rasilimali. Ukurasa wa nane na tisa, Mkoa wa Shinyanga, una watu zaidi ya milioni 3,411, umepewa bilioni 62 *point* kadhaa na nikajaribu kuangalia Mkoa wa Arusha wenye watu milioni 1.5, una bilioni 40 *point* kadhaa, tuangalie kama kuna uwiano pale. Nikachukua Mkoa mwingine Mkoa wa Tanga, una watu milioni 1.8, umepewa bilioni 56, nikachukua Mkoa wa Pwani, una watu 995,000, ukachukua bilioni 36. Naomba mgawanyo huu tuungalie, wataalamu wetu wa Serikali, tusaidieni ili migawanyo hii iende sawa.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, ni suala la umeme. Leo nimepigiwa simu na watu wangu, wanasema, jana tulisikiliza hotuba ya Waziri Mkuu, hatukusikia Bukombe na mimi niliongea na Mheshimiwa Ngeleja hapohapo, akasema kwamba ipo. Mimi ninasema, tusipopata umeme, mtanipa wakati mgumu sana, ninaomba mrahisishe wakati wangu katika mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niwashukuru sana kwa kunisikiliza lakini niwashukuru wananchi wangu wa Wilaya ya Bukombe ambao wanaendelea kuniamini. Naomba wavumilie, maswali waliyoyauliza, Ijumaa wasikilize majibu yatatolewa na Waziri Mkuu na watasikia jinsi Serikali yao inavyowatekelezea matakwa yao. Naamini Serikali yetu ni sikivu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia lilikuwepo suala la kupeleka *SGR*, tunaomba kama ikiwezekana *SGR* waende kule.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na Mungu atubariki sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Awali ya yote, napenda nimpongeze Naibu Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa, kwa hotuba yake nzuri. Nategemea maswali aliyouliza, yatajibiwa na ushauri alioutoa, wataufuata.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuingilia kati uuzwaji wa *Coco Beach.* Hili ni jambo zuri. Inaonyesha ni jinsi gani watu wanaweza wakawa wabinafsi badala ya kujali maslahi ya Taifa, wakajali maslahi yao wenyewe. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aendelee na mikakati hii kwa sababu kuna mikataba mibovu hadi kwenye ngazi za vijiji.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba sasa niende katika mchango wangu kuhusiana na hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia miundombinu ya Jiji letu la Dar es Salaam. Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake, ukurasa wa 70/71 amesema:-

*"Aidha matatizo mengine yanayolikabili Jiji la Dar es Salaam ni pamoja na miundombinu ya barabara isiyokidhi mahitaji yanayopanuka kila siku, miundombinu isiyotosheleza ya maji safi na taka na ukuaji wa Jiji usioenda sambamba na utoaji huduma kwa wananchi. Hali hii inalifanya Jiji la Dar es Salaam lisionekane kama kioo cha nchi yetu. Hivyo, kuna haja ya kuangalia kwa namna ya pekee"*

Mheshimiwa Spika, katika mitaro ya maji machafu katika Mji wa Dar es Salaam, ninashauri Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anaangalia miundombinu ya Dar es Salaam, waangalie ni jinsi gani wanaweza wakafanya mitaro ile ikafunikwa. Mji wa Dar es Salaam, una watu wengi sana, kuna watu zaidi ya milioni tatu na kuna watu wasioaminika. Mitaro ile wengine wanaifanya ni majalala ya uchafu na Kunguru

wanabeba takataka kule na wanapeleka kwenye makazi ya watu. Vilevile inaweza kuwa ni sehemu ya mazalio ya mbu na magonjwa ya kuambakizwa kama kipindupindu na itakuwa ni vigumu kuyadhibiti. Kwa hiyo, ninashauri wafunike na inawezekana kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika mji wetu wa Moshi, mitaro ile imefunikwa. Kwa wakati huu, ninapenda nimpongeze kabisa, Mkuu wetu wa Mkoa, Mheshimiwa Mohammed Babu, kwa kazi nzuri anayoifanya katika Halmashauri yetu ya Moshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Dar es Salaam, nina uhakika, katika Halmashauri zetu zote, kuna Wahandisi lakini Wahandisi hawa bila shaka hawapewi fungu la kutosha. Ukiangalia, kuna barabara zinatengenezwa lakini baada ya muda mfupi zinaharibika.

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo, ni barabara ya *Old Bagamoyo* ambayo Rais Mstaafu anaitumia, Mama Maria Nyerere, anaitumia kwenda nyumbani kwake lakini barabara ile ina mashimo na yanaweza kufanya tukapata ajali. Unakuta wakati mwingine dereva anakwepa shimo anakutana na daladala uso kwa uso. Ni hatari pia kwa wapita njia kwa sababu Madereva wakijaribu kukwepa mashimo, wanakwenda kwenye *pavement* wanaweza pia wakasababisha ajali kwa wale wanaotembea kwa miguu. Ninapenda barabara hiyo, kwa wakati huu sasa, Halmashauri iangalie ni jinsi gani inaweza ika-*repair* barabara ile.

Mhehimiwa Spika, si hilo tu, mvua ikinyesha, kuna kadaraja kako pale katikati ya *Shoppers Plaza* na *TMJ*, panaitwa Chama. Daraja lile, mvua ikinyesha, huwezi kuliona, ni hatari sana. Hivi wanasubiri mpaka mtu afe pale ndiyo waweke alama za chuma? Sidhani kama hili litatugharimu sana, ni kiasi tu cha kuweka alama za daraja katika daraja lile.

Mheshimiwa Spika, katika Mji wa Dar es Salaam vile vile kumekuwa na majengo mengi yanayojengwa ambayo ni marefu sana hasa pale Kariakoo, kuna majengo mengi sana. Nataka kuuliza je, mitaro ya maji taka itakidhi majengo yale yanayojengwa? Ni jambo ambalo tunatakiwa kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, juzi tumesikia kuna jengo ghorofa 10 limeanguka chini. Wakati uliopita, aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowasa, aliunda Tume, wakati ule kule Chang'ombe kuna ghorofa lilianguka, sijui ripoti ile ilikwenda wapi na ilibaini kitu gani? Yale majengo ambayo walibaini hayako kwenye *standard*, je, yamefanyiwa kazi? Tunapenda ile ripoti iwekwe hadharani ili watu waweze kuelewa kuna matatizo gani.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuongelea suala zima la utalii, hapa sitazungumza mengi sana kwa sababu nategemea kuchangia zaidi Wizara husika wakati itakapowasilisha hotuba yake ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hotuba yake, ukurasa 52, amezungumzia jinsi utalii unavyoweza ukaliingizia Taifa pato kubwa. Mwezi wa pili, tulipitisha Sheria hapa ya kuruhusu wazawa kumiliki biashara ya kupandisha watu Mlima Kilimanjaro na kuwapeleka porini lakini kuna makampuni ya kigeni ambayo hayakufurahishwa na uamuzi ule. Ninapenda Serikali itoe tamko rasmi kuhusiana na hizi ripoti ambazo zimeandikwa na gazeti la *Times On*, la Uingereza pamoja na *East Africa*. Wameandika kwamba, wapagazi 20, hufa kila mwaka. Huu ni uwongo mkubwa na ni upotoshaji mkubwa, ukizingatia Mlima Kilimanjaro sasa hivi kutokana na Kitabu cha Hali ya Uchumi, kinaonyesha kwamba watalii zaidi ya 39,000, walipanda Mlima Kilimanjaro mwaka 2007 na sasa hivi ndiyo *season* inaanza, kwa hiyo, wana ajenda muhimu kabisa ya kufanya wageni waogope kuja kupanda mlima ule wakifikiria kwamba mlima wetu ni hatari kwa kupanda. Huu ni upotoshaji mkubwa na ningemwomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia suala la utalii, sasa naomba niende katika suala zima la elimu. Pamoja na Serikali kwa nia njema kabisa, wametuhamasisha wananchi, tukajenga shule katika kila Kata, ni jambo zuri, sijakataa lakini hatuna sababu ya kujenga kwa haraka haraka kama vile hatuna mipango.

Mheshimiwa Spika, katika Kitabu cha Hali ya Uchumi, takwimu zinaonyesha ni watoto wangapi wamezaliwa, mfano ukurasa wa 89, wamesema mwaka 2007, watoto walioko chini ya miaka mitano, ni 7,241,557. Kwa mpango huu, tunaweza kabisa tukapanga kwamba hawa watoto chini ya miaka mitano, tuna uhakika ukifika mwaka 2011 watakuwa wamefikia miaka saba mathalani. Kwa hiyo, tutajua ni madarasa mangapi tutatakiwa tuyajenge, tuwe tumejiandaa kwa madawati na maabara. Tuandae Walimu tangu sasa ili ikifika wakati ule watoto wanafika miaka saba, tuweze kuhakikisha kwamba tuna Walimu wa kutosha na vifaa vya kutosha kwa ajili ya watoto wale.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, pamoja na matatizo ya Walimu lakini pia kuna upungufu katika mipango yetu. Unakuta kuna Walimu Wakuu wa Shule, ni Walimu wa Sayansi, *Biology*, kuna shule zingine Walimu Wakuu hawa hawafundishi, sijui ni kwa nini hawafundishi! Wakichukua masaa mawili kufundisha wanafunzi kutakuwa na tatizo gani? Kwa namna moja ama nyingine, hii inaweza ikasaidia kupunguza tatizo hili la uhaba wa Walimu endapo kama Walimu hawa wangeweza kufundisha. Shule nyingi Walimu Wakuu, Wasaidizi pamoja na Wakuu wa Utawala, hawafundishi wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna huu mtindo ambao upo katika Wizara ya Elimu, wanawahamisha Walimu na kuwapeleka kufanya kazi Wizarani, nafikiri hapa si sawa. Kuna watu wanaoweza kufanya kazi zile za Wizarani na Walimu wakarudi kwenye *field* na hasa ukiangalia kuna matatizo ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, nina mfano hai kabisa katika Shule ya Sekondari ya Tambaza, wamemhamisha Mwalimu wa *Physics*, Mwalimu wa *Biology* na Mwalimu wa *GS*, wamewapeleka Wizarani, wameenda kukaa kwenye ma-*desk*, wengine wameenda kwenye *Primary Education*, kuna sababu gani ya kuhamisha watu kama hawa ukizingatia kuna shida ya Walimu hasa wa sayansi?

Mheshimiwa Spika, nafikiri kama kigezo ni kuwapandisha cheo au kuwapa motisha, wawape wakiwa kulekule, wawaongezee fedha ili wafanye kazi kwenye Shule zetu. Kama ni kuwapa motisha zaidi basi ile *fifty percent* ya *Teaching Allowance*, irudishwe, hata kama ni nyingi, irudishwe *25 percent* ili Walimu wajisikie nao wamekuwa *motivated*.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujua, je, Walimu wanaenda *study tours*? Hii ni mojawapo ya njia ya kuwa-*motivate* Walimu! Siongelei wale Walimu walioko Wizarani, naongelea Walimu walioko kwenye *field*, hawapati *study tours* kabisa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo suala la afya. Ni vizuri kwamba Serikali imesema itajenga zahanati katika kila Wilaya na katika kila Kijiji lakini ninaomba kwanza zile zahanati zilizopo, zirekebishwe na zihakikishwe zina kila kifaa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukienda kwenye zahanati, wengi wanamaliza kazi saa tisa, ndiyo maana zile hospitali za Wilaya zinakuwa na wagonjwa wengi zaidi. Hizi zahanati zikiweza kufanya kazi kwa masaa 24, kwa kiasi kikubwa, zitapunguza msongamano kwenye hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile wakati Serikali inajenga hizi zahanati, tungeomba vile vyuo vifunguliwe. Kuna vile Vyuo vya Wauguzi vya Manesi, vifunguliwe ili wanafunzi wengi zaidi waweze kwenda katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Afya, wahisani wanajaribu sana kufadhili Wizara ya Afya, kuna fedha nyingi sana zinaenda kule lakini ukimwuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, sidhani kama fedha hizo anazo. Wengi wao, sisemi ni wote, kuna baadhi wanakuja na kusema shirika fulani limesema limeisaidia Tanzania *40,000 Euro*, mfano, ni hela nyingi sana lakini *at the end of the day*, unakuta milioni 38 zinarudi kwao, wanaleta wataalamu wao hapa, wanazitumia na milioni mbili inabaki Tanzania lakini tunaonekana tumesaidiwa sana. Kama kweli wanataka kutusaidia, wapeleke hizo hela Hazina halafu sisi tutaziangalia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, ninapenda tu kuongelea kwa haraka haraka kuhusu wawekezaji. Kuna wawekezaji wa Kichina ambao wamekuja Dar es Salaam, wamefungua gereji kila mahali, wanakwangua magari na kadhalika, hata ile kukwangua gari unakuta ni Mchina anakwangua, hivi tunahitaji Mchina kuja kukwangua gari hapa Tanzania? Sidhani kama tunahitaji watu wa namna hiyo kwa sababu kuna vijana wetu ambao wanasoma *VETA* na wanaweza wakafanya kazi hizo. Ninapenda kujua Sheria ya Kazi, inawaruhusu walete watu wangapi kufanya kazi hizo na

wanaruhusiwa kufanya kazi kwa muda gani? Unakuta kazi nyingi ambazo zingefanywa na wazawa, wageni wanakuja kufanya kazi hizo. Ninaomba Serikali iangalie suala hilo na walifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, magari mengi ya Serikali yamekuwa yanaenda kutengenezwa kule. Zamani tulikuwa na *TEMESA* lakini imekufa. Nafikiri ni wakati muafaka sasa wa kufufua *TEMESA* ili tuweze kupunguza matumizi ya Serikali. Magari mengi mabovu unakuta yapo kule *TEMESA* na vijana wetu wa *VETA* wanaweza kuja kufanya kazi kule. Serikali iangalie ni jinsi gani ya kufufua *TEMESA*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matumizi ya Serikali, naomba Waziri Mkuu wakati ana-*wind up,* atueleze ni mara ngapi Serikali inafanya *stocktaking* ya vitu vyake, tungependa kujua hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda niwapongeze Wabunge wote kwa jinsi wanavyochangia na kujaribu kutetea Majimbo yao. Kila Mbunge hapa ndani anasema anataka rasilimali inayopatikana, sehemu inakotoka, *percent* ibakie pale. Hili ni jambo zuri na inaonyesha jinsi gani wameweza kuielewa sera yetu nzuri ya CHADEMA ya Majimbo, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru na ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ili niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na wataalamu wake wa ofisi yake kwa kutuandalia bajeti ambayo ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, nataka nianzie na sekta ya mifugo ambayo imetajwa katika ukurasa wa 54, fungu la 79. Sasa ni zaidi ya miaka 20, tunazungumzia kwamba nchi yetu ni ya tatu katika Bara la Afrika kwa kuwa na mifugo mingi, zaidi ya milioni 18. Sensa ya mwisho ya mifugo sijui imefanyika lini lakini hapa katikati kuna matatizo, mifugo imekufa kwa wingi sana kutokana na ukame, magonjwa mbalimbali, mifugo kutupa mimba, mambo yote haya yanapunguza idadi ya mifugo. Nataka nishauri kwamba ni vizuri tukapata takwimu za *up to date* kuhusiana na idadi ya mifugo tuliyonayo hapa nchini, maana tunaambiwa sisi ni watu wa tatu baada ya Sudan na Ethiopia.

Mheshimiwa Spika, mifugo yetu hata kama ni mingi lakini haileti tija sana katika uchumi wa Tanzania. Mifugo kwa sisi wengine ambao tunakaa mipakani kama Mikoa ya Arusha na hasa tunaopakana na Jamhuri ya Kenya, mifugo mingi sana inakwenda huko na hii ni kwa sababu hatuna mkakati wa dhati wa ndani wa kuboresha sekta ya mifugo pamoja na masoko yake.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma, tulikuwa na soko kubwa sana la mifugo huko Kilimanjaro lilikuwa linaitwa Weruweru, sijui hii imeishia wapi? Lilikuwa ni soko

kubwa sana la ndani, sijui limekufa namna gani! Kama kuna uwezekano wowote tufufue soko hilo kwa sababu ni soko kubwa la ndani na kuweka masoko mengine katika maeneo ya mipakani kama kwangu kule Loliondo sehemu za Ngarisero.

Mheshimiwa Spika, hatuna viwanda vya nyama, ngozi, hata viwanda vya maziwa hatuna, kwa hiyo mazao ya mifugo yanayopatikana yanapotea tu na badala yake yanakwenda katika Jamhuri ya Kenya kwa sababu vitu vyote hivyo kama viwanda, wao wanavyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile hakuna miundombinu, majosho, madawa na hata kama yapo, ni ghali sana kwa mwananchi wa kawaida kuweza kuyanunua. Siku za nyuma tulielezwa na Serikali kwamba kulikuwa na pesa ambazo zingetolewa na *World Bank* na sisi tukaambiwa kama alivyosema mmoja wetu hapa kwamba tulijipanga kuainisha vijiji 10 kwa ajili ya kunufaika na mradi huu wa *World Bank* ambao ungeshughulikia suala zima la maji, lakini kama tunavyosema fedha za wafadhili kwa kweli haina uhakika, siyo wote, lakini kwa sehemu kubwa wanakuwa na nia njema lakini wakati ule tukihitaji hiyo pesa inakuwa haiji kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, pesa hiyo sasa ambayo tulikuwa tuanze kuchimba mabwawa na hasa kwangu kule sehemu za Mbugani ili waweze kunufaika na mifugo na wanyamapori, pesa hiyo mpaka leo hatujaiona. Tunaambiwa sasa kuna mambo ya *Quickwins* na *Cuickwins,* anayewahi ndiye anayepata. Sasa ni vizuri kungekuwa na utaratibu mzuri wa kunufaika na pesa hiyo ya *Quickwins*.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kufahamu, katika bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ni kiasi gani kimetengwa maalumu kwa ajili ya mifugo, kwa sababu kama kimetengwa kiasi fulani cha fedha na pesa hii ikaenda kwa walengwa ambao ni wafugaji wenyewe, wakubwa na wadogo na wenyewe wakakaa na kuibua miradi ya mifugo, wanaweza wakashiriki kikamilifu na mara nyingi wafugaji huwa wana tabia ya kuhamahama. Kwa hiyo, kama Kamati ya Wilaya inayoshughulikia Kilimo na Mifugo, hawapo basi sehemu kubwa ya mifugo inaenda kwenye kilimo na mifugo inakosa bajeti yake, lakini kama tukipata pesa tunaweza kulirekebisha haraka sana.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie habari ya utalii. Hili nalo limeelezwa katika hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 52, fungu la 77. Wilaya ya Ngorongoro, ni kubwa na ina maeneo mengi mazuri sana ya kuwekeza shughuli za utalii. Lakini sehemu kubwa ya Wilaya ya Ngorongoro ni ama hifadhi ya Ngorongoro au ni *game controlled area* kwa maana ya Loliondo *game controlled area*.

Mheshimiwa Spika, eneo la hifadhi ya Ngorongoro lina kilomita za mraba 8300 na eneo lile lingine lililobaki ni kilomita za mraba 5700 na kufanya jumla ya kilomita za mraba katika Wilaya ya Ngorongoro kuwa zaidi kidogo ya 14,000. Eneo ni kubwa na shughuli zinazoendelea kule ni za ufugaji, kuna upigaji wa picha, kuna *camp sites*, kuna *Lodges* na kuna uwindaji wa kitalii kwa maana ya *hunting blocks* na kuna kilimo kidogo ambacho kinafanyika nje ya hifadhi lakini pia nje ya maeneo ambayo yapo chini ya *game controlled area.*

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa hapa tulilonalo ni makampuni mbalimbali yanayoingia katika maeneo yale na yanaingia katika mikataba na wanakijiji. Ile Halmashauri ya watu 25 na Mwenyekiti wake, wanakaa na hao wenye makampuni na nyingi ya kampuni hizo ni za Kizungu, wanaingia mikataba kama ile mikataba ya Karl Peters wa miaka mingi iliyopita, wanadanganya watu, wao wana Wanasheria wao lakini katika Serikali ya Kijiji hakuna Mwanasheria huko, hata Halmashauri zetu, tuna Mwanasheria wa Halmashauri lakini hawawasaidii kuingia mikataba ili kugundua kama mkataba huu una walakini au hapana. Matokeo yake ni kwamba sehemu kubwa ya ardhi inachukuliwa na baadaye wananchi wanajikuta wamedanganywa lakini wameshasaini mikataba, inakuwa ni mgogoro kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali na hasa Wizara inayohusika na utalii ije na utaratibu wa Kampuni hizi zinazochipuka tu zinakwenda kusaini mikataba, kwa kweli kwa sehemu kubwa wanadanganya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kule Loliondo, kuna kampuni zaidi ya 17 na kule wananga'ng'ania kwa sababu maeneo yangu kule hasa Loliondo sehemu za Sukenya, Loloso, Soitambu, Uloipire, kote kule ni sehemu kubwa ya *Serengeti National Park.* Kwa hiyo, ile *immigration* ya *wildebeests* wanapokuja mwezi wa pili hadi wa tano kuja kukaa kwenye ile *plain*, ni lazima wataingia katika maeneo yale. Kwa hiyo, haya makampuni bila kulipa kodi ya Serikali wanaingia huko kwa sababu leseni zao zinawaruhusu kupiga picha lakini wanakwenda kufanya *loggers*, wanaweka *camps* na Serikali haipati kitu chochote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sekta hii kwa kweli ingeweza kunufaisha Taifa zaidi katika kupata pato kubwa zaidi katika uchumi kama wangedhibitiwa na kusimamiwa. Makampuni yenyewe ni *NOMARD*, *THOMASON*, *CC AFRICA*, *HOOPER*, *SOKWE*, *DOROBO,* kutaja machache tu lakini yapo mengi zaidi ya 17.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mkuu wa Wilaya huko anajitahidi kuangalia ni makampuni gani yana leseni na yanalipa kwa Serikali kile ambacho Serikali inataka na wale ambao wanaingia kinyemela na kubebana maana kampuni moja inaweza ikawa inabeba kampuni tatu hadi tano mgongoni, hii kwa kweli inatakiwa isimamiwe kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri Mkuu, ni nzuri na imetufurahisha sana kwa kujali maslahi ya Madiwani wetu, kwa kuangalia posho zao, matibabu, mazishi na usafiri.

Mheshimiwa Spika, Wilaya Ngorongoro ina kero mbalimbali na ninataka hili nisisitize kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba tarehe 20/8/2008 na 23/8/2008, tulipokuwa tunamaliza Bunge la Kumi na Moja, nilikuona ofisini kwako na nikakueleza tatizo la usalama ambalo lipo katika Wilaya ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa kule, kwa kweli wamepata matatizo makubwa kutokana na hawa wawekezaji. Mwekezaji anaingia katika eneo anaweka *fence,* inakuwa

ni marufuku mifugo kuingia kule kupata nyasi na kupata maji na ni eneo hilo hilo tu mambo haya yanapatikana kwa wingi zaidi. Eneo la Sukenya limeleta mgogoro mkubwa sana na ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu baadaye ulitolee tamko suala hili kwa sababu katika mambo haya, watu wanapigwa risasi huko na wale Maaskari wa Makampuni wanashirikiana na Maaskari wetu wa Polisi wakizidiwa huko wanawaita na wale wanalipwa kitu kidogo, hawajalishi tena kuwauliza watu ni namna gani yametokea, wanaishia kupiga watu risasi.

Mheshimiwa Spika, watu wangu wamepigwa, wanne wameuliwa kwa nyakati tofauti katika sura hiyo hiyo. Suala la usalama kwa kweli ile dhana ya kusema kwamba jukumu la Serikali ni kuangalia usalama wa watu na mali zao, najua ni watu wachache, siyo Serikali yote. Lakini ni vizuri hawa nao wakaangaliwa wakashughulikiwa kadri inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kero ya barabara, Mheshimiwa Rais alikuja Jimboni na kila Mbunge anayesimama hapa anaeleza kwamba wakati Rais anafanya kampeni alitoa ahadi na baada ya kampeni alitoa ahadi. Sasa tufike mahali ahadi za Rais zitekelezwe! Mimi sijui kuna matatizo gani kila Mbunge ambaye Rais amepita Jimboni kwake kuna ahadi imetolewa, sasa hivi ahadi za Rais sizianze kuwa kero na Rais asije akaonekana anatoa ahadi ambazo hazitekelezeki. Mimi nimeahidiwa barabara tena ya lami kutoka Mto wa Mbu – Kigongoni kupitia Ngareselo kwenda Loliondo mpaka Musoma. Ni barabara muhimu sana. Tungeondokana na adha ya watu kupita ndani ya hifadhi ya Ngorongoro pamoja na Serengeti. Hiyo barabara ingepita wanakoishi wa watu.

Mheshimiwa Spika, lakini niliahidiwa pia umeme mpango wa *TANESCO* huko nyuma kwa Wilaya ya Ngorongoro ilikuwa tupate umeme mwaka 2015. Lakini Rais alipopita kule alipoahidi tukajua angalau tungepata hata ya *generator* wakati tunasubiri umeme wa *grid* ya Taifa. Lakini mpaka leo nataka nianze kuamini sasa kwamba kutokana na kutotekelezwa ahadi ya Rais, kumbe nakwenda huko huko 2015.

Wakati mimi nina vyanzo vingi vya umeme, umeme ungeweza kutolewa Mgumu, umeme ungeweza kutolewa kule Mto wa Mbu ungeweza kutolewa katika Mto Pinyinyi kwa sababu kuna maporomoko ya kuweza kuzalisha umeme, lakini inawekwa mpaka mwaka 2010. Hata inapingana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kusema Makao Makuu ya Wilaya kufikia kipindi fulani ziwe zimepata umeme. Sijui kama tutafika huko, lakini nadhani Serikali iko hapa imesikia, tunaomba ahadi za Rais ziweze kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, lango la Ngorongoro ni eneo pekee ambalo ukitaka kuingia Ngorongoro ni lazima upite kwenye lango lile. Wanaita Lololyageti. Naunga mkono utaratibu wa kudhibiti watu wa kuingia katika eneo lile kwa sababu eneo la Ngorongoro siyo la kitaifa tu lakini pia ni eneo la kimataifa.

Kwa hiyo, *screening exercise* kwa ajili ya usalama iendelee. Lakini pia isije ikageuka sasa kuwa kero kwa wananchi. Wananchi wa Tarafa ya Loliondo, Tarafa ya Sale wakiwa na vibali vinavyotakiwa, wakishaonyesha waruhusiwe kupita na hata bila

malipo kwa sababu ni watu wanaokaa katika Wilaya ile ile. Lakini kwa magari yenye tani sifuri hadi saba wanatoza Sh. 20,000/= na zaidi ya pale 25,000 magari madogo ni Sh. 10,000/=.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli nimeisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naweza kusema kwa sehemu kubwa imejielekeza kwenye mkataba wetu na wananchi ambayo ni Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005. Mimi katika mchango wangu nitazungumzia masuala ya Mkoa wangu wa Kigoma, Wilaya ya Kigoma, Jimbo la Kigoma Kusini na kwenye maeneo mawili muda ukiruhusu nitazungumzia masuala ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, umesema ulipepesa pepesa macho hapa ukawa hukuniona kwa hiyo ukaruka jina langu, ni kweli, haiamkiniki unakuja hapa unazungumza vitu bila kuwa umecheki kupata taarifa sahihi kutoka kule unakozungumzia. Karibuni Wabunge wote wa Mkoa wa Kigoma, tulikuwa tumetoka hapa, tulikuwa na *briefing* na Mkuu wetu wa Mkoa.

Kama itakumbukwa mwaka jana nilieleza kwenye hoja hii ya Waziri Mkuu nilieleza kwamba hebu mtuachie Mkuu wa Mkoa tuendelee kuwa naye, tunamhitaji. Kwa kweli tunamhitaji. Mkuu wetu wa Mkoa amejitahidi sana kuweka hali ya usalama katika Mkoa wa Kigoma. Mwaka 2004 ilikuwa *IGP* hawezi kuwasilisha taarifa ya Usalama wa Taifa kwenye ngazi za juu kabla hajajua kuna nini Kibondo, Kibondo kila siku kulikuwa kuna tukio ambalo halikuwa nzuri kiusalama.

Leo hii kwa mwaka mzima wa 2007/2008 kumekuwa kuna matukio 16 tu. Hii ni kazi imefanywa na vyombo vya usalama katika Mkoa wa Kigoma chini ya Uongozi wa Mkuu wa Mkoa tuliyenaye. Ameweza kuvisimamia vizuri na upo usalama wa kutosha. Hatusemi kwamba hali ni shwari kabisa, lakini angalau tunaweza tukatembea tukiwa tunajiamini. Kwa hiyo, hilo ni moja ambalo nasema tuachiwe bwana huyu tuendelee kuwa naye aweze kutuwekea yale ambayo sisi tunatarajia kuyapata kutoka kwake na wananchi wote kwa ujumla.

Hata hivyo ningeomba Waziri Mkuu atambue kwamba Ziwa Tanganyika, ambalo na yeye linamhusu katika Mkoa wake, hali sio nzuri sana. Kuna uharamia unaofanywa na wenzetu kutoka *DRC*. Wavuvi katika Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Rukwa wananyang’anywa sana zana zao na wenzetu kutoka upande wa pili.

Ni kweli zipo juhudi ambazo Mkoa unafanya za mikutano ya ujirani mwema ambayo wanakutana kuangalia namna ya kuweza kuondoa tatizo hili. Tunashukuru sana vikao vilivyofanyika hivi karibuni tumeweza kurudishiwa zana ambazo wavuvi wetu

wamenyang'anywa na maharamia kutoka *DRC*. Lakini tunaomba basi, Serikali iendelee kusimamia suala hili ili wavuvi wetu wavue kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la usafiri wa reli na nadhani hata hili na wewe linakugusa. Kikao cha mwisho cha Bunge kilichopita hapa cha Mkutano wa Kumi na Moja Mbunge wa Mpanda - Mheshimiwa Arfi, alitoa hoja binafsi na ile hoja ilikuwa inahusu hasa adha wanayoipata wasafiri wanaotumia huduma za Shirika la reli. Nieleze kwamba mwekezaji huyu ambaye tumempa kwa mkataba wa miaka 20 kama sikosei kwa upande wa kusafirisha mizigo anafanya vizuri sana.

Taarifa nilizonazo ni kwamba, sasa hivi utaratibu wa kufikisha mizigo Kigoma kutoka Dar es Salaam kabla hajachukua ilikuwa inachukua mwezi mzima. Sasa hivi ni wiki moja. Kwa hiyo, upande wa mizigo wanafanya vizuri. Lakini sisi tunaotumia reli ya kati hatuna usafiri mwingine wowote mahususi wa kutupeleka Kigoma; ni zaidi ya reli. Leo hii pengine nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu amwambie Waziri wa Miundombinu, kwamba kila abiria anapoingia kwenye treni sasa apewe vidonge maalum vitakavyomzuia asiweze kupata haja ya kwenda chooni mpaka anafika Kigoma kwa sababu abiria wanashonana kiasi kwamba hawapati muda wa kwenda kupata huduma hiyo ambayo ni huduma muhimu katika maisha ya binadamu. *(Makofi)*

Sasa mwekezaji huyu anadhani anachukua abiria Tanzania kama vile wanavyopanda treini kule India? Sivyo! Kwa hiyo, ningeomba Serikali ikae itazame upya kwanza idadi ya treini zimepunguzwa zile safari na sisi ndiyo usafiri pekee tunaoutegemea. Juzi nilikuwa nasoma kwenye gazeti, kwanza aligomea kutoa huduma kwenye reli ya Tanga, juzi ilipofunguliwa anasema kumbe ina faida kubwa, yeye faida kubwa kwake ni mizigo tu siyo abiria, huduma kwake anaona ni ya mizigo. Sasa Serikali iangalie namna ya kutuhudumia sisi watu tunaopanda treini kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma ambayo inachukua na watu wa Dodoma, Tabora ambayo inahusisha na Urambo vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo mikakati ya kufanya Kigoma kuwa *dry port* kwa ajili ya Congo na Burundi na Dar es Salaam iwe *transit port*. Tungeomba Serikali iharakishe hiyo kwa sababu ni fedha nyingi tutakuwa tunazikosa kama hatukufanya uharaka na wenzetu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya *Congo* wanategemea bandari ya Kigoma zaidi kuliko sehemu nyingine. Najua inawekwa mikakati hapa ya kujenga reli ya kwenda Ruanda, tuna *dry port* pale Isaka. Sasa zikiwa mbili hizi moja ikahudumia Rwanda, Burundi na hii ikachukua Mashariki yote ya *DRC* ambayo inaanzia Kaskazini kule ya *DRC* ambayo ni Baraka kwenda mpaka Moba, tunayo biashara kubwa sana Tanzania ya kufaidika na *dry port* pale Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Kigoma kabla ya mkakati huu wa kujenga sekondari za Kata haujaanza tulikuwa nazo sekondari 34 kwa Mkoa mzima. Lakini kwa juhudi za wananchi, michango ya wananchi chini ya viongozi wao wakiwemo na Waheshimiwa Wabunge wote chini ya uongozi thabiti wa Mkuu wa Mkoa tuliyenaye sasa hivi tunazo Shule za Sekondari 88. Hawa viongozi wana tafsiri vizuri utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Sasa pamoja na kuwepo shule hizo ni vizuri shule hizi zikapata walimu. Tumesikia zimetolewa kauli na Wizara ya Elimu, kwamba wameamua kuondoa mitihani ile ya kuwapima vijana Darasa la Nne na Kidato cha Pili. Mimi siamini kama ni uamuzi sahihi. Lakini nadhani ni uamuzi kutokana na kwamba hatuna walimu wa kutosha kwa hiyo, unawatahini watu kwa kitu ambacho hukuwafundisha, utawatahini nini? Kwa hiyo, Wizara ifanye utaratibu mahususi wa kuongeza walimu na walimu hasa wapelekwe kwenye maeneo ambayo yana mazingira magumu. Moja ya maeneo hayo ni jimbo la Kigoma Kusini. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara ya Elimu kwa ujumla ilione hilo. *(Makofi)*

Lakini kwa hili la elimu liko suala la *VETA* tunatambua *VETA* imehama kutoka Wizara moja kwenda Wizara nyingine, ilikuwa chini ya Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana sasa iko chini ya Wizara ya Elimu. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aelekeze basi, pale Kigoma sisi tuna *boat yard* pale, tuna vijana wanamaliza darasa la saba, tuna vijana wanamaliza Kidato cha Nne, vijana hawa tungetaka wakiingia *VETA* wafundishwe kwa mitaala yenye kuzingatia mazingira ya pale walipo kwa sababu kama hatukufanya hivyo unamfundisha mtu kuwa *welder* kuwa *electrician* kuwa *plumber* ataondoka Kigoma kwenda kutafuta kazi sehemu nyingine. Lakini akifundishwa kuwa mtaalam wa kutengeneza maboti ni dhahiri tutahudumia uvuvi zaidi na kwa maana hiyo, vijana hawa watapata ajira pale walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu katika hotuba yake, kuna kitu naweza nikasema ni *oversight.* Imetokea tunalo suala la ujenzi wa barabara za kuunganisha Mikoa na Mikoa na sasa hivi tunajengewa daraja la Malagarasi ambalo litatufanya tusafiri kwa urahisi kutoka Kigoma kwenda Tabora na kwingineko. Katika hotuba yake hakulizungumzia na tayari Serikali ya Korea ambayo inafadhili daraja lile imekwishatoa fedha. Tulidhani katika majumuisho yake atoe kauli. *(Makofi)*

Barabara nyingine ambayo pengine tulitaka aizungumzie ni ya kuunganisha Kigoma na Rukwa kutokea Simbo kwenda Kalya na barabara hii vile vile inahusisha Mto Malagarasi na tunadhani ipo mikakati inayofanywa sasa daraja pale kwenye Kijiji cha Ilagala. Ni vizuri daraja hili lifanyiwe mkakati lijengwe ili lisaidie katika kusafirisha watu mwambao wa ziwa kule ambako shughuli nyingi za kilimo zinafanyika.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba ninukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sehemu ya tatu ambayo inazungumzia haki na wajibu. Niseme, watu ni sawa. Hii ni sehemu ya ibara ya 13 (1), inasema: “watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki mbele ya sheria.” Kuainisha na hiyo, nakwenda kwenye ilani ambayo nimeizungumzia Waziri Mkuu, kwamba amezingatia katika hotuba yake Ilani ya Uchaguzi ukurasa 132, pale panapozungumzia sekta ya sheria kifungu (b) kinasema: “Kulipatia ufumbuzi suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara.”

Hili suala limekuwa linazungumziwa sana. Hivi Serikali inapata kigugumizi gani cha kuanzisha Mahakama ya Kadhi Tanzania? Tunaomba ieleweke, kazi ya Mahakama

ya Kadhi itahusu jamii ya Waislam peke yao. Watu wenye hofu pengine hawafahamu kazi ya Mahakama ya Kadhi. Kadhi atahusika na mambo ya ndoa, talaka na mirathi.

Sasa kuna watu wana hofu na tunaona sasa inajitokeza tabia ya madhehebu mengine kuwa ni wasemaji kwa ajili ya Waislam. Tunaomba Serikali itambue kwamba kwa mujibu wa kifungu hicho cha Katiba ninachosema, Waislam wana haki yao ya Kikatiba na ambayo ni vyema ikatekelezwa. Kuna watu wamediriki hata kwenda Mahakamani kuzuia suala la Kadhi lisiongelewe. Nashukuru sana utawala bora ulioko Mahakamani, umeliona hili. Sasa ni vyema tulione hili. *(Makofi)*

Mwaka 1993 katika Bunge hili, nilizuia hoja ya Waziri Mkuu kuhusu soko la Kariakoo na baada ya hapo likajitokeza suala la Serikali ya Tanganyika, nikawekwa mimi jina la kwanza nisaini kwamba nimeweza kumpa taabu sana Waziri Mkuu. Hainipi faraja mimi kuonekana nimempa taabu Waziri Mkuu, niliwakatalia kusaini karatasi ile. Lakini ningeomba basi ili tusifikishane pabaya na kwa kweli kama hatupati usumbufu, mimi naahidi kabisa katika Bunge hili Mkutano wa Kumi na Tatu nitakuja na hoja binafsi ya kuiomba Serikali ituambie kwa nini inakataa suala la Mahakama ya Kadhi kwa sababu Mahakama ya Kadhi itaamua masuala ya Waislam na siyo wengineo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, naunga hoja mkono, lakini nikitegemea Serikali itanipa jibu ya hili la Mahakama ya Kadhi wakati wa Majumuisho. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Msambya, Wasemaji wangu wa tatu watakaotufikisha saa saba itakuwa ni Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Jackson Makwetta na Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa. Kwa hiyo, tuanze na Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii mchana huu.

Mheshimiwa Spika, nianze na mimi kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa maamuzi waliyochukua kuwasaidia Madiwani wetu, hakika ni maamuzi mazuri sana. Lakini la pili, nimpongeze kwa kweli Mkuu wa Mkoa wa Kigoma kwa kazi nzuri sana anayofanya kwa ajili ya Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri sana ameanza kulisemea kaka yangu Mheshimiwa Msambya, lakini nami naomba niliseme. Kwa kweli nilikuwa nasubiri niliseme wakati wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, lakini nimeona nianze kulisemea hapa sasa. Moja ya kazi ya Serikali yoyote duniani ni kulinda raia wake na mali zao.

Mheshimiwa Spika, mambo yanayoendelea kwenye *Lake Tanganyika* yanatia huruma, wavuvi wetu wanavamiwa kila siku, wanauawa ziwani, hakuna hata mtu mmoja jambo hili linamuumiza. Linasikitisha sana! Lakini pamoja na hayo, wavuvi wetu

wanachangia lita 10 za mafuta kwa ajili ya kikosi cha ulinzi ili walindwe, lakini pamoja na kuchangia, bado hawalindwi, wanauawa kila siku. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, jambo hili lipewe umuhimu wake walifanyie kazi, wale ni raia wa Tanzania wanayo haki kama Watanzania wengine.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kusikitisha, ilipokuja *SUMATRA* kwa ajili ya kutaka kukamata watu, chombo cha ulinzi kilikuwa tayari kwenda kuingia ziwani kuzuia watu wasiende ziwani mpaka walipie tozo ya *SUMATRA*. Lakini chombo hiki wakati watu wanavamiwa, wanauawa na wananyang'anywa mali zao, hakikuonekana ziwani. Jambo hili linasikitisha sana. Naomba wahusika walifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka kuchangia sasa hivi ni dunia ya *TEKNOHAMA*. Dunia tunayoenda sasa ni ya mawasiliano. Kwa hiyo, lazima Serikali ijiandae namna ya ku-*invest* kwenye *TEKNOHAMA*. Katika hili tulipe *priority number one*.

Mheshimiwa Spika, umuhimu ni mkubwa sana, lakini najua Serikali imetenga fedha kwa ajili ya *ICT Backbone*. Lakini ninapata shida kidogo, tumeamua *ICT Backbone,* hii *infrastructure* itunzwe na *TTCL*, ikitunzwa na *TTCL, TTCL* nayo ni *operator*, tunakwenda huko kutaanza kutokea *conflict of interests*. Natamani ingeanzishwa kama *independent* ambaye anasimamia hiyo *infrastructure*, kwa sababu mwisho wa siku haya Makampuni yote ya simu, watu wote watatumia *infrastructure* hiyo. Sasa hawawezi kwenda kupanga kwa mtu ambaye wanashindana naye kibiashara. Kwa hiyo, ningeomba Serikali ilifikirie upya jambo hili ni la msingi kwa huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ninajua Serikali inataka kwenda kwenye vitambulisho vya uraia. Jambo hili lazima liende na mradi wetu wa *postal code*. Umuhimu wa *postal code* ni rahisi kuwatambua watu wetu kule walikozaliwa na kule wanakoishi. Kwa hiyo, sasa wakati wa kutengeneza vitambulisho vya uraia, watengenezaji wanajua kwamba watu hao wanaowatengenezea ni akina nani. Mimi ninachokiona hapa, *effort* zimeanza kuwa tofauti. Kuna watu wanaongelea *postal code*, kuna wengine wanaongelea vitambulisho vya uraia. Ni muhimu sana *effort* hizi ziwe kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, zipo faida nyingi sana za hizi *postal code*, zitawasaidia watu wa mabenki wakitaka kuwakopesha watu, zitasaidia kwenye mambo ya kulipa *utilities* hizi na zitasaidia vitu vingi sana. Lakini *more serious* zitasaidia kwenye suala la kodi, watakuwa wanajua watu wao wanaolipa kodi wako wapi. Ningeiomba sana Serikali jambo la *postal code* pamoja na vitambulisho vya uraia viende kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nilitaka kuongelea matumizi ya Serikali. Najua *TRA* wanafanya kazi nzuri sana na kazi hiyo wanaifanya na makusanyo yameongezeka sana. Lakini pia ukiangalia kwenye vitabu vyetu na matumizi nayo yameongezeka sana. Nilikuwa naangalia mwaka 2003, bajeti ya Serikali ukiweka matumizi ya maendeleo na matumizi ya kawaida ilikuwa *about* trilioni 4.7. Kwa hiyo, nikaanza kujiuliza, ina maana

tulipo sasa, tukiamua kujifunga mkanda tunaweza tukajitegemea, na heshima ya Serikali yoyote duniani ni kujitegemea. Ili watakaokuja hao wanaotaka kutusaidia wasituwekee masharti, naomba sana suala la matumizi ya Serikali liwe jambo la *priority*.

Mheshimiwa Spika, tulipitisha sheria hapa na zipo *circular* Serikalini. Kwa mfano, tunakopesha magari wafanyakazi wote wa Serikali, lakini wafanyakazi wa Serikali wamekopeshwa magari, halafu bado wanatumia magari ya Serikali. Kwa hiyo, tufike mahali kwanza tujiulize, huyu amekopeshwa gari. Mimi ningetamani, basi angekuja na gari lake toka nyumbani limfikishe ofisini, akifika ofisini ndiyo atumie gari la Serikali. Kupanga ni kuchagua.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, kama hatuwezi kusimamia matumizi, hatuwezi kujifunga mikanda. Hakika tutaendelea hivi hivi, tunapata fedha nyingi, bado haziwezi kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nilitaka kuongea habari ya barabara. Tunayo Sheria yetu ya *Road Fund Board*. Ukiangalia sijui kama wenzangu wameliona, kuna fedha nyingi sana tunaziingiza kwenye barabara zetu mvua zikija zinachukua fedha zote. Mwaka mwingine ukianza tunaanza upya. Sasa lazima tufike sehemu tutafute tunaendaje. Mwaka huu wa fedha tumetumia Shilingi bilioni 218, mwaka uliopita tulitumia Shilingi bilioni 101, mwaka ule mwingine tulitumia Shilingi bilioni 73, mwaka mwingine tukatumia Shilingi bilioni 73, maana yake ni nini? Kwa hiyo, ina maana kila siku tunaongeza fedha, lakini fedha hizo zikiingia, mvua inakuja inazichukua. Mwisho wake ni nini?

Mheshimiwa Spika, nimekuja kuiomba Serikali na nipendekeze yafuatayo:- Ningeomba Serikali inikubalie kwenye Sheria yetu ya Barabara, kile kiwango cha asilimia 10 kwa ajili ya maendeleo kipandishwe iwe asilimia 20. Lakini asilimia 20 ya fedha hizi zikipatikana, tusizisambaze, tuamue mwaka huu tunafanyia kazi labda kwenye Halmashauri tano au Halmashauri sita. Nawaambieni hali ya Miji yetu itabadilika.

Ukiwapa leo kwa mfano, Halmashauri ya Kigoma Mjini kilomita tano tu za lami kwa mwaka huu ni kazi kubwa sana ambayo na *face* ya Mji itabadilika. Ukiwapa leo Jiji la Dar es Salaam kilomita 10 tu za lami una uhakika barabara za Mitaani kuna wengine wanahitaji nusu kilomita, mwingine anahitaji kilomita moja, uhakika hali ya Miji yetu itabadilika.

Mheshimiwa Spika, katika *span* ya miaka kumi, miaka 20 utakuja kushangaa. Kwenye barabara hizi za Miji hakuna magari makubwa, unafanya *surface dressing* tu, huhitaji barabara ya gharama kubwa tu, ukiwa na bilioni moja unatengeneza barabara ya kilomita nne au tano za *surface dressing*. Kwa nini hatufanyi haya maamuzi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuliko hizi fedha ambazo tunapeleka kwenye Halmashauri, zikifika wanapitisha greda mvua ikija inachukua fedha zote, tunaanza upya. Matokeo yake tunarudia mle mle ndani maendeleo hayawezi kupatikana. Ningeomba Serikali katika hili waweze kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia lipo suala la barabara kubwa ambalo ningeweza kulisema. Leo Serikali yetu tumefanya kazi moja na ni vizuri mambo mengine yalisemwa. Tulifanya maamuzi sahihi hapa, tukasema tunaanza kujenga barabara tutoke Mtwara kwenda mpaka Mwanza kwa taxi. Tumefanya ndani ya miaka mitano, limewezekana, limewezekana kwa sababu fedha hizi tulikuwa hatuzipeleki kidogo kidogo. Leo huku kilomita tano na huku kilomita 20, waliamua ku-*concentrate* na barabara moja, kwamba tunatoka Mtwara tunakwenda Mwanza. Kwa hiyo, kila kilichopatikana kilikwenda huko na wengine wakasubiri.

Mheshimiwa Spika, lakini nilitaka kusema, mwaka jana tumefanya maamuzi hapa, tulisema tunaanza barabara ya kutoka Manyoni kwenda mpaka Kigoma, tunaanza kilomita 37, *well and good* mawazo mazuri, *so* nilitarajia mwaka huu nione tena angalau kilomita nyingine 60 tuanzie Tabora *towards* Urambo. Kwa kufanya hivyo, tungeweza kufanya vizuri sana. Lakini tukianza kugawa fedha kidogo kidogo huko tunajenga kilomita tano, huku tunajenga kilomita 20, mwisho wa siku *impact* yake itakuwa siyo kubwa sana. Naomba jambo hili wenzetu walifanyie haraka.

**SPIKA:** Waambie walisikie hilo. Rudia kidogo hapo. *(Kicheko)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema, ni muhimu sana sasa kwamba tuamue ku-*concentrate* kwenye barabara moja, tuimalize halafu tuhamie kwenye barabara nyingine. Mimi ninadhani kwa maana ya jiografia ya nchi hii na kwa maana ya biashara hii, ni muhimu sana sasa tuhakikishe tunafika Kigoma, tuhakikishe tunakwenda Bariadi, tuhakikishe tunakwenda Mpanda, tukisha-*concentrate* hapo tutafika huko tunakotaka kwenda.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nilitaka nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, ipo misamaha tumetoa kwenye Makampuni ya Madini kwa ajili ya tozo ya mafuta inayokwenda kwenye *Road Toll*. Tukifuta msamaha ule kwa mwaka tutapata Shilingi bilioni 24. Jamani fedha hizo ni nyingi sana. Zikiingia tukazipeleka kwenye barabara za maendeleo tutaweza kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nilitaka pia niongelee habari ya Bonde la Luiche, duniani kote sasa hivi tunasema chakula kimeanza kupungua. Lakini Mungu ametupa mabonde mazuri, jamani, tu-*invest* kwenye mabonde hayo tutaweza kulisha nchi hii na tutaweza kulisha nchi nyingine. Lakini tusipoamua sasa hatutafika huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nilitaka kidogo niongelee suala la elimu hasa kwa upande wa mitihani. Mimi naomba niweke msimamo wangu *very clear*. Kama kuna mtu anasema anataka tufute mtihani wa Darasa la Nne na wa Darasa la Saba, na mtihani wa Kidato cha Nne, tubakishe mtihani wa kidato cha sita, nasikia wanataka mitihani iwe mpaka Chuo Kikuu mwaka wa tatu kwamba kwingine kote iwe ni *test.* tutaua kizazi hiki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kuna mtu anataka kulileta hili, anataka kuua hiki kizazi. Niambieni ni nani Mbunge au ni nani kiongozi tuliyenaye hapa ambaye amesoma hakufanya mitihani akawa Profesa? Lakini tunataka kuleta hii *society* kwamba watu waende tu kwamba mtoto akianza Darasa la Kwanza mpaka Kidato cha Sita ndiyo afanye mitihani ni wapi katika duniani hii na kwa *standard* zipi katika dunia hii? Ndugu zangu, jamani, watu wengine bado tuna miaka mingi ya kuishi msikiharibu kizazi hiki. Ninawaombeni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye elimu ukishaharibu kizazi kimoja ku-*recover* unahitaji miaka 20 mpaka 40. Ukiharibu tu, umeharibu na hii ni hatari kubwa sana kwa nchi. Ninawaombeni wanaotengeneza sera hizi, tafadhali zisije kwenye Bunge hili. Hatutaelewana! Anayekuja kufuta mitihani ya Darasa la Nne, mitihani ya Darasa Saba, mitihani ya *Form Four* na *Form Two* hatutamkubalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *experiment* katika elimu ya watoto wetu hapana. Ninaomba sana wenzetu watusaidie katika hili. La mwisho, nilitaka kusema jamani, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma tumefanya kazi kubwa sana. Tumeamua kuanzisha *special economic zone* ya Kigoma. Jamani mfano huu wa Kigoma ni ukombozi kwa nchi yetu. Kwa sababu Kigoma tunapakana na nchi nyingi sana, nawaombeni Serikali tu-*invest heavily* kwenye hii *sales* ili ianze sasa. Kwa kweli ikianza na kwa sababu bandari tunayo pale na bandari yetu ya Dar es Salaam na barabara hizi tukazijenga zitakuwa hazina maana kama zile *sales* hazipo. Ninaomba sana wenzetu wa Serikali watusaidie kwenye jambo hili.

La mwisho ni suala la uvuvi. Nimesoma *speech* ya Mheshimiwa Waziri hapa. *(Hapa kengele ililia)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Serukamba kwa mchango wako mzuri sana. Sijalisikia hili la kufuta mitihani. Kuna nchi inafuta mitihani, watu wanakwenda tu. Haya! Mheshimiwa Jackson Makwetta, halafu Mheshimiwa Khalifa atamalizia.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Ndugu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa maoni yangu na ushauri wangu kwa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa, kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na ya kina na ninaomba pongezi hizi ziwafikie wasaidizi wake akiwemo Katibu Mkuu wake Ndugu Mrisho ambaye ni *School Mate and College Mate.* Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Pili, ningependa kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyosimamia shughuli za Serikali ndani ya Bunge na kwa jinsi anavyoratibu maendeleo ya nchi hii tangu ateuliwe kuwa Waziri Mkuu. Sisi wenzako tulio chini ya uongozi wako, wewe na Mheshimiwa Spika tunaona fahari na tunajivunia kuwa chini ya

uongozi wenu na tunaona Mwenyezi Mungu awape afya ya mwili na kiroho ili muweze kutuongoza vyema ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Mkuu asiye na makuu. Lakini kwa jinsi tunavyoona ni msikivu na ni mtu anayetaka mambo yote awe na uhakika kabla ya kuamua. Tabia hiyo ni ngumu kuwa nayo lakini Waziri Mkuu nadhani una bahati nzuri. Dumisha sifa hizo. *(Makofi)*

Ndugu Spika, mimi nimesimama hapa kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu. Lakini nilikuwa na ushauri katika baadhi ya maeneo. Moja linahusu chakula. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 44, naomba nitumie nafasi hii kunukuu sentensi moja, nayo inasema, kwa idhini yako nanukuu.

*"Sisi kama Taifa hatuna budi tujiandae katika kipindi cha muda mfupi na kujiwekea mkakati wa muda mrefu wa kujitosheleza kwa chakula."* Mazungumzo yangu mengi yatahusu sentensi hii. Leo chakula ni dhahabu! Leo na kesho hali itakuwa ngumu zaidi. Tushukuru kwamba Tanzania bado hali haijawa mbaya sana. Lakini chakula ni silaha. Unaweza kumshinda adui kwa kumnyima chakula. Sasa hali ya chakula duniani ni mbaya. Chakula kinapungua, uzalishaji unapungua na mahali pa kuzalishia, yaani ardhi inaanza kutumika kwa mambo mengine zaidi ya chakula. Kwa hiyo, kuna upungufu wa uzalishaji, lakini bei ya chakula, vile vile inazidi kupanda kiasi kwamba hali hii ikiendelea kama ilivyo kwa mafuta, maskini baadaye watakufa kwa njaa. Afadhali kufa kwa ugonjwa kuliko kufa kwa njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili, sisi Watanzania tulikuwa na bahati ya kuwa na ardhi nzuri. Kwa hiyo, tusipotumia vizuri ardhi, tukatapanya au kufuja matumizi ya ardhi katika nchi hii tutakuja kujuta. Nchi yetu kwa bahati nzuri ina sifa zinazotofautiana, na Mungu amefanya hivyo.

Kuna maeneo ya mbuga ambazo zinafaa kwa ufugaji wa mifugo kama haya ya Dodoma, Arusha, Tabora, Singida na maeneo mengine. Haya yanafaa kwa ufugaji wa ng'ombe wa nyama na duniani kote ng'ombe wa nyama wanafugwa katika maeneo ambayo kidogo ni kame kame na nyama ya maeneo haya ni nzuri sana. Lakini maeneo kama ya Nyanda za Juu ya Njombe sio maeneo ya kufuga ng'ombe wa nyama.

Sasa sisi bila kuangalia sifa hizo, tumeanza kusambaza mifugo nchi nzima, hata kule ambako Mungu alikataa. Hivi watu wa Lindi, Ruvuma wanachotaka ni ng'ombe wenye kwato au nyama? Maana tuangalie tukijaza ng'ombe hawa katika mabonde ya Lwiche, Rukwa, Dakawa, Kilombero, Pangani, Rufiji wakajaa humo na wakaua mabonde hayo, tumekwisha. Tulikuwa na bahati ya kuwa na maeneo haya ambayo ni kama eneo, kiwanda cha kuzalishia chakula. Lakini tukipeleka ng'ombe kwato zitaoza, maji yatakauka, ardhi itaharibika na hatutakuwa na mabonde kama haya.

Bahati hii tungeitumia kwa makusudi kwamba haya ni maeneo, hiki ni kiwanda cha kuzalishia nafaka katika mazingira haya ambapo nafaka sasa ni za shida na ni tatizo katika dunia. Hili ni suala la kisiasa. Ng'ombe wamekwenda Ihefu tumesema wahamie pengine. Tunawapeleka Lindi-Mtwara ambako hawana mazoea ya ufugaji, lakini bila

kubadilisha mtindo. Mtindo ni ule ule wa kuchunga na sio kufuga. Mimi sipingi mbinu za kutatua matatizo, lakini napinga mtindo wa kusambaza matatizo. *(Makofi)*

Bila maandalizi imara na ya kutosha ya kutatua tatizo hili la mifugo, tutakuwa tunaaharisha matatizo tu. Leo mahali pengine wakulima na wafugaji wanagombana, lakini hatuwaambii wala hatutatui tatizo, tunasema mkae salama, mkae vizuri. Elimu inatakiwa. Elimu gani wanahitaji? Wote wanahitaji ardhi. Sasa leo mkulima ana eneo linajulikana. Hili ni eneo la shamba la fulani la kilimo na apate *lease*. Huyu mfugaji tunamsema, ana shamba wapi? Anatangatanga nchi nzima. Mara yuko Lindi, mara yuko Njombe, mara yuko Monduli, Mara yuko wapi! Huyu mfugaji utamkuta wapi hata ng'ombe hawa milioni 15 una kauli nao? Ukitaka kuchinja auze nje, una kauli nao kama ulivyo na kauli mtu wa korosho na mahindi na mchele. *(Makofi)*

Nadhani ifikie wakati tuitazame nchi yetu hii na kuigawa katika maeneo kwa kufuatana na mazingira na sifa zinazofaa kwa kitu kipi na kusimamia taratibu hizo. Hata Botswana wana utaratibu. Sasa kwa nini tusiseme kwamba eneo la Dodoma linafaa kwa ufugaji? Kwa makusudi tukasema tutilie mkazo mabwawa na tugawe maeneo tukasema kwamba ninyi watu wa Dodoma Kati, au Mkoa wa Dodoma msilime mahindi. Wanataka walime mahindi, mtama, wafuge mbuzi, kondoo, ng'ombe, kila kitu huyo huyo na ardhi haikubali. Huu mtindo wa mtu mmoja kuwa na ng'ombe zaidi ya 10,000 katika dunia uko wapi? *(Kicheko)*

Maana tuwe wa kweli hapa kwamba kweli unaweza ukafuga ukiwa na ng'ombe 10,000. Lazima uchunge na hii inaruhusiwa tu kwa sababu hapa bado pana parks romana. Yaani amani chini ya Himaya ya Warumi ni kwamba unaweza ukatembea popote pale mpaka wakati mwingine hatujui hata mipaka yetu. Lakini sasa tuanze kurudi kwenye utaratibu wa kisasa wa kufuga mifugo. Tuwe na maeneo na kwa njia hiyo tu unaweza ukaelekeza huduma katika maeneo hayo. Lakini kwa njia hii ya ng'ombe kutembeza nchi nzima kwa kweli tunajidanganya.

Sasa kwa sababu za kisiasa inabidi tujaribu kuzungumza lugha za kisiasa ili tuendelee ku-*survive.* Itatusaidia nini tuki-*survive* wakati mali inaangamia? Kwani kuwa na ushauri huo kwa somo hilo labda niende kwenye somo jingine na hii kwa bahati nzuri ukurasa ule wa 54 na 55 baadhi ya Mikoa imeanza kutenga maeneo ya mifugo na kilimo. Sasa tuwe na nidhamu hiyo na tunahitaji ramani ya matumizi ya ardhi kwa nchi nzima.

Ya pili, suala la elimu amelisema vizuri aliyenitangulia. Labda niseme tu kwamba huenda kuna haja ya kutazama upya muundo wa Wizara ya Elimu ili kukidhi haya mabadiliko. Kisheria elimu ya Sekondari inasimamiwa na Mkurugenzi wa Sekondari kutoka Makao Makuu ya Wizara. Kwa mazingira haya yaliyobadilika haya tunatumia *REO* kama kwa hisani tu. Lakini pale tumeondoa wataalam wote, hana watu. Sasa yeye anasimia *Primary School* na Sekondari na pale tumeondoa *manpower* yote, kule Wilayani tumesema apelekwe Mratibu awe chini ya *DC* wakati wenzake wa Elimu ya Msingi wapo mahali pengine.

Mimi nadhani ni vizuri tukatazama kwa undani, muundo wa elimu wa sasa haukidhi kwa sababu mambo yamebadilika. Kila Wilaya ina zaidi ya sekondari labda 50 au zaidi. Sasa katika mazingira haya muundo ungali ule ule. Nitapata nafasi labda katika Wizara inayohusika, lakini tumepiga hatua kubwa, ila matatizo ni mengi na makubwa. Kufuta mitihani katika mazingira haya ambapo walimu ni wachache na matatizo ni mengi nadhani kutaathiri zaidi elimu kuliko njia nyingine.

Kwa sasa mwalimu anajilazimisha kufundisha kwa kuangalia shule jirani kwamba ooh! Wenzangu walipasi mwaka jana na mimi nisipopasisha nitatazamwa vibaya na hatuna wakaguzi wa kutosha. Leo tena njia hii ambayo inakusaidia kusimamia walimu unaifuta, walimu wote watakuwa wanasuka nywele au wanakwenda kufanya biashara na utapoteza kabisa hata nia. Utakuwa unapitisha watu tu katika miaka kutoka Darasa la Kwanza mpaka darasa la mwisho wakiwa hawana elimu. *(Makofi)*

Ningependa hili suala la upandaji wa mafuta nimalizie kwa vile muda utaniruhusu, kwamba hivi sisi tunafanyaje? Nilidhani njia mojawapo muhimu ambayo itawafanya Watanzania waendelee kuishi na kusafiri na kuzalisha chakula na kufanya biashara ni kufufua na kuimarisha usafiri wa reli. Tuna *TAZARA*, tuna Reli ya Kati, tuna reli inayokwenda *North.* Njia hizo zinatumia mafuta kidogo zaidi na usafiri wa mabasi makubwa mijini na Mikoani. Njia hizi za kutumia usafiri wa magari madogo zitatumaliza kwa sababu tunaleta magari bila mafuta.

Kwa kuwa muda hauruhusu ningependa vile vile niseme kwamba baadhi ya mambo muhimu ambayo yanagusa nchi yetu kwa mfano ujenzi wa nyumba katika miji, hizi nyumba fupi au ndogo ndogo au *bungalow* unasababisha umaskini,kwa sababu kila unapopanuka ni kuwafukuza walima. Njia ya kujenga maghorofa katika miji ndio njia ya kisasa. Vinginevyo tutafikia wakati ambapo miji yote ya Tanzania itaungana na hapatakuwepo mahali pa kulima. *(Kicheko)*

Nimalizie kwa kusema kwamba huenda ni vizuri wakati umefika kwa Wizara au Serikali kuanza kuzungumzia madhara ya ongezeko la joto duniani. Hii agenda ni muhimu na haisemwi popote, wakati tishio linaonekana ni kubwa zaidi. Ni agenda ambayo inatakiwa kwa sababu tunadhani kwamba endapo hali hiyo itakuwa ni kweli hata kilimo kitaathirika na mambo mengi yatazuka.

Kwa Jimbo langu la Njombe naomba nimalizie kwa kusema kwamba tunahitaji Makambako kuwa mji ili tuweze kumudu zaidi na Lupembe, Njombe tujenga barabara ya lami. Ni eneo ambalo udongo wake ni mgumu, lakini ndio eneo linaleta uchumi wa hali ya juu kuliko mahali pengine popote katika Mkoa wa Iringa. Kuna chai, kuna mbao, sasa magari wakati wa kifuku yanakwama na chai tunamwaga njiani na magari ambayo yanakwama.

Hizi ni njia za lazima za kuimarisha uchumi na ni kama ile njia ya kuimarisha uchumi wa kijiografia. Tupeleke mahali ambapo tutapata fedha haraka, itusaidie kule ambako kiuchumi labda sio kuzuri sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kusema kwamba mkakati wetu wa kuboresha huduma kama tiba elimu uambatane na kuimarisha uchumi. Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Seneta Makwetta. Inapendeza kuwa na watu kama hawa na unapata mambo yenye uzoefu mzito. Basi tutamalizia na Mheshimiwa Khalifa.

**SPIKA:** Vipi yakhe! Leo namna gani?

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru dua zako hizo zimesaidia. *(Kicheko)*

Nakushukuru kwanza kwa kunipa fursa hii kuwa mchangia wa mwisho wa asubuhi hii. Lakini na pia na mimi nipate fursa ya kusema katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba nitangulize maneno machache yafuatayo. Kwanza naipongeza hotuba yake, ni nzuri sana. Nami nimekuwa Bungeni hapa kwa kipindi cha tatu hiki, nimefurahishwa sana na hotuba hii ya jana. Napenda nitumie fursa hii vile vile kusema yale yaliyosemwa na upande wa Upinzani, ni mazuri na nia ni nzuri vile vile.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Kiongozi wa Serikali Bungeni ambaye kwa uzuri sote tulimchagua pamoja. Tungeweza kumkataa siku ya kupigiwa kura, lakini kwa sababu ya kumwamini, kumheshimu na kuona ni mwenzetu tukampa kura zote. Sasa tuna kila haki ya kumwuliza. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Rais ni Rais wetu sote, akishakula kiapo tu, ni wetu. Sasa ni kweli kuwa Rais ametokana na Chama cha Mapinduzi na Serikali imeundwa na Chama cha Mapinduzi, lakini ni ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Sisi tunataka iwe imara, tunaiuliza na tunaihoji kwa madhumuni tu ya kuifanya iwe Serikali madhubuti, tumjengee heshima Rais wetu. Katika hotuba ya Waziri Mkuu sikuona kuzungumzia sana suala la maafa.

Napenda niseme kidogo katika suala la maafa. Kitengo hiki mimi napendekeza sasa kiongezewe nguvu, isiishie tu pale ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini kitawanyike hasa katika Jeshi la Polisi kwa zile sehemu ambazo zinapakana na Bahari au Maziwa.

Mheshimiwa Spika, utafiti nilioufanya katika kipindi cha miaka 18 iliyopita baina ya maafa yaliyotokea baharini baina ya Unguja - Pemba, Tanga - Pemba, Mombasa-Pemba ni mengi. Lakini naomba nitaje maafa ya Boti kama nne hivi.

Mwaka 1990/1991 ilitokea maafa ya boti moja inaitwa Kabuli ilikuwa ikitoka Unguja kuja Pemba, ilikuwa na abiria zaidi ya 50. Wote walikwenda. 99 ilitokea ajali ya boti nyingine ya Mtambwe ilikuwa na abiria kama 35 – 40 wote walikwenda.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 ilitokea ajali ya boti moja inaitwa Nasukuru ilikuwa ikitoka Tanga kuja Pemba ilikuwa na abiria 37. Walikufa 35 wakapona wawili na mpaka sasa wapo.

Juzi boti hii inayoitwa *Spider* iliyokuwa ikitoka Tanga kuja Pemba ilipata ajali, kulikuwa na abiria 22 na 30 kwa sababu ya ile kurashiarashia huyu anaomba apate, huyu anaomba asafiri. Lakini watu hawa wanapoteza maisha yao. Haionekani kwa maoni yangu kuwa kuna mkakati wa makusudi inapotokea ajali kama hizi ku-*save* maisha ya watu hawa. Sasa ni wajibu wa Serikali basi kuangalia usalama wa maisha ya watu wake. Israel wamepigana na Hisbulla kwa askari wao wawili tu waliotekwa wala hawakuuliwa, walitekwa. Lakini nchi iliingia vitani.

Sasa kama sisi hatuwezi kujiandaa kuokoa maisha ya raia kama hawa na inasikitisha kwa sababu taarifa katika maafa yote haya inatolewa, lakini hakuna hatua inayochukuliwa yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii boti ya juzi tumechukua hatua zote za kutoa taarifa. Sasa mimi najiuliza, basi hivi hizi helkopta za Polisi zilizopo zinafanya kazi gani kama sio kazi kama hii angalau kupita wakaangalia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano wa boti hii ya Nashukuru iliyotokea mwaka 2003. Wale *survivors* wawili tuliowapata wanatueleza kuwa watu walikufa siku ya tano ya baharini, maana yake walikaa siku saba. Siku ya tano ndiyo watu wanapoteza maisha kwa njaa na baridi ya baharini. Taarifa tumetoa. Sisi wengine tulikuwa tayari kuchangia mafuta ili boti kama zipo za Serikali zitoke zikawatafute wenzetu wale. Hakuna hatua iliyochukuliwa. Sasa inaonekana tunahafifisha vitu vizito ambavyo vinahusu wananchi wetu. Wananchi ndio raslimali.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kupitia kwako Kitengo hiki akitazame, akiimarishe ili mambo kama haya yasiweze kutokea tena. *(Makofi)*

La pili, ningependa kidogo kuzungumzia kuhusu simu. Juzi hapa kwenye bajeti na kwa bahati nzuri tumeambiwa yale maeneo ambayo yamezungumzwa na yana uwezekano wa kufanyiwa marekebisho, basi yatafanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, simu imeongezewa malipo au kodi kutoka asilimia saba kwenda 10. Ni hatari kubwa! Hivi sasa katika wakati huu tulionao hii asilimia saba ukiangalia sisi ambao ni *member* wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wenzetu Kenya wana makampuni kama mawili, au matatu na wao wanatumia senti 10 za dola kwa dakika moja katika *Air Time.* Sisi hivi sasa tunatumia zaidi ya senti 30 za dola kwa malipo ya dakika moja ya *air time.*

Mheshimiwa Spika, inatisha kwa sababu bei au gharama ya matumizi ya simu katika Tanzania ni ya pili katika dunia nzima inatanguliwa na Uturuki tu. Watafiti wapo hawafanyi utafiti. Sasa ikiwa katika asilimia saba hali ni hiyo tu, tunakwenda asilimia 10! Mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu wewe ndiyo Mkuu wa Shughuli za

Serikali katika nchi yetu, naomba uliangalie hili na ikiwezekana utusaidie sana vinginevyo hatutafika. Kwa sababu *disparity* ya namna hii itakuja kuwapa fursa makampuni ya wenzetu waweze kuchukua nafasi wakiwa huko huko kwao. Sasa hii ni hatari. Ni vizuri sana tukajua hili.

Lakini la pili, baya zaidi makampuni hapa yapo matano. Lakini bei haishuki. Hata sokoni tu ikiwa samaki wapo wengi wanashuka bei. Mihogo ikiwepo mingi sokoni inashuka bei. Hivi haya makampuni yana-*catel* ya namna fulani ambayo Serikali haijui! Hebu yafuatilieni! Vinginevyo tunaumia. *(Makofi)*

Sasa napenda nizungumzie kidogo kuhusu *Vodacom. Vodacom* mimi nafikiri wana bahati. Sasa sijui bahati hii imepangwa itokee! Kama imepangwa ni kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, *Vodacom* katika miaka mitano ya kwanza, wamesahemewa *income tax.* Wamesamehewa *Co-operate tax, okay* labla walikuwa wanaanza, ni *Vodacom* peke yao. Lakini kwa bahati, nipende kusema tu, *VAT* wanayolipa *Vodacom* kwa mwezi ni baina ya shilingi bilioni 80 na bilioni 60 *VAT.* Ikiwa wanalipa bilioni *60 let us say* wanalipa shilingi bilioni sita na nane tujalie wanalipa bilioni 6. Kwa mwaka maana yake ni Shilingi bilioni 72 katika *simple arithmetic* unajua, 6 x 12 ni 72. Lakini sasa *VAT* ni asilimia 20. Ina maana ukizidisha mara tano *simple arithmetic* inatuambia, saba mara tano ni 35, maana yake ni shilingi bilioni 350. Unawasamehe kodi hiyo watu ambao wanatengeneza pesa safi, shilingi bilioni 280 kwa mwezi. Hii si kuwakosesha wananchi haki yao ya kupata kodi? *(Makofi)*

Lakini la pili hutengenezi *fair playing field* baina ya kampuni hii na makampuni mengine. Kinachosikitisha zaidi ni hii kampuni imeongezewa tena *tax holiday* hii ya *income tax* na *corporate tax* kwa miaka mitano mingine kinyemela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza leo hapa, amri hii ametoa nani? Kwa idhini ya nani bila ya Bunge hili kujulishwa? Ni hatari kubwa! Hatuwezi kufika kwa namna hii! Kwa sababu inaonekana kuna mikono ya baraka iliyoko nyuma ya pazia inayowabariki watu ambao wengine wanaumia na wananchi wanaumia. Lazima tufike mahali na ni mambo haya haya yanayofanya yaulizwe maswali mengi humu ndani. Kwa kawaida maswali hayapati majibu, hata Msikitini Mheshimiwa Spika, hakuna Msahafu mpya unaoletwa, ni juu ya mambo yale yale! Kanisani ni Biblia ile ile! Lakini kila siku yanaulizwa kwa sababu hayajapata majibu. Sasa lazima tuulize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda nije kidogo katika masuala ya askari. Tunasema mengi kuhusu Serikali kwa sababu Waziri Mkuu au Ofisi yake ndiyo ambayo ndiyo kinara katika Serikali nzima.

Mheshimiwa mimi nafikiri wakati umefika wa kuiangalia kasma ya Mambo ya Ndani. Wizara ya Mambo ya Ndani Kasma yake iangaliwe ili yale madai ya msingi ya askari yaweze kupatikana. Askari wengi wanalalamika na wanalalamika kwa hoja za msingi tu.

Mheshimiwa Spika, ikiwa mwanafunzi unamlipa posho ya chakula ya Sh.5,000 kwa siku. Askari Polisi ambaye ndiye anayefanya kazi *twenty four hours* unamlipa kiwango cha Sh. 2,500/= haki iko wapi? Lazima atalalamika! Tuangalie sisi Waheshimiwa Wabunge hapa, jalia unakwenda kwenye mkahawa wa kawaida tu hapo mjini, ile kuanzia asubuhi mpaka usiku Sh.10,000/= haitakutosha. Sasa unamtegemea kuwa askari umlipe Sh.2,500/= kwa siku ale yeye na watoto wake labda watano! Haiwezekani! Lazima kasma ya Wizara hii iangaliwe na iangaliwe ili waweze kupata nyongeza itakayowasaidia kulipa sio tu posho ya chakula, lakini malimbikizo ya madeni na mambo mengine. Nami naamini namwelewa sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mtu ambaye ni *very considerate* ni mtu ambaye anaangalia maslahi ya watu. Ataweza kusaidia kwa hili na tunangemwomba asaidie. *(Makofi)*

Karibuni lilizungumzwa na askari fulani hivi , wakalalamika wanasema kuna askari fulani walikuwa wanatumika kuanzia mwaka 1996 mpaka kipindi hiki kufanya *escort* kwenye matreni haya. Wana madeni yasiyopungua shilingi milioni 500 hawajalipwa. Sasa sijui kama hili linakwenda Mambo ya Ndani, lakini pengine linakwenda kwenye Shirika la Reli.

Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba ufuatilie ili hili nalo lipungue au walipwe kabisa. Mwisho, niseme tu kwamba pale kwetu Kaskazini askari hasa wa Wete pale wamewekewa mita hizi kule kwetu wanaziita Tukuza. Hapa tunaita LUKU. Zile hazina muhali. Ukiisha umeme inabidi ununue. Askari hawa umeme kwetu haupatikani. Lakini LUKU ndiyo inasema ulipe. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu mambo yote haya ni vizuri awaambie Wasaidizi wake wayaangalie ili mustakabali wa askari wetu na wa wananchi wetu uweze kupatikana. Watu wakipata matakwa yao, wakipata maslahi yao ugomvi haupo.

La mwisho, tarehe 30 Desemba, 2005 Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Jakaya Mrisho Kikwete alikuja Bungeni akazungumza wazi kabisa mgogoro wa Zanzibar. Inaonekana anapata matatizo. Sasa mimi ningeomba, basi Mheshimiwa Waziri Mkuu amwambie Mheshimiwa Rais wetu kama kote huko anakwazwa, aje Bungeni na sisi Wabunge kwa pamoja tumsaidie njia ya kutatua jambo hili ili liishe, na heshima ya Rais wetu iweze kuwepo isiweze kuchezewa. Alilolisema humu ni zito. Yeye ni sehemu ya Bunge hili. Ana wasiwasi wa nini? Aje na sote tushirikiane kumsaidia hili jambo liishe. Wananchi wakaye wangalie mambo mengine. Tutasema jambo hilo hilo miaka mingapi?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Khalifa. Waheshimiwa Wabunge, pamoja na yote hayo, wachangiaji bado ni 85. Kwa hiyo, wale ambao wameleta majina yao leo wala sikuyafikiria, wanisamehe maana yake nitakuwa nawapa matumaini hewa na mambo hewa siyo mazuri. Jioni saa 11.00 nawataja watano wa kwanza. Tutaanza na Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Shaaban Kwaangw’, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Amour Arfi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ania Said Chaurembo na James Philipo Musalika. Hao ndio watano, tunaomba wawahi

ili tuweze kuanza vizuri. Baada ya kusema hayo, kwa sababu muda umekaribia kabisa wa kusitisha shughuli za Bunge kwa mchana huu, basi nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni, Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai)Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa 12. Kikao cha 10 leo jioni mzungumzaji wetu wa kwanza kama alivyotajwa na Mheshimiwa Spika asubuhi, atakuwa ni Mheshimiwa Kabuzi Faustin Rwilomba na atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Shaaban Kwaangw'. Sasa namwita Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kwanza jioni hii ili niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyeweza kunifikisha leo na kunipa nguvu niweze kutoa maoni yangu kwa niaba ya wananchi wangu wa Busanda, Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kumpongeza Mheshimiwa Pinda kwa nafasi aliyoipata. Ninaamini kabisa ni uadilifu wake pamoja na jicho la Mwenyezi Mungu, kumwelekeza Rais, awe Waziri Mkuu. Nampongeza sana. Nami binafsi ninaahidi kwamba nitampa ushirikiano wa kutosha. Mamlaka hayo yametoka kwa Mungu, Warumi XIII inasema:

"Mamlaka yanatoka kwa Mungu." Tuna imani naye sana na ndio maana hata hotuba yake, tangu nimekuwa nikisikiliza, safari hii, sina maneno mengi sana. Huwa ninaanza na ugomvi wa kulalamikia kasungura, lakini naona alivyokagawagawa kwa kweli kanakwenda vizuri. Safari hii sina malalamiko makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze vilevile dada yangu Selina Kombani, hekima yake, uadilifu wake, anavyojibu maswali, uangalifu na wema, anavyojali watu wake na anavyotujali sisi Wabunge pamoja na wananchi wetu, kwa kweli nampa hongera. Ninadhani Mheshimiwa Rais, hakukosea kumtoa pale alipo na kumpandisha na bahati nzuri walikuwa ofisi moja. Nadhani ulezi wa Mheshimiwa Pinda ulikuwa unafaa. Nampongeza pia Mheshimiwa Mwanri, tulikuwanaye huku kwenye benchi, lakini nadhani anaanza kudhihirisha u-*DC* wake, alicheweshwa nadhani, alifaa apewe Ukuu wa Mkoa. Kwa kweli anafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna Mtendaji Mkuu, ambaye kwa kweli kwa jina lake ndio linamuathiri anafanya kazi sana. Katibu Mkuu, Mama Tarishi, kwa kweli huyu mama huwa halazi kazi, anafanya kazi nzuri na mimi katika Makatibu Wakuu, ukienda yeye anakupokea na anajaribu kushughulikia. Sijawahi kuacha faili nikaenda jioni nikakuta amelilaza, kwa kweli huyu mama Mungu amsaidie azidi kuendelea na yeye

mumuangalie ni mwenzenu, nafikiri ndiye amewafikisha pale mulipo kwasababu anafanya kazi vizuri. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema bajeti hii sina kelele nyingi sana kwasababu kasungura kalivyoanza kugawanywa, kila mmoja wakati huu wa bajeti watu wake wanamsubiri kwamba atakwenda na nini.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 13 ameanza vizuri na Rais alikwenda kule kwetu kukubali kutengeneza barabara ya kutoka Geita kwenda Usagara. Natoa ahsante kwa niaba ya wananchi wa Geita, ni mkombozi kwetu na ile *ferry*, tunashukuru sana na ameitaja, nashukuru sana. Amefanya kazi nzuri sana, tunashukuru sana. Halafu kuonesha kwamba ninyi sio wachoyo, mmewajali sana Madiwani. Kwa kweli ni kitu kizuri wanatusaidia, wanafanya kazi, ni watu ambao kwa kweli wamekuwa wanyonge muda mrefu sana, lakini safari hii amejaribu kuangalia.

Ila naomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuleta ile sheria na ningeomba kabla ya Bunge hili, ikiwezekana ule Muswada uje basi wapate hii. Ninaomba uwe wazi maana inaonekana amesema pikipiki, afya na nini, sasa na posho ni kiasi gani? Ni vizuri awe wazi tuweze kufahamu na wenyewe wajisikie vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa naangalia tusije tukalisha pua tu tukasahau mdomo. Wenzangu wameshawataja, kuna Wenyeviti wa Vijiji na wa Serikali za Mitaa pamoja na Wenyeviti wa Vitongoji. Hawa watu wanafanya kazi kubwa sana. Ndio wanaotusaidia sisi kwa kweli kufanya kazi na ndio wanaoisaidia Serikali. Huwezi ukafanya mkutano wowote au ukafanikisha kitu chochote kule bila hawa watu kushirikishwa.

Nadhani kuna haja ya kuwafikiria mapema iwezekanavyo kuwaongezea hata posho angalau apeleke kipande kidogo cha nyama kwa mke wake amwonyeshe. Kwa sababu akitokea jambazi anapelekwa kwa Mtendaji wa Kijiji au kwa Mwenyekiti wa Kijiji au kwa Mwenyekiti wa Kitongoji. Ukitokea ugomvi wa familia ni kiongozi wa Kitongoji. Sasa mimi nilikuwa naomba tuwafikirie. Najua watasema, lakini jamani kasungura ni kadogo, mimi bado naamini kwamba sio kadogo, tunaweza tukafanya jitihada tukazipata fedha hizi.

Tukiimarisha bandari yetu, fedha inapatikana, tukirekebisha hizi sheria za madini tukaweka vizuri, fedha inapatikana. Tukipunguza hizi *road blocks* ambazo zinazuwia watu kwenda kufanya biashara zao, fedha zinapatikana. *TRA* wakiwa waaminifu kiasi cha kutosha, fedha hizi zinapatikana, halafu na hawa wote ambao tunawapa fedha kuwapelekea, tumeona kitabu cha *CAG* kinatushitaki. Hakuna ambapo watendaji wamekuwa waaminifu kuanzia Mkoa mpaka Halmashauri. Sasa fedha hizi zikiangaliwa zikafanya tulilolikusudia, hawa watu tunaweza tukawalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, alivyokuwa mwema aendelee kuwa hivyo hivyo. Wanasema ukiwa mroho usiwe mchoyo. Kula uliwe, wape wenzako, kuna hapa na wale pale, ndio tunasaidiana hivyo na Mungu

anakupa neema. Methali inasema, usipotoa sadaka wewe hupati. Ukishangaa, unazidi kuhangaika, maana yake wewe hutoi sadaka Kanisani, sasa hii ndio sadaka unawapa. Kwa Kisukuma wanasema “masamvwa ule king’a”, unawapa wenzako na wenyewe wafurahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri, bajeti nzuri lakini kuna maeneo ambayo nilikuwa napenda anifafanulie kidogo. Amezungumzia suala la maji kwenye bajeti yake, amezungumzia vizuri tu nia njema ya Serikali na nini. Lakini bajeti ya maji imepunguzwa kulingana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Bajeti ya maji imepunguzwa na nilipoambiwa imepunguzwa, mimi nilishtuka sana nikasisimka! Kwa nini imepunguzwa? Nikadhani tungeendelea! Imepunguzwa na imepunguzwa kwa sababu mradi wa Shinyanga umekwisha. Je, matatizo yamekwisha? Nikafikiri labda hawaelewi kwamba kuna sehemu nyingi zina matatizo. Shinyanga kule kuna matatizo na kweli wana tatizo kubwa, lakini Geita na penyewe kuna matatizo makubwa zaidi na Dodoma kuna matatizo. Nitatoa mfano wa Geita, kwa kuwa natoka kule na wamenituma.

Tuliwahi kuelezwa Geita, maji ya Geita ya visima sio salama, kuna madini chini. Mheshimiwa Lowassa, akiwa Waziri wa Maji, alieleza kwamba maji ya Mkoa wa Mwanza hususan Geita sio salama kwasababu chini yana madini ambayo yanaathiri binadamu na wanyama. Bahati mbaya tena maji ya mito na mabwawa yamejaa *mercury*, bahati mbaya tena maji ya mvua wakati mvua ikinyesha maji yale huwezi kuyatumia kwasababu ya *polution* ya migodi pale, ukitega yale maji yanakuja na tope wakati mwingine unakuwa kama unajipaka oil chafu *(grease).*

Sasa Mheshimiwa, wanaposema Shinyanga, Geita haina maji ilikuwa imeweka kwenye *MC Challenge*. Sasahivi hakuna maji! Wanashangaa, kweli wanasikitika wanapoona maji yanaingia mgodini pale. Kwa kweli, napenda Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili suala la maji liangaliwe Geita yote.

Kuna miradi Geita imekaa, kuna mradi wa Nyang’wale umekaa miaka mingi, kuna mradi wa Chankolongo – Nyakagomba, ni mradi mkubwa, tunasikitika sana tunapokwenda sehemu nyingine tunakuta mradi mpya unaanza wakati mradi wa Nyakagomba – Chankolongo kwenda Katoro, haujafanyiwa kazi.

Mwaka 1976 mradi huo umejengwa. *Seventy six!* Labda niseme kwa kizungu nitaeleweka. Mpaka mwaka 1976 mradi huu umeanza, kuna matenki, kuna mabomba yalishawekwa chini. Amekwenda Mheshimiwa Diallo, Mheshimiwa Mwangunga, alifika kule na Mawaziri wameshafika kule wameliona, wanatuambia *quick wings.* Sasa hizi *quick wings* zinakuwa *slow wings. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi nashindwa niwaeleze nini! Au labda mna njama ya kunifukuza mimi? Basi, haya ninyi endeleeni kuwa Wabunge, mimi

wananchi wangu wawe hivyohivyo. Mheshimiwa, sijui mnataka nilie hapa? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukatisha Shinyanga kuna tatizo, Geita ni kilometa 20, tulinyamaza kwa sababu ya tatizo la Shinyanga, lakini kutoa maji Mwanza kupeleka Shinyanga hatusemi vibaya, lakini mimi kilometa 20 kwenda pale ni tatizo? Tunaomba maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri Mkuu, ulisema vizuri suala la nishati ya umeme, ukurasa wa 33 na 34, ukataja Mikoa yote ambayo iko kwenye *MC Challenge*, ukanishtua uliposahau Mwanza. Sijui umesahau, sijui ilikuwa ndio hivyo tumefutwa au namna gani! Lakini Waziri wa Nishati na Madini, alituambia akatupa na karatasi na vijiji 44. Nami vijiji vyangu ambavyo vinatakiwa kupata umeme ikiwemo Kamena, Nyakagomba, Nyarugusu, Katolo, Rwamgas, Bukondo, Nungwe, maeneo ya barabara zote eneo hilo, vilitajwa viko kwenye *MC Challenge* na mimi nikashangilia nikawaambia wananchi sasa tumepata na sisi tunaingia kwenye mwanga tunatoka gizani. Kwenye giza wanakaa wachawi, sasa na sisi tutakuwa binadamu.

Sasa Mheshimiwa hakutaja Mwanza, kuna nini? Hebu tuambie? Kwa sababu tukipata umeme, dhahabu itachimbwa kwa urahisi, gharama zitapungua, benki zitapelekwa kule na kule ndio kuna uzalishaji. Mheshimiwa Waziri, nitapenda kufahamu huu Mkoa ulisahaulika kwa bahati mbaya? Au kama ni *typist* basi aambiwe kwa kweli hafai kukaa kwenye ofisi ya Waziri Mkuu kama amesahau kitu kama hiki muhimu sana. Kwa kweli, kama ni *typist* au ni Katibu, una hasara, kwa kweli ni tatizo! *(Makofi).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa vizuri sana suala la utawala. Umelizungumza vizuri na umezungumzia katika nguvu zako na uwezo mzuri katika hotuba yako. Nikawa nasikiliza ombi ambalo tumelileta muda mrefu. Hapa napenda nizungumze polepole kwa sababu tulikuomba ukiwa *TAMISEMI*, ukawa na lugha nzuri tukawa na matumaini makubwa. Ulipochaguliwa kuwa Waziri Mkuu, mimi kwa kweli niliviringika chini kwamba kwa kweli limefika mahali pake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliomba Mkoa na tulitarajia sasa utasema, hata kama hukututaja, kuna mikoa inatarajiwa kuundwa. Sisi wa Geita tuliomba Mkoa na tuliomba ukatupa maelekezo ukiwa kule kwamba, angalieni Wilaya zinazokaribiana kama zinaweza kuunda Mkoa kwa sababu fedha iliyopo ni kidogo. Tukakaa kwenye Halmashauri, tukakaa kwenye *RCC* tukapendekeza.

Tukapendekeza kama inawezekana Geita, Bukombe, Chato, ambazo ziko karibu, ambazo hazisumbui katika ramani, lakini ambazo zina matatizo yanayofanana. Kwa sababu kutoka Geita kwenda Mwanza, inabidi usafiri upite Wilaya ya Sengerema ambayo tunafikiri na yenyewe ikiwa Geita, itakuwa bora zaidi. Ukija Mwanza uvuke ziwa, ukivuka ziwa unaingia Wilaya ya Misungwi, ukitoka Wilaya ya Misungwi unaingia Mwanza Vijijini. Ukitoka Mwanza Vijijini unaingia Mwanza Mjini, unakwenda kupata huduma. Hata Chato ni hivyo hivyo, anayesafiri aende Muleba, atoke Muleba aingie Bukoba Vijijini, atoke Bukoba Vijijini aingie Bukoba. Bukombe hivyo hivyo, atoke

aende Bukombe aende Shinyanga, Kahama- Shinyanga vijijini, aingie Shinyanga Mjini. Kwa hiyo, ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Geita tunapata tatizo. Pale Busisi na pale Kamanga, kuna makaburi ya watu wa Geita walioshindwa kupata huduma wakienda hospitali, tumezika pale. Ndio maana tunahitaji Mkoa, angalau basi tujikongoje tuombe huduma hata za hospitali. Geita tunapata ujambazi kwa sababu hatuna askari wa kutosha pale. Tunahitaji *RPC*. Geita ni kubwa sana, ina watu karibu 1,000,000 inakaribia Mkoa wa Singida, wanafunzi wa Wilaya ya Geita tu ni sawa sawa na wananchi wa Mkoa wa Lindi, wanafnchi idadi tunakaribiana na nchi ya Zanzibar. Sasa hilo dude lote kubwa kiutawala ni tatizo. Tunaomba Mkoa. Naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushuru sana Mheshimiwa Kabuzi Faustin Rwilomba, kwa mchango wako. Naona Wasukuma hapa wameamua kuchemka hapa. Sasa namwita Mheshimiwa Omar Shaaban Kwaang', atafuatiwa na Mheshimiwa Said Amour Arfi.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Mheshimiwa Kabuzi, ametumia dakika yangu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Babati Mjini, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa waziri Mkuu, kwa kuteuliwa kwake, lakini vile vile niwapongeze Mawaziri, walioko ndani ya Ofisi yake Mheshimiwa Selina Kombani, Mheshimiwa Philip Marmo na Mheshimiwa Agrey Mwanri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameanza hotuba yake kwa maneno ya busara ya mwandishi mmoja Glen Bland. Nataka ninukuu tu ile sentensi ya mwisho amesema hivi, *"Mipango yetu itafanikiwa kama tutatumia fedha zilizotengwa kwa ajili ya kile kilichopangwa."* Mheshimiwa Waziri Mkuu, akamalizia vile vile kwa swali lililoulizwa na mtu mmoja kwamba, bajeti ni nini? Akamalizia kwamba, "*Ni mpangilio mzuri wa kuishi ndani ya uwezo tulionao'*. Kasema, "*Tunaomba tuidhinishiwe fedha hizo ili tuweze kuendeleza yote ambayo tumepanga ndani ya uwezo wetu wa serikali'*. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa maneno haya ya hekima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulipokuwa hapa wakati wa bajeti ya Waziri Mkuu, nilisema sana na ninakumbuka tulifikishana mpaka kwenye vifungu na Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Edward Lowassa, anakumbuka. Tulikuwa tunabishana zaidi juu ya kumalizia jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kuanza kwa Hospitali ya Mkoa.

Sasa leo nataka nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwamba fedha zote ambazo zilihitajika kwa ajili ya kumalizia jengo la Mkoa zilitolewa zote na jengo ni la kisasa na sasa Mkuu wa Mkoa yupo ndani ya jengo hilo. Tunaishukuru sana Serikali na tunamshukuru sana Mheshimiwa Lowassa pamoja na wale waliokuwepo wakati ule. Lakini vilevile niliomba tuanze hospitali ya Mkoa mwaka huu. Sasa naomba nitumie

nafasi hii kusema kwamba kwa kweli Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu. Mmetenga shilingi bilioni mbili kuanza hospitali mpya ya Mkoa wa Manyara, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, sasa naomba nianze na yale mambo ya nyumbani kabisa kule kwenye Jimbo langu. La kwanza, niseme kwamba wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu, kwenye ukurasa wa 27, 28 wananchi wangu walikuwa wanasikiliza alipokuwa anataja barabara kuu na barabara za Mikoa. Sasa wakati amemaliza vile vifungu, wananchi wale wakanitumia meseji hapa, kwamba ni kwanini Waziri Mkuu hakuonyesha kwamba barabara ya Minjingu Babati kwenda Singida itajengwa? Lakini pili, wakauliza kwamba kwa nini haku-*mention* au hakuonyesha barabara ya Dodoma, Babati na Iringa ambayo ni muhimu sana?

Pia walinikumbusha hao hao wapiga kura, maana mpaka jana saa 5:00 usiku wanaendelea kunipigia simu, kwamba Tanzania ndio ambao hatutaki kukamilisha historia nzuri ya kuwa na barabara kuu ya Kaskazini ambayo inaanza Misri kwenda mpaka *Cape Town,* kipande ambacho hakina lami ni kinachotoka Minjingu, Dodoma mpaka Iringa, sasa wakawa wanasema kwanini Waziri Mkuu, hakuitaja barabara hii? Sasa mimi nikawajibu tu kwamba alisema tu baadhi na kwa sababu bajeti ya barabara inakuja basi, lakini nadhani meseji yao imefika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tuna takwimu nyingi hapa, kwa ruksa yako nitakuwa naangalia angalia takwimu hasa za bajeti kwa namna fedha zilivyopangwa, kwenye Mkoa na Halmashauri zetu. Nianze na maombi ambayo kwa kweli tumeyaleta kutoka Jimbo la Babati Mjini ambako kuna Halmashauri ya Mji wa Babati. Halmashauri ya Mji wa Babati hivi karibuni imekabidhiwa hospitali iliyokuwa chini ya mamlaka ya Wilaya ya Babati. Hospitali iliyopo pale mjini Babati, imekabidhiwa rasmi na itaanza kazi kuwa chini ya Halmashauri ya mji Julai hii na kwa mantiki hiyo, hospitali hiyo ndiyo inayobeba matatizo yote ya Mkoa. Vikao vyote vya Mkoa vimefanyika na ninashukuru vilevile Kamati karibu mbili za Bunge, zimepita na zikaona hali ya Hospitali ile.

Tukakubaliana kwamba basi tuiombe Serikali itoe fedha kidogo kwenye yale mafungu ya ukarabati wa hospitali za Mikoa au mafungu kwenye ukarabati wa Hospitali za Wilaya ile hospitali ikarabatiwe kidogo iweze kubeba majukumu ya Mkoa kwa sasa kwa sababu hospitali hiyo ambayo itaanzwa ya Mkoa, kwa vyovyote vile itachukua miaka mingi mpaka ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokiomba kwa kweli ni ukarabati wa ile hospitali, tunahitaji kujenga *ward* kama nne, lakini hatuna chumba cha kuhifadhia maiti ambacho kwa kweli ni chumba muhimu sana, lakini vilevile hatuna *fence.* Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba hicho tu na kwa sababu ngazi zote za Serikali kweli zimeshajadiliana mpaka kwenye *RCC* tulishamaliza hilo, kwa kweli tunaomba tupate fedha za ukarabati kwa ajili ya hospitali hiyo muhimu sana. Idadi ya wananchi kwa kweli imezidi kuongezeka kutokana na Babati kuwa Makao Makuu ya Mkoa. Hilo ni ombi rasmi kabisa ambalo tungependa Serikali ilishughulikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeomba karibu Sh. 1,940,000,000/= kwaajili ya shughuli hiyo tunadhani ingeweza kumaliza ukarabati na uimarishaji wa hospitali hiyo ya Wilaya. Lakini vilevile tuliomba fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa Makao Makuu ya Halmashuri ya Mji. Halmashuri ya Mji haina jengo na kama mnavyofahamu, ina Halmashauri mpya. Tuliomba fedha mwaka jana, vilevile na kama utakavyokumbuka ilibidi Mheshimiwa waziri Mkuu aite viongozi wa Halmashauri ya Mji wa Babati kuja hapa kueleza tatizo lililotokea kwamba mwaka jana hatukupewa fedha. Lakini baadaye tunashukuru Serikali ilitupa fedha na ujenzi sasa umeanza na sasa kwa kweli tunachohitaji ni fungu ambalo litaweza kukamilisha hilo jengo, kwahiyo tunaomba fungu hilo.

Nimeona hapa kuna kiasi kilichotengwa kwenye fungu, nadhani fungu 6402, nitaangalia vizuri baadaye, karibu Sh. 600,000,000/= hivi na kitu. Sina hakika kama ndio fungu lenyewe, lakini nilidhani kwamba ni vizuri fedha hizo, sisi tumeomba karibu shilingi bilioni 1.1 kwa sababu tulishapata karibu Sh. 400,000,000/= na ujenzi utakamilika baada ya kupata. Ujenzi kamili ni shilingi bilioni 1.4. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba hilo kwa sababu Halmashauri yetu ya Mji haina kabisa ofisi na tunatumia jengo ambalo kwa kweli ni la zamani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine ambalo tulilitoa, tuna tatizo la mafuriko katika eneo la mji wa Babati. Kutokana na mafuriko hayo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali alifanya utafiti na baada ya utafiti ikaonekana kuna umuhimu sana wa kuhakikisha kwamba kwa kweli kunajengwa mfereji mkubwa wa kudumu kuhakikisha kwamba ziwa Babati linapungua, kwa sababu kila baada ya miaka fualani ziwa lile linafurika na linaleta maafa makubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba kile Kitengo cha Maafa kikubaliane na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Tuliomba fedha karibu Sh. 251,000,000/= lakini nadhani hazikupatikana.

Sasa kwa kweli gharama zinaongezeka sasa kwa kweli ni karibu Shilingi milioni 600. Kwa hiyo, tunaomba kwa kweli jambo hili ni la kudumu liangaliwe na hasa kwa sababu eneo lile barabara kuu ambayo itajengwa lami itapita eneo hilo. Kwa hiyo, ni muhimu mfereji huo mkubwa ukajengwa kunusuru Mji wenyewe wa Babati pamoja na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ndani ya Halmashauri ya mji wa Babati, tumeona tusiendelee kujenga barabara za changarawe tu kila wakati, hata kwa fedha ndogo ambazo mnatupa, tunataka kujenga mji ambao utakuwa na barabara za lami kwenye mitaa yake. Kazi hii tulishaianza, lazima tuondokane na hii hali ya kuweka vifusi kwenye mitaa yetu. Hatuwezi kwenda mbele kwa mtindo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishaanza kujenga kilometa karibu nne, lakini zile ilikuwa kwa ajili ya uso wa mji wa Mkoa, lakini kilometa moja ilijengwa kuelekea hospitali. Sasa kulikuwa na kilometa nyingine ambayo nina hakika Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe mwenyewe uliona ulipokuja ukiwa Waziri wa *TAMISEMI*, kwenda upande wa Ikulu ndogo kule juu ambapo tulidhani kwamba barabara ingeweza kufika hapo.

Sasa tunahitaji vilevile kujenga kilometa karibu mbili za lami kwenye barabara inayoitwa ya Nyerere. Lakini tukasema tuanze na kilometa moja. Sasa tunaomba fedha hizo za kukamilisha hiyo barabara moja halafu na hiyo nyingine kwa ajili ya kuanza hiyo barabara ya lami kwa ajili ya Mtaa wa Nyerere ili kwa kweli mji wetu uanze kupendeza. Tusingependa kuendelea kutengeneza barabara za udongo ndani ya mji na hasa kwa sababu ni makao mapya ya Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kama tunavyofahamu, Halmashauri ya mji ina vijiji 13. Katika vijiji 13 tuna Zahanati moja tu katika vijiji vyote 13. Sasa katika maombi, vilevile tuliomba tupate angalau fedha kama shilingi milioni 120 ili zisaidiane vilevile na nguvu za wananchi tujenge angalau zahanati nne au sita kwenye vijiji sita ikiwezekana ili ule mpango unaoanza wa Serikali na sisi tuuanze kwenye utaratibu huo. Kwa kweli kwa vijiji 13 kuwa na zahanati moja, kwa kweli utaona kwamba ni jambo ambalo sio zuri sana. Kwa hiyo, tunaomba maombi haya yazingatiwe kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda nao umekimbia, naomba nimalizie tu kwa kusema mambo machache. Moja ni suala la mkulima, ameelemewa sana. Mkulima gharama za kulima heka moja ya mahindi, kwa mfano pale Babati, nimepiga hesabu zimekwenda mpaka 260,000/= akipata mapato ya gunia 15 akiuza tu kwa Sh. 10,000/=, maana yake ndio bei ambayo baada ya kutoa shambani inakuwa hapo, ni kama Sh. 150,000/=. Kwa hiyo, anapata hasara ya Sh. 110,000/= akiuza kwa Sh. 15,000/= bado atapata hasara ya karibu Sh. 35,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima ameelemewa sana, bei ya mazao yake hana maamuzi, mfumuko wa bei umemuumiza sana. Hii itaathiri wigo wa kodi ya Serikali. Kama mkulima hawezi kununua shuka, hawezi kununua kiatu, hawezi kununua mbolea, viatu, vinywaji, Serikali inapata wapi kodi? Kwa hiyo, tuangalie sana suala la mkulima, ameelemewa sana.

Zaidi, mkulima huyu anachangia elimu, anachangia afya, anachangia barabara, anachangia vitu vingi sana. Mkulima ameelemewa sana! Bado vilevile bei ya pembejeo iko juu, kwa hiyo, bado mkulima huyu analo tatizo. Tunasema tumesamehe vifaa kama trekta ama kodi au leseni, tatizo ni vipuri (*spear parts)* zinatozwa *VAT* kubwa sana. Ukienda kununua hata sahani ya jembe au jembe, kifaa chochote, kipuri chochote, kinatozwa *VAT*. Lingekuwa ni jambo la msingi kuondoa ile *VAT* wala sio kusamehe sana kwa kiwango hicho. Kodi hii ni mara moja tu, lakini vipuri atakuwa ananunua kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima ameelemewa sana! Vilevile anahitaji ulinzi wa mali yake na usalama wake. Pale kwenye Jimbo langu nilipata tatizo, wakulima waliathirika sana na dawa ambayo walinunua kutoka Balton ya kunyunyizia kwa ajili ya kuondoa wadudu wa kahawa, lakini walipata hasara, kahawa yao yote iliungua kutokana na dawa hizo ambazo zilinunuliwa kutoka Balton. Wakapata hasara ya Sh. 248,000,000/=. Jambo hili limekwenda kwa muda mwingi sana miaka zaidi ya tisa au kumi sasa, lakini nashukuru suala hili sasa limefika kwa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo,

tunadhani pengine atawaona, angalau wapate huruma, hawa watu wanaathirika na majanga ya ajabu sana lakini hatuwasaidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia tena, mkulima ameelemewa sana, anahitaji kusaidiwa, mipango ya kilimo, miradi hii ya A*SDP*, *DADPs*, *AMSDP* tunaomba ... *(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe ile Kanuni ya 151, msichukue muda mwingi sana katika kupongeza, mtajikuta hamna muda wa kutosha kuchangia hoja. Sasa namwita Mheshimiwa Said Amour Arfi atafuatiwa na Mheshimiwa Ania Said Chaurembo.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo ameiwasilisha yenye matumaini makubwa na hasa pale alipowagusa Madiwani ambao ni Wasaidizi Wakuu katika shughuli zote za maendeleao katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo katika mchango wangu wa maandishi katika Wizara ya Fedha nilikuwa nimehoji kwamba ili kuwajengea uwezo, Wizara ya Fedha ilikuwa inaandaa mafunzo maalum kwa ajili ya Maafisa Tawala, Ma-*DC,* Mameya pamoja na Wenyeviti wa Halmashauri ili waweze kuzisimamia bajeti na hasa fedha katika Halmashauri, nikahoji kwamba hawa wana ukaribu gani na fedha za Halmashauri kuliko Madiwani? Nilikuwa ninapendekeza kwamba katika mpango huo wa kuwajengea uwezo, ni vyema pia wakaangalia suala la kuwashirikisha Madiwani ili waweze kusimamia vizuri fedha za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nilikuwa ninapenda sana leo nijikite katika Jimbo langu la Mpanda Kati, lakini nimeguswa tu na kauli ya Waziri wa Fedha aliyoitoa mapema juu ya kadhia hii ya *EPA,* imeongeza maswali badala ya majibu. Itabidi tena Waziri atuambie, Serikali ni kwa sababu gani ilimwajiri Enesten Yang kukagua fedha za *EPA* wakati fedha zile sio za Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Waziri atuambie pia ni kwa nini na kwa sababu gani Marehemu Balali aliwajibishwa wakati Mheshimiwa Rais anasema kwamba ilitokana na kutokusimamia vizuri fedha za *EPA.* Vinginevyo pia Benki ya Taifa ya Biashara, *NBC* atuambie tu Waziri kwamba ilikuwa ni ya matajiri au ilikuwa ni ya walalahoi, wananchi wa nchi ambao ndio walikuwa wanaimiliki kwa asilimia mia moja na ndio walipewa dhamana ya kuangalia fedha za *EPA*! Nasema hivyo kwa sababu fedha hizo zingeweza kununua jenereta mbili au tatu na kutuondolea kabisa tatizo la umeme Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunalo tatizo kubwa sana la umeme katika Mji wa Mpanda hatuna umeme kabisa wa hakika, mashine ni za muda mrefu, chakavu, hazina vipuri, hazikupata matengenezo kwa mujibu wa taratibu, sasa hivi zimefikia kusimama kabisa na hakuna umeme. Jana tu ndio zimewashwa hizo mashine na bado zinasuasua, eneo fulani lina umeme, eneo lingine halina umeme. Tatizo la kukosa umeme limechangia kupandisha gharama za maisha katika Mji wa Mpanda, pia imesababisha ukosefu na upungufu mkubwa wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kuiomba Serikali, pamoja na jitihada zinazofanywa sasa hivi na *TANESCO*, nilikuwa ninaiomba Serikali iangalie suala la tatizo la umeme Mpanda, wakati Mheshimiwa Rais alipokuwa akipita kuomba ridhaa kutoka kwa Wananchi wa Mkoa wa Rukwa, aliahidi kushughulikia matatizo ya umeme katika Mji wa Mpanda na Nkasi.

Kwa ujumla tatizo la umeme katika Mkoa wa Rukwa ni tatizo kubwa sana. Sumbawanga hawana umeme wa uhakika pamoja na kwamba wanapata umeme kutoka Zambia, Mheshimiwa Paul Kimiti hapa aliwahi kuliambia Bunge hili katika kipindi cha mwaka mmoja umeme ulikatika zaidi ya mara 1,300 na zaidi, Nkasi hawana umeme, Mpanda ndio huo umeme sasa ni matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimefarijika tu na kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba uko mpango wa *North West Grid* ambao tutapata umeme kutokea Geita nafikiri kuteremka Biharamlo, Kibondo, Kasulu, Kigoma, Mpanda na hatimaye Nkasi na Sumbawanga. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu sina matatizo kabisa na mpango huu, lakini ile *time frame* ndio inayonitia mashaka sana, katika mpango kabambe wa kufikisha umeme Nkasi inatarajiwa umeme ufike mwaka 2035, kwa kweli hatuna matumaini ya haraka kwamba Mkoa wa Rukwa utaunganishwa katika Gridi ya Taifa. Nilichokuwa ninajaribu kukitazama ni kwamba ni sawa sawa na yule mtu ambaye unamuuliza nionyeshe sikio lako badala ya kukwambia hili hapa anakwambia hili hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni busara kweli kutoa umeme kutoka Geita kuuleta Sumbawanga badala ya kuutoa Mbeya kuuleta Sumbawanga, Mbeya ni karibu zaidi na Sumbawanga wangeweza kufikisha umeme Sumbawanga, Nkasi na Mpanda kuliko kusubiri umeme utakaotoka Kaskazini, itatuchukua muda mrefu.

Vivyo hivyo kwa sababu umeme wa gridi umeshafika mpaka Urambo, ni rahisi pia kuufikisha Kigoma kuliko kuendelea kusubiri umeme unaotoka Kaskazini. Ninaiomba Serikali iangalie suala la usambazaji huu wa Gridi ya Taifa, Mikoa ya Rukwa na Kigoma na yenyewe ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inahitaji kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia suala la umeme, tunayo matatizo mengine kadhaa, lakini tatizo kubwa ni usafiri kwa maana ya usafiri wa barabara na usafiri wa reli. Ndugu yangu Mheshimiwa Msambya amezungumza hapa asubuhi adha wanazopata wasafiri wa treni wa *central line* kwa maana ya reli ya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana matatizo hayo ya reli ya kati ni kidogo sana, wakati ninaondoka Mpanda nilipofanya mkutano wa kuongea na wananchi wakanituma nije niseme maneno yafuatayo na wakaniambia watasikiliza kama nitasema kama walivyosema wao. Wameniambia kwamba baada ya miaka 46 ya uhuru, Watanzania leo wanasafirishwa katika mabehewa ya ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nikuhakikishie, sikushuhudia mabehewa ya ng'ombe, lakini mimi mwenyewe ambaye nimesafiri katika garimoshi hilo hilo nimewaona Watanzania wakisafirishwa katika mabehewa matupu yanayopelekwa Mpanda kwa ajili ya kwenda kupakia tumbaku. Ndio hali tuliyofikia wananchi wa Mpanda. Tunasafirishwa katika mabehewa ya mizigo.

Tulikuwa tunapata mabehewa matatu ya daraja la tatu, leo tunapelekewa behewa moja au mawili. Yakipelekwa mawili kwa maana ya abiria wa kutoka Mpanda behewa moja na wa kutoka Katumba behewa moja. Abiria wote wanaoanzia baada ya Katumba, Kaboronge, Kambuzi, Ugala na kuendelea mpaka ufike Kaliuwa wanasafiri kwa namna gani? Hakuna barabara! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mkoa wa Rukwa wameipandisha hadhi barabara ya kutoka Mpanda mpaka Ugala kuwa barabara ya Mkoa, mnawasaidiaje hawa watu wa kutoka Ugala mpaka Kaliuwa? Ni vyema sasa na Tabora wakaangalia suala la kuipandisha hadhi barabara ya kutoka Kaliuwa kuja Ugala ili hata reli itakaposimama wananchi hawa wawe na njia mbadala ya usafiri wa kuweza kuwafikisha kupata mahitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe Barabara ya Ipole, Inyonga, Mpanda inayotokea Sikonge, barabara hii haina fedha. Reli imetengewa fedha kidogo. Reli ya Mpanda na Reli ya Shinganya sijui shilingi milioni 100! Barabara haina fedha! Bila kuimarisha barabara ya kutoka Mpanda kwenda Tabora bado hamjawatendea haki wananchi wa Wilaya ya Mpanda. Ni lazima barabara hii iimarishwe.

Napenda kuishukuru sana Serikali katika awamu mbili zilizopita wametenga fedha kipande cha kutoka Ipole mpaka Inyonga kimeimarika, lakini bado sehemu ya kutoka Inyonga mpaka Mpanda inahitaji matengenezo. Nilikuwa naiomba Serikali iangalie suala la kuimarisha barabara ya kutoka Tabora kuja Mpanda. Nimefarijika tu kwamba kuna fedha imetengwa kwa ajili ya barabara ya kutoka Mpanda kwenda Kigoma na Mpanda kwenda Sumbawanga. Ninawashukuru sana na ninaishukuru sana Serikali kwa jitihada inazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado tunayo matatizo mengi katika Mkoa wetu wa Rukwa, pamoja na kwamba ni Mkoa ambao unaongoza katika uzalishaji wa chakula na ina wananchi ambao ni mahodari wa kufanya kazi za kilimo, lakini bado wanahitaji kusaidiwa.

Kuna mpango ambao umebuniwa wa maendeleo ya kilimo na Serikali kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, kuna miradi ambayo imeibuliwa na wananchi wa Mkoa wa Rukwa na hususan Wilaya ya Mpanda katika mabonde ya kule Usevya, Kakese, Ikola - Karema, Kapalamsenga, Kirando kule hata Kalya ni maeneo ambayo yana maji ya uhakika yanahitaji kuendelezwa, miradi imeibuliwa na wananchi, imeshapitishwa katika hatua kadhaa, lakini imekaliwa Wizarani. Tunataka kujua kwa nini fedha haziletwi kwa ajili ya kuanzisha miradi hii ambayo itaongeza uzalishaji wa chakula mara dufu hasa kwenye kilimo cha mpunga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la maji katika Mji wa Mpanda, hatuwezi kusema Mpanda inafanana na Kongwa au Dodoma, tumezungukwa na maji, tuna mito ya kudumu ya uhakika, tuna mabwawa, tuna maji ya mitiririko, lakini ni namna gani tunawafikishia maji yale walaji? Ndio tatizo la Mpanda, Mradi wa Ikolongo.

Ninaiomba Serikali kadri wanavyochelewa kufanya maamuzi ya kuanzisha na kutekeleza mradi huu, ndivyo gharama zinavyoongezeka, lakini kwa sababu mradi haujaanza, tuna tatizo sana la magonjwa ya homa ya matumbo katika Mji wa Mpanda kwa sababu ya maji yasiyokuwa salama. Maji ya bomba na maji ya mtiririko ya Manga sio safi na sio salama, kwa hiyo, tunahitaji kupata visima kuzunguka Mji wa Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo katika Hospitali yetu ya Wilaya, Hospitali haitoshelezi. Tuna *town clinic* pale mijini, mimi nilikuwa naiomba Serikali, ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya Wilaya ya Mpanda, basi ile *town clinic* iwe na maana ya kuwa *town clinic* kwamba kina mama wajawazito na watoto wapate huduma za kulazwa hospitalini, tujengewe wodi katika ile *clinic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la malimbikizo ya mishahara na madai mengine ya watumishi, madai ya walimu, madai ya Askari Polisi, madai ya Wauguzi na Madaktari. Ninaomba Serikali iangalie suala la kuwalipa mafao na madai yao watumishi hawa ili waweze kuwa na *moral* ya kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nilichokuwa ninataka kusema ni kwamba, mimi sijapata kusikia hata siku moja magari ya Serikali, hata magari ya Mawaziri yamesimama kwa sababu ya kukosa mafuta. Pamoja na kwamba fedha zinatengwa kwa ajili ya mafuta ya magari ya Serikali, gharama za mafuta zinaongezeka mara dufu lakini magari yanaendelea.

Fedha zinazotengwa kwa ajili ya chakula cha watoto wa shule mara tu chakula kinapokwisha shule zinafungwa. Inakuwaje magari yatembee, shule zifungwe? Ni lazima tuliangalie suala hili la kuhakikisha kwamba shule zote za bweni wanapata chakula katika kipindi chote cha muhula na isiwe sababu ya kufunga shule ovyo ovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda nipate maelezo kuhusu tukio la kufungwa Shule ya Kantalamba na maafa ya wale watoto waliokuja pale Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii nami nichangie hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa napenda kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kutuletea hotuba hii ambayo imemgusa kila mtu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kutoa pole kwa waathirika wote katika Wilaya ya Ilala na Mkoa wa Dar es Salaam waliopoteza ndugu yao na wale walioumia, Mwenyezi Mungu atawapa afya njema baada ya ghorofa kumi kudondoka katika Mtaa wa Mtendeni na Kisutu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema hivi kwamba matukio haya yaliyojitokeza sasa hivi katika Jiji la Dar es Salaam ni matukio ambayo nina hakika kabisa yatakuwa yanaendelea, kwa sababu gani nasema hivi? Kwa sababu mimi mwenyewe ninakaa Wilaya ya Ilala na saa zote niko mitaani nikiziona hali jinsi gani majumba yanavyojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo nyumba iliyodondoka Mtaa wa Mtendeni ni moja tu ya nyumba ambazo zitaendelea kudondoka, nyingine iko Mtaa wa Uhuru na *keep left* ya ghorofa kumi hivyo hivyo iliingia wapangaji baada ya kupasuka wakaondoka na nyingine iko Mtaa wa Rufiji ya Mchina ambayo kila siku inapasuka, tunaona na taarifa zinafika Serikalini, lakini watendaji wanaohusika hawachukui hatua yeyote na ndio maana ninasema nyumba zitaendelea kudondoka Dar es Salaam bila Serikali kuchukua hatua madhubuti kabisa ya kuzikagua upya nyumba zote zilizojengwa katika Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mambo ya Dar es Salaam, kuna jambo lingine ambalo ni kero kubwa wa wananchi wa maeneo yale ambayo yanajengwa majumba makubwa. Haya majumba makubwa yanayojengwa wanachimba chini ili watengeneze *basement* ya ghorofa na wanaathiri sana zile nyumba ndogo ndogo ambazo ziko jirani na nyumba kubwa ambazo zinajengwa na wananchi wale wakipeleka madai yao kwenye Serikali za Kata au nini wanaambiwa waende Mahakamani.

Kwa hiyo, inaonekana wazi kwamba nyumba ya ghorofa inayojengwa itafika ghorofa kumi wakati inaonekana ni mbovu, kuna harufu ya rushwa ndani yake ambayo inaendelea kati ya mjenzi na watendaji wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema habari ya nyumba hizo, sasa hivi ninaelekea katika majengo. Dar es Salaam sasa hivi imekuwa na majanga mengi ya moto. Kuna janga limetokea Mtaa wa Mahiwa nyumba ya ghorofa ambayo ilikuwa na matairi imeungua moto. Moto ulianza kuwaka tangu saa sita usiku haukuweza kuzimika mpaka saa sita mchana siku ya pili kwa kukosa vifaa na uwezo mdogo wa magari ya Zimamoto katika Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hii, tunaomba kabisa, mimi ninaamini kama Dar es Salaam Waziri Mkuu katuambia kwamba ndio jiji ambalo la biashara linakuwa na

upungufu mkubwa wa vifaa vya Zimamoto siamini kama huko Nyarugusu na Mwanza na Tabora ndugu zangu Wanyamwezi wamepelekewa gari za Zimamoto za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni tatizo na ninaamini ni tatizo la Tanzania nzima, kwa hiyo, ninaomba Ofisi ya Waziri Mkuu iliangalie tatizo hili kwa makini kabisa na vilevile Kitengo cha *Disaster* kiangaliwe kabisa kwa makini na kipatiwe vifaa. Nami ningependa Waziri Mkuu tufanye ziara mimi na yeye anipeleke katika Kitengo cha *Disaster* nikaone vitendea kazi vilivyopo katika kitengo hiki ambacho Watanzania tunakitegemea sana na tumeona majanga mengi, sasa hivi yametukuta bila kupatiwa ufumbuzi wa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam jiji la biashara, ilishatangazwa rasmi hapa leo, Jiji la Dar es Salaam likinyesha mvua dakika kumi tu, ni kosa kubwa. Mfanyabiashara anahitaji muda wa biashara zake, sasa kutoka *PPF Tower* kuja mpaka Bibi Titi Mohamed na Morogoro *Road* siku ya mvua unachukua masaa manne kusota. *(Makofi)*

Mfanyabiashara gani huyu jamani tusipomwangalia na wakati wake wa kazi zake, tunashindwa kutengeneza *drainages* hizi za kupeleka baharini? Nimekuwa nikirudia mara kwa mara kuhusu mifereji hii ya maji taka. Bahari iko pua na mdomo, mfano hai, *United Nations*, Shule ya Muhimbili pakinyesha mvua pale inakuwa mpaka mtu upite kwa boti labda na bahari iko *Salander Bridge* pale. Haya ni mambo ya aibu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimefarijika na hotuba hii ya Waziri Mkuu, amesema kwanza Dar es Salaam imepewa kipaumbele, safari hii na Waziri Mkuu alikubaliana kabisa na Madiwani wa Mkoa wa Dar es Salaam kwamba Dar es Salaam ina matatizo ya miundombinu, ina matatizo ya uchafu, ina matatizo ya *system* ya maji na ina matatizo mbalimbali na ameahidi kwamba ataitekeleza. Ninampongeza Waziri Mkuu kwa kuipa Dar es Salaam kipaumbele. Ahsante sana Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia mambo haya nakwenda moja kwa moja katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 69, 70, naomba kunukuu, amesema kwamba, *"Serikali imefanya uamuzi wa kupanua na kuimarisha uchaguzi huu."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, ukurasa wa 69 amesema kwamba *"Shughuli kubwa zitakazofanyika katika maandalizi haya ni pamoja na kuhakiki mipaka ya vitongoji, vijiji na mitaa, kufanya mapitio ya Kanuni za Uchaguzi na kufanya mikutano ya Halmashauri na Vyama vya Siasa. Aidha, shughuli nyingine zitafanyika ni kukusanya maoni ya wadau mbalimbali kuhusu mapendekezo ya kutumia daftari na namna nzima ya uchaguzi wa Serikali ya Mtaa"*, ninaishia hapo ili muda usiende sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukwambia kwamba hivi sasa Waziri Mkuu kashapanga mipango ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa za mwaka 2009, keshaipanga kabisa, katuletea hapa, lakini bado mpaka leo kuna watendaji kuanzia Mikoa wa Serikali mpaka Wilaya, Halmashauri, Kata mpaka kwenye Serikali zenyewe za Mitaa bado kuna

unyanyasaji mkubwa wa wananchi ambao wamechaguliwa na wananchi. Napenda kutoa mifano michache tu mbele yako kisha nielezee matatizo yanayojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Dakawa Kata ya Dakila Morogoro Vijijini kuteuliwa kwa mwanachama ambaye hausiki na chama kuziba nafasi ya wazi katika kijiji hicho baada ya kumjulisha Mkurugenzi wa Halmashauri kutangaza ili uchaguzi ufanyike kisheria, mtu anaamua kumchukua mtu na kumweka pale kuchukua nafasi ile. Sheria hii hakuna wala Kanuni hii hakuna katika Katiba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Kijiji cha Mbeya Itini Kata ya Ihanga, Mbeya Vijijini vilevile Mshindi shughuli zilifanyika, kura zimeonekana zina matatizo zimezidi, lakini msimamizi anaamua kumweka mtu ambaye anataka yeye anamtangaze. Hapo hakuna demokrasia ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Hali hii vilevile iko katika Jiji la Ukerewe Kijiji cha Ihindo Wilaya ya Kongwa. Mwenyekiti wa Kijiji ambaye ameshinda ametangazwa siku saba na baada ya siku saba anakuja anaenguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niambie uchaguzi huo wa Serikali za Mitaa Waziri Mkuu safari hii lazima auanzie sasa hivi kuuchunguza na kuangalia watendaji ambao ni wabadhirifu na wanaokereketwa wa chama fulani katika chama fulani, hatuwezi kufanya kazi kwa njia hiyo. Matatizo haya yanajitokeza kiasi kwamba mpaka mtu anaamua kabisa kuchukua madaraka mkononi mwake kuwatia watu ndani, kuwa-*harass* watu na nini. Tunaomba tabia hii ikomeshwe na Waziri Mkuu. Tunaomba uisimamie sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno haya, naomba kidogo nizungumze kuhusu elimu, mchango wa watu wanaoambiwa walipe katika kujenga madarasa ya sekondari katika Kijiji cha Kasingiri Kata ya Ilala, Shinyanga Vijijini Jimbo la Solwa, wananchi wanachanga kwa hiari yao, kwa mapenzi yao kuchanga siyo lazima, ni hiari. Tuna haki kama Watanzania kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Lakini jambo la ajabu ni kwamba mtu analazimishwa kuchanga Sh. 25,000/= kijiji hicho nyumba hadi nyumba sungusungu wamepita kuangalia watu ambao hawajachanga Sh. 25,000/= na matokeo yake mzee mmoja ambaye anaitwa Shimo, yeye alikuwa hayumo ndani ya nyumba yake wakamkuta mkewe ana mimba ya miezi tisa wakamchukua yule mama, mama anawaambia hali yangu siyo nzuri mchukueni binti yangu mumpeleke, wanamwambia tutakuchukua wewe. Wakampeleka wakamtia *lockup* na ndani ya *lockup* yule mama kulikuwa kuna wanawake wawili na mwanaume mmoja akashikwa na uchungu, wanawake walipiga kelele, lakini hakuna mtu aliyethubutu kuja kufungua mlango. Akajifungua mtoto ndani ya sero hiyo mbele ya mwanaume. Huu ni udhalilishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba hii ni utovu wa haki za binadamu, asubuhi yake mama akazimia wanakuja wanafungua sero wanamchukua yule mama kumpeleka katika zahanati kupata huduma ya kwanza. Sungusungu hawa wakiongozwa

na Katibu Kata, hii sio haki kabisa wanayotendewa wananchi katika kuchangishwa kodi za kujenga madarasa na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kusikitisha mumewe akaenda akatafuta Sh.21,000/= kwenda kumnusuru mke wake wakazikataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonekana wazi ni kwamba hii ni chuki tena chuki za kisiasa. Kwa hiyo, tunaomba Waziri Mkuu aangalie matatizo haya! Huyu mama, Mheshimiwa Waziri Mkuu nakuomba hili jambo lifuatiliziwe katika Kijiji hicho, nimeshakitaja, Kata ya Ilala na Jimbo la Solwa, Shinyanga Vijijini.

Kwa hiyo, hii inasikitisha sana na hata pale wananchi walipokuja juu, bado Katibu Kata anaitisha Mkutano wa wananchi na kuwaeleza kwamba hili ni jambo la kawaida. Huu ni utovu wa nidhamu na ni utovu wa adabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nasema ahsante sana kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Lakini pamoja na ushauri wake mzuri kwamba tunapoteza muda mwingi kutoa pongezi, tunalazimika kufanya hivyo kwa sababu mimi binafsi siwezi kujisikia vizuri bila kumpongeza Waziri Mkuu kwa upole wake, unyenyekevu wake, uchapaji kazi wake na umakini wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima kwa kweli nimpongeze, niwapongeze Mawaziri katika ofisi hiyo, Mheshimiwa Kombani pamoja na Mheshimiwa Mwanri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siwezi kumwacha Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Mama Maimuna Tarisi, mama huyu mbali na uchapakazi na lakini naye ni mnyenyekevu anamsikiliza kila mtu na anachukua hatua na ni kila siku miaka yote.

Kwa hiyo, ninapenda nimpongeze sana na katika utendaji tunawapa moyo waendelee kufanya kazi wananchi wafurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na mimi nimefurashishwa sana kwa kuanza kuwafikiria Madiwani sasa. Ningependa hapa niseme kwamba, mafao au maslahi ya Madiwani, yangeendelea kuangaliwa kila wakati na hususan mafao ya mwisho, wanapomaliza kipindi chao cha miaka mitano; kwa sababu Madiwani katika kipindi chao cha kazi wengine hata shughuli zao huwa zinalala iwe za

kilimo au biashara. Kwa hiyo, wanapoacha Udiwani wengi wanaadhirika baada ya muda mfupi sana. Kwa hiyo ni vizuri mafao yao yakaangaliwa upya, kwa sababu huyu mtu amefanya kazi kwa miaka mitano ni vizuri sasa naye apate posho au mafao ambayo yatamuwezesha kimaisha kabla hajarudia hali yake ya nyuma, ambayo aliicha kwa miaka mitano. Mafao hayo yatamsaidia namna ya kuanza maisha upya, baada ya kupoteza Kata, kujiuzulu au vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Madiwani wanasaidiwa sana na Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji. Wenzangu wameshasema, hawa ndiyo Serikali za Mitaa, kwa sababu ndiyo mtandao wenyewe; sasa wafikiriwe hata kama ni kuanzia kidogokidogo ni vizuri wakafikiriwa wakapata kila mwezi chochote kile kitakachowasaidia. Serikali inaweza ikaweka nia, nadhani ina uwezo wa kulifanya hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazidi kutoa shukrani zangu kwa Serikali, baada ya kuamua kujenga kiwango cha lami, barabara yetu ya kutoka Geita kwenda Usagara. Hapa nataka nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Rais; alikuja kuizindua barabara hii tarehe 12 Mei, 2008. Katika uzinduzi wake, kila sehemu aliyosimama kusema au kusalimia wananchi, alitusemea vizuri sana Wabunge wa Geita, Sengerema na Misungwi kwamba, hapa ndani ya Bunge tumeipigia kelele barabara hiyo na Serikali imekubali ikajipanga na leo barabara inajengwa. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais; si wote ambao watapata nafasi ya kusemewa vizuri na kiongozi mkubwa kama huyu wa nchi. Kwa hiyo, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara hii, kwanza, napenda kumwomba na nimpongeze Meneja wa *TANROAD* Mkoa wa Mwanza, anavyoshughulikia barabara sasa hivi na nashukuru kwa barabara yangu ya Busisi kwenda Nyangorongo, ambayo nimekuwa nikiisemea kila wakati sasa hivi inapitika. Kabla sijaja hapa, kulikuwa na kipande kimebakia cha kutoka Kayenze kwenda Bukwimba, ambacho niliacha tayari kuna mitambo. Juzi niliwasiliana na *TANROAD* Mkoa wakasema, Mkandarasi alikuwa hana fedha na ameshalipwa fedha za mafuta, bila shaka atakuwa *site;* kama yupo huko naomba sasa aende haraka sana, kwa sababu pesa zipo kipande hicho cha barabara kiweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna maombi ambayo vikao vyetu vya *RCC*, yaani Vikao vya Ushauri vya Mkoa, viliomba kupitisha maombi ya kuipandisha hadhi barabara ya kutoka Sengerema hadi Ngoma, ambayo sasa hivi ipo chini ya Halmashauri na kipande cha barabara kutoka Nyangorongo kwenda Segese Wilayani Kahama. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumeweka barabara ambayo itaunganisha Miji ya Biashara ya Kahama, Segese, Karumwa, Busora, Ngoma hadi Sengerema. Barabara hii ni muhimu sana, kuna magari mengi sana ya biashara yanapita huko. Kwa hiyo, tulikuwa tunadhani Waziri muhusika, alisikie hili na aipandishe kwa Sheria ambayo tumempa na ambayo tayari tumeshaiweka kwamba, yeye anaweza kupandisha hadhi kutoka Halmashauri kwenda *TANROADS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitakuwa sijasema chochote leo, kama sitazungumzia tatizo la maji la Mji wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Geita ipo kwenye sura za Milima ya Geita, kwa juu kuna shughuli za madini yaani kuna migodi; kuna mgodi mkubwa wa *GGM*, lakini bado kuna wachimbaji wadogowadogo. Sasa shughuli zote hizi zinatumia kemikali na hususan *mercury*. *Mercury* inaaminika kuwa ina kawaida ya kuzama chini, kwa hiyo, inaingia kwenye *water table.* Mji wa Geita wanakunywa maji ya visima vifupi, yaani vingi vifupi. Kwa hiyo, kemikali hii inapoingia kwenye maji, yaani kwenye *water table*, yanakwenda kwenye visima hivi ambavyo watu wanakunywa maji.

Zebaki hii inasemekana inasababisha Ugonjwa wa Kansa; sasa sijui ni kansa ipi; ya titi, ubongo au mifupa? Kama itakuwa ni kansa ya ubongo, kwa hiyo, unategemea baada ya muda fulani wananchi wote wa Geita watakuwa taahira. Mkuu wa Wilaya taahira, *OCD* taahira, Wabunge taahira, kwa sababu wanakunywa kemikali. Maaskofu, Wachungaji na Mashehe taahira, yaani watu 200,000 taahira.

Sisi Wabunge tunashindwa kusema; sijui tuiambie nini Serikali? Waziri Mkuu aliyepita ni shahidi, ukienda Geita kitu cha kwanza wanakwambia suala la maji na sasa imefikia mahali hawasemi wanazomea. Mawaziri wanazomewa tena mbele ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Lowassa yupo hapa ni shahidi. Sisi Wabunge pia tunazomewa. Wanaona kuzomea ndiyo njia ya kufikisha ujumbe Serikalini. Tumeshasema sana juu ya maji ya Geita. Nilikuwa nauliza wenzangu; Mheshimiwa Kabuzi na Mabina, labda na sisi tuizomee Serikali kwa sababu na sisi tunazomewa kule! Tujipange hapa siku moja tumzomee Waziri Mkuu na Waziri wa Maji; bado hatujakubaliana hili. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali itusaidie kwani hivi sasa Geita ndoo ya maji ni shilingi 200, maji yenyewe ni machafu; yenye zebaki, yenye wadudu wa *typhoid* na *amoeba*. Geita ukienda maabara kupima, huwa hawakuulizi, anakuandikia tu yule anayepima kwamba, kwa sababu maji yote ndivyo yalivyo. Kwa hiyo, kuna *typhoid;* maji yenyewe ni aghali; na yapo kilomita 28 tu kutoka Ziwa Viktoria.

Tuliishukuru Serikali ilipotangaza kuwa Geita itapata maji kutoka kwenye Mradi wa *Millennium Change Cooperation.* Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyepita, walitangaza hivyo, baadaye hawa mabwana wakubwa wakaiondoa Geita haimo. Ninapochangia hapa wenzangu wananiangalia sana, labda tayari nina kansa ya ubongo kwa kuwa ninasema sema hivi. Tunaomba Serikali itueleze, tuombe vipi ili Geita tupewe maji?

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu hujaenda Geita, naomba kabla hujapanga safari ya kwenda Geita hilo suala la maji ni vizuri kwanza ukaacha yakaenda. Mimi sipendi Waziri Mkuu kama wewe; sisi Wabunge tuzomewe mbele yako au wewe uzomewe, pengine wale watu ni taahira kwani hawaogopi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Jimbo la Nyang'hwale lina ukame kwa sababu linapakana na Shinyanga Vijijini. Vilevile ipo miradi ya zamani kama ule wa Nyakagomba, Mradi wa Nyamtukuza kupitia Vijiji vya Kakora, Nyarubere, Ikangara, Karuma, Kayenze mpaka Bukwimba wa miaka ya 76, ulikuwa umepangiwa pesa kwenye

Mradi wa *Quick Wins* mwaka huu, lakini baadaye uliondolewa. Mradi huo ulikuwa umepangiwa shilingi milioni 60; Wananchi, Madiwani na mimi Mbunge, tulienda kuwaambia wananchi wakafurahi sana, lakini baadaye Mradi huu ukaondolewa kwenye hiyo Programu.

Niliongea na Uongozi wa Halmashauri wakaniambia kwamba, umemekwa kwenye Mpango mwingine wa *Rural Water Supply Sanitation Program*, ambao mwezi wa saba utaanza kwa utafiti, wanaita upembuzi yakinifu na baadaye uendelee chini ya *World Bank.* Ninaomba sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu ufanye kila njia, utusaidie Geita tupate maji. Watu wa Jimboni kwangu wananunua maji, ndoo ni shilingi 200 pale Msalala na Karumwa, wananchi hawana fedha hizo.

Naishukuru Halmashauri, Mradi wa Nyang'hwale umekarabatiwa; kulikuwa na tatizo la pampu sasa hivi nadhani litakuwa limeshughulikiwa na ninaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichangie kuhusu hili suala la Sekondari zetu hizi za Kata. Najua Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameshasema huko nyuma kwamba, utaratibu unaotumika siyo mzuri kwamba, shule huwa zinafunguliwa mwezi wa kwanza, kwa hiyo, inahitajika wananchi wachangie kati ya mwezi Novemba, Desemba na Januari. Wananchi wanapelekeshwa vibaya sana kuchangia fedha hii, kwa maelekezo ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ili wanafunzi wote waliochaguliwa kuingia *form one* wasiachwe, kitu ambacho ni kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu hapa ni kwamba, kipindi hicho mkulima wa kawaida kwanza, anakuwa hana akiba ya hela; kwa hiyo, akiuza mazao yake anaishiwa, lakini pia ndiyo wakati ambapo anakuwa hana akiba ya chakula. Vilevile wakati anatakiwa aandae *uniform* ya mtoto na ada, ndiyo wakati ambao anashughulikia kilimo. Sasa unapompelekea achangie sekondari wakati huo, tena kwa kutumia mgambo; hata wanyama wana Sheria zao kwamba, Serengeti wanyama mwezi wa kwanza mpaka wa sita nadhani hawaruhusiwi kuwindwa, kwa sababu ni kipindi cha kuzaliana, hata samaki kuna wakati huwezi kuvua.

Sasa wakulima hawa, waacheni kipindi hicho washughulike na masuala ya kilimo, wajikimu maisha yao, wanunue chakula; michango hii ifanyike mwezi Juni, Julai, Agosti, Septemba na Oktoba, kwa awamu. Mheshimiwa Waziri Mkuu umeshalisema hili, lakini kuna Kata ambazo bado zinafanya hivyo. Ninaomba wakati ukifanya majumuisho ya hotuba yako, hilo ulitolee maelekezo na bahati nzuri Wakuu wa Mikoa wapo hapa wanasikia na wananchi wanaona. Kero tulizozifuta za kodi ya maendeleo na ushuru wa mifugo ni kana kwamba sasa zipo tena kwa sura hiyo ambayo siyo nzuri na mfano nimeutoa sasa hivi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda unakwenda lakini nisemee kuhusu umeme. Katika Kijiji cha Karumwa ni kero ya siku nyingi mpaka wananchi waliji-*organise* siku moja, wakafanya maandamano yao namna ya kuikumbusha Serikali. Karumwa pale umeme ni wa kuteremsha, tayari upo unaopita kwenda Nyamtukuza, Vijiji vya Busorwa,

Nyarubere, Shabaka, Karumwa; naomba sana safari hii na Kata zote za Nyang'hwale wapate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la pesa za wajasiriamali, mara mbili hapa Serikali hii kwenye Bunge lako nimekuwa nikiahidiwa kwamba, Nyang'hwale haikuwamo kwenye awamu ya kwanza ya Geita; kwa hiyo, kuna fungu maalum limetengwa kwa ajili ya wananchi hao. Tumesubiri wakati wa kilimo hatukuona pesa hiyo, sasa ni mwezi Juni pesa hiyo haipo na Serikali hapa mara mbili inasema pesa hizo zipo zitakuja Nyang'hwale. Wananchi wanasubiri, wananipigia simu. Kuanzia sasa wakinipigia simu nataka niwape namba ya Waziri Mkuu wampigie yeye, kwa sababu wamesikiliza ahadi za Serikali lakini hawaoni na wakinipigia mimi sina majibu; sasa nifanye nini? Naomba huo mgao ulioahidi Nyang'hwale wananchi wanasubiri, upelekwe haraka.

Niongelee suala la Wilaya na wenzangu wameshalizungumzia. Wilaya ya Geita ni kubwa, ina zaidi ya watu milioni moja; wana *OCD* mmoja na Hospitali ya Wilaya moja. Tunaomba Wilaya ya Geita igawanywe kwa sababi ni kubwa mno. Ningekuwa na takwimu vizuri, sijui inaweza ikaingia mara ngapi kwa Wilaya ya Geita ambayo ina Kata nne na sisi tuna Kata 33 kubwa kubwa. Najua Serikali imeshatoa ahadi kwamba, itaigawa Wilaya ya Geita, lakini sasa ni vizuri Waziri Mkuu ukasema kwamba, angalau kufikia mwezi fulani tutaanza kushughulikia suala hili. Najua litakuwa limeshaingia kwako, sisi kule tumeshalimaliza kwenye Halmashauri na *RCC* wameshamaliza. Nadhani yameshafika ofisini kwako, sasa tunasubiri Serikali itutamkie kwamba ni lini mtaigawa Wilaya hii kubwa ya Geita?

Naomba suala hili liende sambamba na ombi ambalo limesemwa na wenzangu kwamba, jiografia yetu moja kwa moja inaturuhusu tuwe na mkoa ambao unachukua sehemu ndogondogo kutoka Mikoa mitatu ya Kagera, Mwanza na Shinyanga na kufanya mkoa mmoja pale ambao jina lake Serikali inaweza ikalifikiria. Hili nalo ni la haraka, kwa sababu tunapata matatizo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa James Musalika, tunakushukuru sana. Niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge wa Geita, yaani Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa James Musalika na Mheshimiwa Samuel Chitalilo kwamba, hapa Dodoma kuna Hospitali ya Serikali ambayo inashughulikia yale matatizo yote ya vichwa; kwa hiyo, wasiwe na wasiwasi. *(Kicheko)*

Sasa namwita Mheshimiwa Estherina Kilasi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Mkapa.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Naomba nianze kwa kuipongeza sana Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu; Hotuba hii ni nzuri sana. Kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo langu la Mbarali, kutokana na simu ambazo nimekuwa nikizipata, wanasema kwamba, wanategemea mambo mazuri sana yaliyowekwa kwenye hii Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kuwa haya yaliyoainishwa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, yakitekelezwa vizuri, kwa asilimia kubwa kero za wananchi zitakuwa zimeondoka na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 itakuwa imetekelezwa kwa asilimia kubwa. Kwa hiyo, naomba nipongeze sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kiongozi wetu wa Bunge na mimi nimekuwa nikipata tabu sana, mambo mazuri yanaposemwa halafu yanakuja mambo mengine ambayo wananchi yanawaweka mahali ambapo wanashindwa kuamua! Wenzetu Kambi ya Upinzani, tumewaachia Kamati tatu zenye kuangalia mapato na matumizi na matatizo sugu ambayo ndani yake tumechangayika sisi Wajumbe wa Chama cha Mapinduzi. Mambo mengi yakishasemwa kwenye Kamati yanakuja kuripotiwa ndani ya Bunge na Bunge linaidhinisha.

Kwa hiyo, nami nilikuwa na imani siku zote hizi kuwa wenzetu wakikaa pamoja, huwa wanaulizana kwenye Kamati ya *PAC* mnasema nini, kwenye Kamati ya *LAAC* mnasema nini na kwenye *POAC* mnasema nini? Kuna masuala ambayo ni sugu, Kamati zetu huwa zinayashughulikia. Sikutegemea leo hapa sisi kabla hatujaleta taarifa, Waziri Mkuu aanze kupata tabu ya kujibu masuala ambayo Kamati hizi bado zinayashughulikia. (*Makofi*)

Kwa mfano, nimepata shida sana kwa upande wa *Commodity Import Support Fund*, ni tatizo sugu ambalo Kamati mbili zinashughulikia, lilikuwa likishughulikiwa na *PAC* na sasa linashughulikiwa na Kamati ya Mashirika ya Umma chini ya *TIB.* Kwa hiyo, hili litaletwa na kuripotiwa Bungeni; lisimpe tabu sana Waziri Mkuu kulijibu, kwa sababu tutalileta hapa na itabidi lipatiwe majibu.

Madeni sugu ambayo tumekuwa tukiyasema ndani ya Bunge, orodha tuliletewa ndani ya Bunge na tulipewa sisi kama Kamati tushughulikie. Kwa hiyo, tuwe na subira, Kamati zetu zitatoa taarifa ndani ya Bunge na Wabunge wote tutapata nafasi ya kujadili kwa makini. Kwa hiyo, hilo nilitaka niliweke vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende upande wa Jimbo langu, hayo yalinigusa nilitaka niyaseme.

Nina mambo matatu ya kuyasema; la kwanza, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye mwenyewe ametembelea Wilaya ya Mbarali, hali halisi ya kiutawala ni kubwa sana. Wilaya yenye ukubwa wa kilomita za mraba 16,600, ambayo labda inaweza kukaribia Mkoa wa Kilimanjaro hivi, ina Tarafa mbili tu mpaka leo na tuna Maafisa Tarafa wawili. Taratibu zote tulishazikamilisha kwenye upande wa *RCC* na tumezileta Ofisini, yaani Ofisi ya TAMISEMI, ambayo ipo chini ya Waziri Mkuu. Tunaamini kabisa, Waziri Mkuu ataweza kulishughulikia sasa ili tuweze kupata angalau Nyongeza ya Tarafa.

Tuna tatizo la Kata, nimekuwa nikilisema hapa mara nyingi na jimbo ni kubwa lakini naelewa kabisa kwamba, jibu lake ni wakati tukimaliza kipindi hiki cha 2005/2010. Tarafa wakati wowote ule zinaweza zikaongezwa. Kwa hiyo, ninaomba sana atufikirie kwa hilo ili na tuweze kupunguza ukubwa wa maeneo ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni upande wa kilimo. Nichukue nafasi hii, kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mtakumbuka kipindi kilichopita, wakati mashamba makubwa yale yanauzwa, nilizungumza kwa uchungu sana kwamba, je, wananchi wangu wakulima wadogo wadogo baada ya haya mashamba kuuzwa watakwenda wapi? Serikali kwa umakini ikasema wataandaliwa sehemu muhimu hekta zisizozidi 10,000 ikianzia mwaka huu wa 2007/2008. Nina furaha kwamba, kazi hiyo, imeanza na Waziri Mkuu aliyepita alitembelea. Kwa hiyo, nafarijika na wananchi wa Mbarali wanashukuru kwamba, sasa Serikali ikisema inafanya jambo, kweli inaweza kufanya. Kwa hiyo, naomba nipongeze kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie tu yale mashamba makubwa na Serikali kwa Wilaya ya Mbarali, imewekeza kwa kiwango kikubwa sana kwenye kilimo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, watume wataalamu wako wakaainishe pesa za kilimo cha umwagiliaji; pesa zilizopelekwa Mbarali ni nyingi sana. Tuna mashamba makubwa matatu, ukiacha haya madogo madogo, ambayo yamegharimu pesa nyingi sana lakini haya mawili tumeyauza. Je, baada ya kuyauza tumekuwa tukiwasaidia kwa namna gani, kwa sababu lengo la Serikali la kuuza yale mashamba lilikuwa ni kuhakikisha kwamba kilimo cha mpunga tu ndicho kitakacholimwa; na lazima wazalishe mazao mara mbili au zaidi ya mara mbili ya yale mazao ambayo yalikuwa yanazalishwa huko nyuma kabla Serikali haijauza yale mashamba?

Kwa hiyo, ninawaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Kilimo na Wataalamu; sasa wale ni wakulima wa kawaida siyo wakubwa sana, bado wanahitaji kufuatiliwa kwa karibu kuhakikisha kwamba, wanafanya yale ambayo waliahidi ndani ya makubaliano ya Serikali na wao ili kuweza kuondoa tatizo la chakula hapa kwetu Tanzania. Kilimo cha umwagiliaji Mbarali ndiyo tegemeo kuu. Ikisimamia miradi yote iliyopo Mbarali kwa asilimia 50, kwa upande wa kilimo cha mpunga unaweza ukaondoa tatizo hilo kabisa kwa nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, naomba sana Serikali isimamie upande huo kwa karibu sana.

Nimefurahi sana Mheshimiwa Waziri Mkuu umelisemea hapa suala la mbolea, labda la msingi tu ni utaratibu utakaotumika. Mwanzoni, tuliomba sana Vyama vya Ushirika ndiyo vifanye hiyo kazi, lakini kama kuna utaratibu kama ni wa *voucher system*, kwa hili nitaomba tuwe makini, kwa sababu walengwa mara nyingi wamekuwa hawafikiwi. Utaratibu unaowekwa sasa ni vizuri ukawekwa vizuri, ukahakikisha kwamba yule mkulima ambaye tumemkusudia anapata mbolea na isije ikanunuliwa na kuuzwa tena nje ya Wilaya ile ambayo inatakiwa.

Naungana na Wabunge wenzangu kwamba, sasa wakati muafaka umefika, tusitegemee maeneo machache tu ndiyo yapate mbolea; angalau sehemu zote ambazo watahitaji mbolea na Mikoa yote waweze kupata mbolea ili tuweze kuongeza kilimo na tuweze kuongeza chakula kwa Tanzania nzima.

Lingine kubwa zaidi, Wilaya yangu ya Mbarali imepata mambo mengi sana; nikisema mara nyingi ninaonekana ninalalamika. Wananchi wa Mbarali wameguswa na mambo mazito mengi, wamezungumza Wabunge wenzangu hapa, tukianzia mambo ya uhamishaji wa mifugo. Walikuja wafugaji sawa lakini waliokuwepo pale, unaposema umeweka azimio la kuwaondoa wafugaji na wenyeji waliguswa wamehamishwa sehemu zile. Sasa zile sehemu walizohamishiwa mifugo yao, bado hawajapata zile huduma muhimu maana yake tuliambiwa tubakize mifugo 65,000, huko walikohama wameacha malambo na wameacha kila kitu, lakini walipohamia bado Serikali haijaweka mkono wake.

Lingine, tumeongeza Hifadhi ya Ruaha, kule kumegusa kata moja nzima imehama na vijiji vingine zaidi ya vinne wanatakiwa kuhama. Fidia iliyotolewa na mmekuwa mkiisoma kwenye magazeti na vyombo vya habari; wananchi wanalalamika sana. Tathmini iliyofanywa ukilinganisha na hali halisi ya maisha haviendani.

La pili, tulichowaahidi wana-Mbarali wale sicho kinachofanyika sasa, kwa sababu lile azimio lilipoletwa lililetwa kwa Mkuu wa Mkoa, pamoja na Mkuu wa Mkoa tukahamasisha sote na tuliwaahidi mambo ya msingi kwamba, huko mnakohamia miundombinu yote itawekwa tayari. Kama ni barabara zitawekwa, maji, shule, zahanati na kadhalika, halafu ndiyo mtahamia pale. Wananchi wa Mbarali waliitikia wito huo bila manung’uniko kwamba, hili ni Azimio la Serikali; kwamba, tunataka kulinda vyanzo vya maji na Serikali imetuahidi mambo haya yafanyike haraka iwezekanavyo.

Ninapozungumza hivi sasa, hali halisi haipo hivyo na wakati ule tuliambiwa Wizara nne ndizo zitahusika; sasa cha ajabu kama ni Wizara ya Maliasili kupitia *TANAPA* ndiyo tunaowaona kule na wao nguvu walizonazo kila siku wamesema tulibajeti bilioni nne za kuhamisha watu na miundombinu, lakini mpaka sasa zinatakiwa bilioni 6.6. Shule zilizobomolewa na MMEM na Zahanati zitakazogharimu zaidi ya shilingi milioni 20 kila Zahanati hazijajengwa. Wananchi wamehamia kwenye maeneo yale, hamna maji wala chochote na wengine walihamia wakati wa mvua, kwa hiyo, kulikuwa hakuna kitu chochote pale ambacho kiliwafanya waweze kuishi.

Sasa ninachowaomba Serikali ili kupunguza gharama hizi ni vizuri tukaelekeza nguvu huko. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuma ujumbe wako ili kusaidiana na Wizara zinazohusika zote, kama ni TAMISEMI waangalie kama shule hizi zitajengwa. Hii ni Kwa sababu sisi tuliwaahidi kwamba, kila kitu kitajengwa na Serikali ninyi shughuli yenu itakuwa ni kuhamia. Sasa leo ukiwaambia waanze kuchangia bati, tofali na kadhalika, itakuwa ni kuwaonea sana. Hili limenigusa kwa sababu na mimi mwenzenu silali kila siku napigiwa simu; Mheshimiwa tumepewa fidia shilingi 20,000 na siku za kwenda kukaa huko. Hivi leo ukimhamisha mtu kabla hujajenga nyumba, unamwambia

utakwenda kukaa kwa mwezi shilingi 1,500; utapanga chumba gani kwa hela hiyo hata ukipewa za mwaka mzima?

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama tumechelewa kupitia vile viwango vipya kwa dharura kama hii, tungewafikiria tofauti sana Wananchi wa Mbarali. Wameitikia kila kitu bila unyonge wala malalamiko, wakitegemea Serikali yao na wao itawasaidia kwa kila hali kuhakikisha kwamba, wanapata maisha mazuri zaidi, kwa sababu tulisema mkihama hiki kijiji mnahamia kwenye mazingira mazuri kuliko hapa mnapohama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba sana Waziri Mkuu asimamie hili aone, kwa kweli wale wananchi hawaendelei kulalamika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa elimu; sina tatizo na asilimia ambayo nimeisikia kwenye bajeti, tatizo ni Walimu. *Ratio* ya Walimu imekuwa ni tatizo na mazingira ya Walimu kule ni tatizo. Ukiangalia watu wanakaa vijijini; sehemu hasa za wafugaji mazingira yao ni magumu sana, najua tutakaposikia Bajeti ya Wizara ya Elimu, mambo haya yote yatakuwa yamebadilishwa na bila kusahau barabara vijijini.

Barabara zimesomwa hapa; barabara yangu moja ya kutoka Igawa - Madibira - Mafinga sikuisikia lakini ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi, inatakiwa itengenezwe kwa kiwango cha lami. Nimeangalia vitabu vyote haipo, lakini najua Ilani ya uchaguzi ni ndani ya miaka mitano, kama leo sikuwekwa naamini kipindi kijacho au popote itakapopatikana pesa, basi angalau kilomita moja, mbili au tatu zitaanza kusogea angalau mpaka pale Makao Makuu ya Wilaya ya Mbarali pawe na lami badala ya kupita kwenye vumbi. Wewe mwenyewe umepita juzi, umeona jinsi ambavyo njia hairidhishi na hata Waziri Mkuu aliyepita aliona ile njia. Kwa hiyo, ninaomba na ninafikiri Mbarali tangu tumeanza mambo ya Ihefu; Mawaziri wengi wamepita kule na wameiona hali halisi.

La mwisho, niseme tu kwamba, naipongeza Kamati ya Katiba, Utawala na Sheria, kwa kusisitiza sana mpango wa *CDF*. Wabunge wote tunaunga mkono, tusaidiwe Mfuko wa *CDF* utasaidia kabisa kuleta maendeleo kwenye majimbo yote vizuri. Wabunge hali zetu mnazifahamu, ili sote tuonekane tunafanana kusiwe na tofauti kwa Wabunge wote. Kwa hiyo, hilo ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na bila kusahau na mimi kwa niaba ya Wabunge wenzangu, kama Kamishna waliyenichagua ndani ya Bunge hili, ninayetetea maslahi ya Wabunge, basi ile Sheria ya kupitisha *National Assembly Fund* iharakishwe kadiri inavyowezekana, kabla hatujamaliza Bunge hili hiyo Sheria tuwe tumeipitisha na sisi tuweze kufanya kazi yetu vizuri. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na kukupongeza sana. Nakutakia kazi njema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Estherina Kilasi. Kama nilivyosema mwanzo, anayefuata ni Mheshimiwa Dunstan Mkapa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby. Mheshimiwa *Che Nkapa!*

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniita *Che Nkapa,* maana yake umenirudisha nyumbani kabisa, nakushukuru sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema mengi, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia zote mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga hoja mkono, napenda nichukue fursa hii, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Makatibu Wakuu; Ndugu Mrisho, Mama Tarishi na Wasidizi wake wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuiandaa bajeti hii. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kulalamika kwamba, uwiano wa maendeleo katika nchi hii hauko sawasawa. Mwaka jana, niliwahi kuuliza swali Bungeni hapa nikajibiwa kwamba, Mikoa iliyomo pembezoni mwa nchi itapewa upendeleo maalum, lakini nachelea kusema kwamba, upendeleo huo sijauona. Nilichokiona ni mambo haya haya ya kawaida na kwamba, sisi tunaendelea kubaki nyuma hasa Wilayani kwangu Nanyumbu, kwa sababu ya upendeleo ambao umesemwa na Ofisi ya Waziri Mkuu hapa Bungeni. Labda nielezwe upendeleo tulioletewa kule ni wa kiasi gani? Haya majibu nayaomba wakati Waziri Mkuu atakapojumuisha hotuba yake.

Hali ni mbaya sana, wenzetu wanakimbia nchi hii hii lakini sisi tuko kule, tumebaki kama yatima. Nchi hii hii moja; wengine wanapendelewa, sisi tumebaki tunaangalia. Tunajua kwamba, maendeleo ya nchi huletwa na wananchi wenyewe, lakini kama mwananchi hawezeshwi, atakwendaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na kilimo; nanukuu Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema: “Kilimo bado ni msingi wa uchumi wa Taifa letu.” Nakubaliana naye kabisa, lakini narudia palepale, wakulima wangu kule Wilayani Nanyumbu bado wapo duni kabisa. Jembe ni lile lile la mkono la mwaka 47, mimi nimelikuta, hakuna maendeleo yoyote yanayopatikana kwenye kilimo, hatuna zana nzuri na pembejeo ni tabu.

Namshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa sasa, Kanali Tarimo, amejitahidi sana kuleta maendeleo ya kweli hasa katika Zao la Korosho. Alipata tabu sana katika kuelezea na kuleta msukumo wa stakabadhi ya ghalani lakini mwisho stakabadhi ghalani imefanikiwa na ameonekana kwamba, sasa ni shujaa na imewasaidia sana wananchi hasa kwa kupata bei nzuri ya korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo ni pembejeo za korosho kuchelewa sana. Kwa kawaida, kupulizia korosho ni mwezi wa Nne hadi wa Tano, lakini mpaka sasa kuna baadhi ya sehemu hazijapata pembejeo za korosho hasa *sulphur*, *bifidan* na nyinginezo. Wakati natembelea vijijini, baadhi ya wakulima wa korosho wamelalamikia pembejeo ya *sulphur* ya maji. Wao wanapendelea zaidi *sulphur* ya unga, kwa sababu wameizoea na wameona manufaa yake. Sasa wakati tunabadilika kwenda kwenye *sulphur* ya maji, basi

elimu ingetolewa kwa hawa wakulima ili waone ubora zaidi wa *sulphur* ya maji kwa sababu waliizoea sana *sulphur* ya unga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kukuta Zao la Korosho msimu huu pengine litapungua kwa sababu ya shida hii kwamba, kwanza pembejeo ya *sulphur* imechelewa na pili, wakulima walizoea sulphur ya unga, wamebadilishiwa wameletewa *sulphur* ya maji ambayo ndiyo yenye ruzuku. *Sulphur* ya unga ina bei kubwa sana, imefikia Sh. 30,000 mpaka 50,000, walanguzi wanalangua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala la kuwahisha pembejeo za korosho kwa wakulima litiliwe mkazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba nije kwenye elimu. Elimu Wilayani kwangu ni duni sana na kwa taarifa, mwaka jana tulitangaziwa humu kwamba, Wilaya ya Nanyumbu ndiyo ya mwisho kufaulisha watoto katika Mtihani wa Darasa la Saba. Niliona aibu sana. Tatizo halipo kwa wananchi wala watoto, tatizo lipo kwenye Serikali. Kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu Wilaya ya Nanyumbu kwanza lilikuwa ni dampo la kupeleka walimu wabovu; wale wanaopewa adhabu, walevi na watoro. Wilaya ya Masasi wakati ule ikiwa moja, ilikuwa hakuna sehemu nyingine ni kuwapeleka Nanyumbu. Sasa unategemea nini wakati Mwalimu saa mbili ameshalewa chakari anakwenda darasani, hivi atafundisha kweli? Haiwezekani, kwa kweli hali ya walimu ni mbaya sana Wilayani Nanyumbu. Nimeshalifikisha suala hili kwa Waziri anayehusika, lakini mpaka sasa bado ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule kama za Namatumbusi, Marumba na Lipupu ndiko kwenye matatizo makubwa. Huu ni mifano tu, lakini kote kuna matatizo ya kuwa na Walimu wachache; kuna shule nyingine unawakuta Walimu wawili tu tangu darasa la kwanza mpaka la saba na kila darasa lina mikondo; hebu fikiria walimu wawili watafanya nini? Hakuna, watakwenda asubuhi, watarudi kwenda kuendelea na shughuli zao za kunywa gongo. *(Kicheko)*

Ndiyo, maana kazi zikizidi utafanya nini, unaelemewa unaona bora niache kama ilivyo nikafanye mambo yangu mwenyewe. Vilevile kuna tatizo la nyumba za Walimu na shule nyingine ni za nyasi. Hivi nchi hii mmeshawahi kuona shule ya msingi ya nyasi, njooni kwetu Nanyumbu mtazikuta hizo, ipo pale Mkoromwana. Ndiyo maana tunasema jamani upendeleo usiwe upande mmoja na sisi wa Nanyumbu tunataka maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna miaka 47 ya Uhuru, lakini shule inakuwa ya nyasi! Kwa kweli hili ni tatizo kubwa sana. Wanika ni kijiji kikubwa lakini hakina hata shule ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamalizia mwishoni lakini naomba niseme tu kwamba, hali ya shule, madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo na uhaba wa madawati ni tatizo kubwa sana Wilayani kwangu Nanyumbu. Namshukuru sana Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu, amejitahidi kuhimiza watoto kwenda shule, sababu *rate* ya hali ya ujauzito kwa watoto kule ilikuwa ni kubwa, kwa sababu hii hii; mtoto anakwenda darasani hasomi, atakaa wapi; atasomea wapi? Anaona afadhali arudi nyumbani, akaendelee na shughuli nyingine. Jamani tuangalieni watu wa Nanyumbu tunateseka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu suala la afya. Hivi nchi hii kuna sehemu mtu anasafiri kilomita ishirini kufuata zahanati? Njooni Nanyumbu, mtu anatoka Mbangala Mbuyuni aidha anakwenda Lupaso au Mkonona kilomita ishirini, mgonjwa yuko hoi amebebwa kwenye tenga utafikiri ndizi, ukifunua kumbe ni mgonjwa anapelekwa hospitali. Sitanii hii ni kweli kabisa, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aje Nanyumbu.

Bahati mbaya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyepita, aliikatisha njiani ziara yake, ilikuwa tumweleze yote haya. Namwomba sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Pinda, anionee huruma, wapiga kura wangu wanateseka, najua yeye ni mtu wa huruma, tafadhali aje Nanyumbu ajionee hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu kuna uhaba wa wafanyakazi wa Idara ya Afya, vitendea kazi, Kituo cha Afya cha Nanyumbu hakina gari; ndiyo hayo hayo, unakuta mtu kabebwa kwenye baiskeli anapelekwa Wilayani Masasi au kwenye Kituo cha Afya cha Mangaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie kuhusu miundombinu. Naishukuru Serikali imeanza kujenga barabara ya kutoka Masasi kwenda Mangaka kwa kiwango cha lami. Kwa hilo, nashukuru sana kwa niaba ya Wananchi wa Nanyumbu. Ningeomba vilevile barabara ya kutoka Mangaka kwenda Mtambaswala, kunakojengwa daraja la Umoja, nayo ijengwe kwa kiwango cha lami ili iweze kurahisisha mawasiliano kati ya Mangaka na Mtambaswala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana humu humu Bungeni, Wizara ya Miundombinu ilinihakikishia kwamba, ingeanza ujenzi wa Daraja la Mto Lukwamba lililopo kati ya Napacho pale kwenye Kijiji cha Mpombe. Kazi hiyo haijafanyika, naomba Waziri wa Miundombinu ajiandae, kwa sababu nitatoa shilingi kwa ahadi hewa ambayo alinipa. Hilo ajiandae kabisa, kama kazi hiyo haijaanza tukiwa hapa, basi namhakikishia kwamba nitatoa shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la wanyamapori. Kwa kweli wanyamapori wanamaliza sana wapiga kura wangu kule Nanyumbu. Mwaka jana mpaka mwaka huu kule Mitonga, Chipuputa na Mtawatawa, watu waliuawa kwa tembo. Sasa hali hii inapunguza watu wangu wanaonipigia kura. Sipigiwi kura na tembo, napigiwa kura na wananchi, sasa iweje leo Serikali haitufikirii, tunalalamika kila siku jamani wanyamapori wanatumaliza sisi na mazao yetu lakini Serikali haifanyi lolote? Naomba Wizara ya

Maliasili na Utalii, ituletee angalau gari moja ili liweze kufanya kazi pale Mangaka ya kufanya *patrol* kwenye hizi mbuga na kuwasaka hawa wanyama waharibifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumzia linahusu ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya na nyumba za Halmashauri pale Nanyumbu. Nyumba na Ofisi ya *DC* bado hazijakamilika, zimechukua muda mrefu sana; naomba ofisi yako iwasukume hawa watu wanaofanya kazi hii angalau *DC* wangu aweze kulala na kufanya kazi mahali pazuri. Vilevile Makao Makuu ya Wilaya ya Nanyumbu, bado tumepanga tu kwenye nyumba za Wamishenari, haileti hali nzuri na naomba Ofisi ya Waziri Mkuu ijitahidi kutusaidia ili tuweze kupata ofisi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho linahusu maji. Pale Makao Makuu Mangaka hakuna maji; *DC* wangu anapata tabu sana ya kutafuta maji, ingawa wamechimba kisima lakini yale maji si salama sana yanamwezesha tu kufanya shughuli nyingine. Maji ni tatizo, Wananchi wa Mangaka wanapata tabu, wanatembea huku na kule kusaka maji, wakati huu wa masika inakuwa nafuu lakini maji yenyewe ndiyo hayo ambayo si salama. Vilevile Wilaya nzima tunaushukuru Mradi wa *Quick Wins*, umeweza kutatua baadhi ya kero, lakini tunaomba Awamu ya Pili itusaidie kuwezesha mtandao wa maji Wilayani Nanyumbu ili tuweze kufaidika na matunda ya Uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dunstan Mkapa na tunawapa pole sana Wananchi wa Nanyumbu huko Mangaka, Mtawatawa, Lukwika, Lupaso na Napacho. Kama nilivyosema mwanzo, anafuata Mheshimiwa Shabiby na Mheshimiwa George Simbachawene ajiandae.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu. Vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Wasaidizi wake wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisimama toka niingie Bungeni, kuchangia masuala ya Kitaifa, sijawahi kuchangia masuala ya Jimboni kwangu labda kwenye maswali. Hii ilikuwa inatokana na ahadi, kwa sababu nilikuwa namwona Waziri ananipa ahadi, kwa hiyo, nilikuwa naona haina sababu ya kuja kuzungumza hapa, lakini naona kila siku hizi ahadi zimekuwa hewa. Ndiyo maana leo inanipasa nizungumze. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na Mheshimiwa Mkapa kwamba ni kweli kuna maeneo yanapendelewa bila sababu za msingi au maalum kwenye hii nchi. Watu wamezungumzia kuhusu kugawa Wilaya; Wilaya ya Kilosa ina kilomita za mraba 14,245. Wengine wanaweza kuwa na kilomita za mraba nyingi lakini mashamba tu ya kulima. Wilaya hii ina wakazi wapatao laki sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni sababu ya Mkoa wa Kilimanjaro kuwa mdogo kuliko Wilaya ya Kilosa na ukawa na Wilaya saba na nyingine unaweza kutembea na

baiskeli tu ukazimaliza. Halafu nilipouliza tarehe 8 Februari, 2006 katika Kikao cha Pili, Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa alikuwa Mheshimiwa Celina Kombani, alikiri kutokana na vifungu vya Sheria ya Kugawa Maeneo Mapya ya Utawala, kifungu Na. 7 na 8 cha mwaka 1982 na Kifungu Na. 12 cha mwaka 1914 kwamba, sasa hivi Wilaya ya Kilosa ina kila sababu, kutokana na jiografia yake; idadi ya watu, ukubwa wa eneo, jinsi ilivyo mabonde na milima mikubwa kwamba, sasa inatakiwa kuwa Wilaya isipokuwa inangoja hali ya uchumi kuwa nzuri. Mwaka mmoja tu, aliyekuwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tarehe 2 Julai wakati anajibu swali langu la msingi alisema kwamba, kuanzisha Wilaya ni shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mwaka mmoja, aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa alisema, kuanzisha Wilaya ni Sh. 4.5bn, kuanzisha Halmashauri ni Sh. 5.5bn. Sasa kwa muda wa mwaka mmoja, imetoka Sh. 1bn mpaka Sh. 4.5bn! Sisi tunasubiri hali ya uchumi ipande mpaka hizi Wilaya ifike Sh. 80bn. Halafu majibu yasivyokuwa ya uhakika, tarehe 23 katika kikao kilichopita cha 11, Mheshimiwa Celina Kombani alimjibu Mheshimiwa Msindai kwamba, kuanzisha Wilaya ni Sh. 2bn, sasa inapanda na kushuka! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tu peke yake, inaonekana kabisa kwamba, haya majibu hayana uhakika kabisa. Ninazo *Hansard* zote, zikihitajika nitazileta kwa ushahidi, napenda sana kutunza ushahidi. Nasema vilevile katika swali langu la nyongeza la tarehe 8 Februari, Kikao cha Pili, alijibu ambaye sasa hivi ni Waziri Mkuu wakati huo akiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mizengo Pinda kwamba, mwaka 2005 tumegawa Wilaya saba na sasa tumebakisha Wilaya kumi na moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo kuna Wilaya 35 zinazoomba, wakati mwaka 2005 zilikuwa 11 katika kumi na nane. Wilaya nyingine zilizogawiwa kwa mguu tu unaweza kutembea ukamaliza huku na kule siyo kama Gairo. Gairo si mchezo, usione pale unapopita kwenye vituo vya mafuta ile siyo Gairo, ule ni Mtaa wa Gairo. Pale barabarani Mheshimiwa Ndugai na Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa walishafanya kazi katika Wilaya ile, wanaifahamu vizuri. Pale tunapopita kwenye vituo vya mafuta, kilomita mbili ndiyo Mji wa Gairo, pale ni barabarani panaitwa Njia Panda. Kutoka pale kwenda Tarafa ya Nongwe ni kilomita 110, milima yake ni mirefu kuliko ya Lushoto. Hajawahi kufika Kiongozi wa Kitaifa kwenye Tarafa ya Nongwe toka dunia ianze. *(Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na bahati mbaya, akionja siku moja harudi tena mpaka anahama. Akija Mkuu wa Wilaya akienda kule harudi tena, huyu Mkurugenzi wa Wilaya hajawahi kufika hata siku moja; sasa maendeleo yatatoka wapi? Utakuta kuna wahandisi tu hata hawaeleweki, wakiambiwa jenga daraja Mkurugenzi mwenyewe hata hatembelei, ukienda Mbunge unaambiwa mimi ndiye mtaalam; hata mimi mtaalam wa kuona vilevile. Maana yake utaalam wa kuona nao hauna haja ya kusomea kitu hicho na nina uzoefu wa kujenga. Shahidi yangu ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, wakati akiwa Waziri wa Maji na Mzee Wasira,

tuliandikiwa kwamba tutatengenezewa visima vya maji, kila mashine moja ina-*cost* Sh. 21.4m.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri, nilipomwomba Mzee Wasira kwa wakati tofauti, pamoja na Naibu wake, alimkuta yule Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Kilosa anachomelea ile mashine, yaani hata laki tatu ile mashine haifiki; akamwuliza yaani wewe unachoma mbele yangu leo nimekukamata hivi hivi. Cha ajabu yule kahamishwa Wilaya ya Kilosa kapelekwa Bunda, yaani kama unachukua ugonjwa hapa unaupeleka sehemu nyingine. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu mnasema tutapata maendeleo, hii hotuba haitakuwa nzuri kama Serikali za Mitaa hazitakaa sawasawa. Juzi niliongea na Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, nikamwambia twende ukaone daraja. Daraja limegharimu zaidi ya shilingi milioni na kitu, lakini zimewekwa tripu tatu za mawe. Nikamwambia, nataka ukaone wewe mwenyewe. Kisingizio, ninyi Wabunge kwenye Halmashauri hampo. Sasa wewe upo hapa, kama leo unachangia halafu ndiyo unaitwa na wakikugundua kama unawabana sana na unaelewa hawakuandikii na utasikia tulifanya juzi, barua yako hujaipata. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya sasa ni mambo ya kuwaharibia Waheshimiwa Wabunge. Kwa mfano, kama mimi nikitoka Gairo mpaka nifike Wilayani Kilosa ni kilomita 178. Diwani wa Chanjale nikitaka kumfuata lazima nipite kwa Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kilomita 17 kuingia Mpwapwa Mjini, nakata tena mkono wa kushoto kilomita tano, naingia Jimboni kwangu kilomita zaidi ya 80. Kwa hiyo, akitaka kutoka kule mpaka aje Gairo, kwanza, hapati hata hizo barua. Kata ya Mandege kuna msitu mkubwa wa Ukaguru lakini sijawahi kuona yeyote akipita kule, hata mwenye cheo, hakuna hilo, wanaogopa milima ile. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyejkiti, nimeshaangusha gari kule imekuwa *write-off* na si langu tu magari mengi yameshaangushwa, lakini hakuna cha kuzungumza. Sasa moja ya utawala mzuri ni kugawanywa Wilaya hii ili yale maeneo ambayo tunataka kuyatawala yawe karibu karibu. Mwaka jana, Shule ya Msingi Chanjale yenye wanafunzi 750, haikufanya Mtihani wa Darasa la Saba kwa sababu walimu wote hawataki kwenda. Sasa tukifika hapa tuna kazi ya nadharia, tunasoma kwenye vitabu, tulifanya hivi na vile utendaji sifuri. Siwezi kufagilia mambo ambayo unaona hayaendi sawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye kitu cha msingi, ikifika mwaka 2010, kama nikitaka kugombea Ubunge sifikirii kama watu wanaangalia huyu Shabiby au nani, watu wameshaweka maswali kabisa, nitatolewa mkuku mpaka nitachanganyikiwa. Unafikiri mwananchi wa Gairo nitakwenda kumwambia masuala ya *EPA,* sijui *Richmond,* anajua wapi kwanza hiyo, yeye atasema ulituahidi maji yako wapi, tena Mheshimiwa Rais mwenyewe, kwa bahati nzuri amepita mara mbili pale. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kabla hajaja huku amepita pale akafungua kambi ya vijana. Alipotoka Morogoro kuja Dodoma alipita tena

pale, alipowaona tu akasema najua tatizo lenu ni maji, hakuna kitu. Umekuja ule Mpango wa *World Bank* wa vijiji kumi, tumekiingiza Kijiji cha Chakwale tumechanga Sh. 5.3m, mpaka leo huo Mpango hata haueleweki umefia wapi. Gairo ndoo moja ya maji ni Sh. 900; Mzee Malecela na Mwenyekiti mwenyewe ni mashahidi. Vilevile Mheshimiwa Kombani ni shahidi kwa sababu alikuja wakati akiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Wamechimba kisima kinatoa lita 20,000 kwa saa, wakasema sasa tumeshapata maji tutachimba visima vinane, waombeni watu wa barabara watuwekee kalvati; tumeomba, tumekwenda wenyewe, toka kichimbwe hicho kisima mpaka leo, hakijatokea kisima hapa. Kwa hiyo, propaganda sasa hivi ndiyo zinazoenea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nasema hatuwezi katika Hotuba ya Waziri Mkuu, hasa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo inalenga kwa wananchi wetu wa Vijijini, kama hatuna mpangilio mzuri. Hii itakuwa hadithi, mtawapa mabilioni ya pesa yataishia mifukoni mwa watu, mkija hapa mnawapa Hati Safi tu. Tanzania nzima hakuna Hati Safi hata moja, hebu wekeni basi wataalam hata kutoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenyewe au Miundombinu, wawe wanapitia zile kazi zinazofanywa wazione. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naunga mkono hoja, lakini Bunge lijalo …

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Shabiby, nami kama jirani yako, nashuhudia kwamba Wilaya ya Kilosa ni kubwa sana. Mheshimiwa George Simbachawene, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nami pia nianze kwa kuipongeza hotuba hii nzuri, ambayo imetolewa na Waziri Mkuu na ninawapongeza pia Watendaji wote wa Ofisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nami nianzie hapo hapo kwenye Halmashauri. Nimekuwa kwenye Kamati ya *LAAC,* kwa kiasi fulani nazifahamu Halmashauri karibu zote nchi nzima. Ukinitajia Halmashauri yoyote, naweza kukupa *status* yake iko hivi na vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie, kama kweli tunasema maisha bora yanawezekana kwa kila Mtanzania, basi inawezekana tu kama tutaweza kuzikamata Halmashauri zetu zikafanya kazi zinayotakiwa kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mengi mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuambia hapa katika hotuba yake, ikiwa ni pamoja na kuongeza posho kwa

Madiwani na mambo kadha, nampongeza lakini nataka niseme kwamba, hali ya Halmashauri zetu kiutendaji si sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipende kutafuta sifa tu hapa ya kusema tunazipongeza Halmashauri, lakini ukweli wa dhati hali si sawasawa. Nadhani kuna haja ya kufanya mambo kadhaa katika kurekebisha hali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani nilikuwa najiuliza hivi mtu ili awe Mkurugenzi anapatikanaje, yaani unapoambiwa huyu Mkurugenzi wa Halmashauri fulani anachaguliwa kwa sifa zipi, anapimwa na nani na kwa vigezo gani? Maana yake kuna Wakurugenzi wengine unaangalia jukumu alilopewa lilivyo zito la kuhakikisha kwamba watu wale wanatoka katika umaskini, kuhakikisha kwamba watu wote kwenye Halmashauri zote wanapata maendeleo, asimamie masuala ya ujenzi wa miundombinu, maendeleo ya elimu, mifugo, kilimo halafu unasikitika kama kweli hivi huyu mtu amepimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa *DCs*, nauona upo makini kidogo, lakini wa Wakurugenzi nadhani tufike mahali tukubaliane, tusiajiri kwa utaratibu wa kuteua ni afadhali wakaingia mkataba, ikawa ni kazi ambayo wanaomba na wanafanyiwa usaili kwa sifa zinazotakiwa na kwa uwezo utakaopimwa pale ili waweze kupewa ile kazi siyo unamchukua mtu aliyekuwa mwalimu wa sekondari. *Okay*, anaweza kufanya kama anafahamu Halmashauri zinafanyaje, lakini ametolewa mahali ambapo haijui *Local Government* kabisa, anapewa Ukurugenzi. Haya tumeyaona, hali ni mbaya. Nadhani sasa kuna haja Serikali kuangalia utaratibu wa uteuzi wa Wakurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi ndiye *Accounting Officer* kwenye Halmashauri na ndiye *custodian* wa kila kinachotokea kwenye Halmashauri yake. Hapa chini anakutana na watu wajanja ajabu, atazungukwa hakuna kitakachofanyika, itakuwa kama mwenzangu Mheshimiwa Shabiby alivyokuwa anasema, hata sisi ni mafundi wa kuangalia kwa macho. Kwa hiyo, nasema Serikali ilione jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la Makao Makuu Dodoma. Nimesoma ukurasa wa 74, naomba ninukuu maelezo ya Hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 74 ile aya ya kwanza, ameeleza vizuri kwamba; “Serikali inataka kupitia upya Programu ya Kuendeleza Makao Makuu, lakini anasema Programu hii itafanya marekebisho ya kimfumo yatakayozingatia mabadiliko katika mazingira ya nchi yetu kwa hivi sasa.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana naye kabisa kupitia upya, lakini kuna mahali kidogo sina uhakika kama tafsiri yangu ipo sahihi, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa anamaanisha amesema hivi: “Katika mwaka 2008/2009, Serikali itaendesha mjadala wa Kitaifa utakaoshirikisha wadau mbalimbali, kuhusu suala la uhamishaji wa Makao Makuu kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma. Baada ya mjadala huo, Serikali itaandaa mapendekezo ya kutunga Sheria mpya, kuitambua rasmi Dodoma kuwa Makao Makuu.” Suala la kutunga Sheria mpya sina tatizo nalo, maana itakuwa na

madhumuni ya kutaka suala zima la kuhamishia Makao Makuu Dodoma liwezekane. Vilevile Sheria iliyopo ina upungufu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu hapa ni huo mjadala, tunajadili nini? Makao Makuu kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma ni suala ambalo limekuwepo; *it is a fact* kwamba, Mtanzania yeyote anajua Makao Makuu ya nchi yetu yapo Dodoma. Sasa tunajadili kitu gani? Sina hakika kama nilielewa vizuri. Nadhani hapa nitaomba nieleweshwe ilikuwa ina maana gani? Ilimradi tu maana ile isiwe kuleta mjadala wa jambo hili zima na kama ni mjadala kwa ajili ya kupeleka mbele utaratibu huu mzima wa kuhamishia Makao Makuu Dodoma, siyo kuuliza hapana au ndiyo, sawa; lakini kama ni kinyume na hapo, nadhani siafikiani nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichangie mambo yanayohusu Jimbo langu. Miradi ya Maji, nilipoingia kwenye Bunge hili niliambiwa tuna miradi kumi katika Wilaya ya Mpwapwa na mimi Kibakwe nilipata miradi mitano ya *World Bank*. Kwa hiyo, nikajua hapa mambo safi kwamba nitawekewa maji Vijiji vya Kidenge, Chinyang'huku, Wiyenzele, Makose, Kisima kwa Mradi wa *World Bank*, lakini *Quick Wins* utaweka Kibakwe, Kisima, Minguwi, Singonali na Wiyenzele. Nikatoka hapa kwa jeuri kubwa, nikaenda kwa mbwembwe nyingi, nikatamba sana kwamba, mambo sasa safi, wanaoshindwa Ubunge wanashindwa tu, mimi nimekwishauweza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha ni hali hii kwamba, kumbe mambo haya bado, imekuwa ni ahadi nilizozitoa na ukipewa ahadi ya Serikali ukienda kule unatamba kweli na *document* unaonyesha, mnaona hii miradi; lakini mpaka leo ninavyozungumza, siwezi nikaeleza hata *status* yake ikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema *we must be serious*. Tumesema mpaka kufikia mwaka 2010, asilimia 65 ya watu wa vijijini watakuwa wamepata maji. Tuna maana ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, tutahojiwa hayo. Miradi ya Maji sina hakika nchi nzima imekwenda vipi, lakini kwa maana ya Wilaya yetu ya Mpwapwa, hali ipo pale pale. Naiomba sana Serikali, ituambie kwa ufasaha na kwa uwazi ili tuache kusutwa kule na wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, nataka niseme, kama miradi hii haitafanyika mimi Ubunge sina. Mimi nitaukosa Ubunge, lakini sina hakika Serikali yangu itakuwa inahukumiwa vipi? Kwa hiyo, ninasema tushirikiane katika jambo hili, Miradi hii ya *World Bank* na ya *Quick Wins* iweze kufanyika kama tulivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mgawanyo wa maeneo ya kiutawala. Imefika mahali, suala la kupata kibali cha kijiji au Kata nalo linakuwa ni gumu kama unavyozungumzia Wilaya yenye mamilioni haya wanayosema. Imebadilika sasa inakuwa suala la wewe kutuletea Kata au kama hautatuletea hatutakuchagua, inakuwa siasa. Badala ya kusema tu-*achieve* katika mambo mazito na muhimu ya maendeleo kama ya elimu na nini; unahukumiwa kwa suala la kugawanya Kata tu kusema Mtendaji wa Kata ni fulani basi, sana sana subiri mpaka uchaguzi ukifika achaguliwe Diwani,

maana pale watumishi wapo wangapi, nafikiri ni wawili, watatu tu, Afisa Mtendaji wa Kata, Mifugo na kadhalika, hao wengine hata wakibakia!

Mheshimiwa Spika, kuna gharama gani hapa kutenganisha Kata? Nimeomba Kata ya Rudi itenganishwe, mtu anapotoka Rudi pale mpaka afike kule kwenye Bwawa la Mtera ni kilomita karibu 62, umbali huo ni mkubwa, Mtendaji wa Kata hawezi akatoka hapo akaenda kule na hana pikipiki. Mimi ninasema jambo hili hebu lisigeuke kuwa siasa au hukumu ya Viongozi wa Siasa; hili ni jambo jepesi na linalowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atuambie *status* ya hii nayo kama ina ugumu kama zilivyo Wilaya na Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kwenye mambo mengine; nizungumzie suala zima la ujenzi wa barabara za vijijini. Mwaka jana kwenye bajeti walisema wametenga shilingi bilioni 65 kwa ajili ya barabara za vijijini. Hali kadhalika, mwaka huu zimetengwa bilioni hizo hizo. Ninataka tujiulize *impact* ya zile bilioni 65, nani anaweza akaijua; ni dhahiri kwamba hakuna kitu. Mimi ninasema tatizo kubwa linalotokea kule, nizungumzie kwa kifupi tu ni kwamba, Wakandarasi wetu, kweli Sekta Binafsi lazima tuishirikishe katika uchumi, haiwezi ikaachwa lazima Serikali iitunze Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunafahamu uwezo wa Sekta Binafsi; wakandarasi wetu hawana uwezo mkubwa wa kuweza kununua mashine kubwa kama *bulldozer* na nyingine kwa ajili ya kutengenezea barabara. Hivi kuna ugumu gani kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuagiza tu kwamba kila Halmashauri iweke mipango yake ya kununua vyombo vyake kwa ajili ya kuwakodisha hao wakandarasi? Fedha nyingi zinapotea wanapokwenda kukodi *bulldozer* kutoka Tanga ije mpaka Mpwapwa - Kibakwe, fedha nyingi zinatumika hapo na wanakodishwa kwa siku. *Bulldozer* hizo zikiwa ni za Halmashauri, nina hakika wakandarasi watakodi pale na barabara zitakuwa nzuri, kwa sababu gharama za uendeshaji zitakuwa ndogo, kwa hiyo, wata-*perform* kitu kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tukiwabana vipi hawatafanya vizuri, kwa sababu gharama ni kubwa ya kukodi hivyo vifaa kutoka sehemu za mbali. Anaweza kukodi, lakini roda ya kubebea ile *bulldozer* anapata wapi hiyo fedha, atakuja pale atachukua kwanza malipo ya awali akienda kule zimekwisha, anakuja tena anambembeleza *engineer*. Kwa hiyo, ninasema tutafika mahali tutajikuta hatuoni thamani ya fedha tunazoziweka, kwa sababu ya kitu hicho. Kama inawezekana, Mheshimiwa Waziri Mkuu, aziagize Halmashauri ziweze kuwa na vifaa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mabati yaliyotumika katika kujenga majengo yetu ya sekondari na shule za msingi. Nitoe ombi tu kwa Serikali, ifanye tathmini ya mabati yaliyotumika kujengea majengo yale. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC*, nilifika kuyaona ndani yana geji 30 na 32 lakini yamepigwa mhuri wa geji 28. Fanyeni utafiti na Serikali iagize kama inawezekana, makampuni hayo yanayouza mabati hayo maana yanajulikana, yaweze kulipa fidia kama wataonekana wame-*supply* mabati yaliyopigwa mihuri ya namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezitembelea Halmashauri nyingi na tumezikuta hivyo ni tatizo kubwa. Serikali iliangalie suala la mabati, shule tulizojenga mwaka juzi na mwaka jana, zimekwishaanza kuoza na hali si nzuri. Kabla hatujamaliza kipindi hiki cha miaka mitano, shule zitahitajika kuezekwa tena, hili ni tatizo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima la kilimo. Kule vijijini tuziamini Halmashauri. Mimi ninasema Halmashauri zishindanishwe. Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe agizo la kushindanishwa Halmashauri namna ya ku-*supply* zana za kilimo, washindanishwe wamekopesha trekta ngapi kwa wakulima; majembe ya kukokotwa na ng'ombe wangapi; na wamekopesha *power tillers* ngapi? Ninaamini ikienda kwa *assessment* ya namna hiyo, baada ya miaka kumi tutajikuta karibu wakulima wengi wamepata mikopo, lakini kusema mikopo ya benki siyo rahisi mwananchi wa kawaida apate mkopo wa benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu lingine ni la madini. Nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitaja Winza ambako yamegundulika madini ya *safayer* kwamba ni eneo la wachimbaji wadogo. Napenda nichukue nafasi hii, kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Mwakapungi na Kamishna wa Madini, Dr. Kafumu, kwa namna nilivyoshirikiana nao kuhakikisha kwamba, mpango ule wa wachimbaji wadogo kupata maeneo unawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Simbachawene ninakushukuru sana. Kama nilivyosema, atakayefuata ni Mheshimiwa Grace Kiwelu na mzungumzaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Mudhihir.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hotuba hii ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri, ambayo tunategemea yaliyoandikwa kwenye kitabu chake cha hotuba, ndiyo yatakayotekelezwa; maana uzuri wa kitabu unategemea na jinsi watendaji watakavyopokea na jinsi watakavyotekeleza. Kwa hiyo, tunawaomba watekelezaji, yale yaliyoandikwa kwenye kitabu waweze kuyasimamia ili wananchi wetu waweze kupata hayo maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Halmashauri zetu. Mimi pia ni Mjumbe wa *LAAC*, kwa kipindi cha pili sasa. Niunge mkono hoja ile aliyoiacha Mheshimiwa George Simbachawene ya kuhusu Wakurugenzi. Tuambiwe ni vigezo gani vinavyotumika kuwapata Wakurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu zinapelekewa fedha nyingi sana, lakini kama Wakurugenzi hao watashindwa kusimamia vizuri, hatutaweza kuona *impact* ya fedha zile zilizopelekwa kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu tumefanya ziara nyingi katika Halmashauri zetu tumejionea, tumewauliza maswali Wakurugenzi, tumeshindwa kupata majibu. Ndiyo maana imefika mahali sasa Wajumbe wa Kamati ya *LAAC*, tunaomba kama hakuna vigezo ambavyo vinatumika kuwapata Wakurugenzi, basi tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa kuwe na vigezo kwa ajili ya kuwapata Wakurugenzi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi huko vijijini haitekelezwi kwa viwango vinavyopaswa na hii inatokana na wale ambao wamepewa majukumu kutokusimamia vizuri utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Waziri Mkuu, zile takwimu walizozisoma ndani ya Bunge kuhusu shule zilizojengwa si sahihi, kwa sababu kuna miradi ya mwaka 2006/2007, ambayo haijatekelezwa mpaka leo hii ninapoongea mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, takwimu zile si sahihi, zipo nyumba za walimu hazijajengwa mpaka leo na fedha zilikwishatolewa, lakini hakuna kilichofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda sasa ufike wakati, wale waliokabidhiwa nafasi hizo waweze kuzisimamia vizuri. Madarasa na nyumba za walimu zilizojengwa, ninahofia kusema na ninamwomba Mwenyezi Mungu yasije yakatokea yale yaliyotokea Dar es Salaam; yanaonyesha kabisa yana nyufa, mchanga unatumika zaidi kuliko sementi na watoto wetu wanasomea mle madarasani. Nyumba za walimu hali kadhalika zipo hivyo hivyo. Walimu ni kama wafanyakazi wengine, nao wanahitaji kupata nyumba nzuri, waweze kukaa kwenye maeneo mazuri na wapate zile huduma zote muhimu, kama kweli tunataka elimu bora kwa watoto wetu. Hatuwezi tu kujenga jengo tukaliwekea bati, hakuna madirisha, hakuna milango, tukasema nyumba imekamilika na tukamtaka mwalimu yule akae mle ndani ili aweze kutufundishia watoto wetu, walimu hawatakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo basi, tunaomba Wizara inayohusika, iweze kuhakikisha miradi hiyo ya nyumba za walimu inakamilika kama kweli tunataka walimu waende huko. Lipo tatizo la ukosefu wa walimu katika shule zetu; shule zetu nyingi zimejengwa, wananchi wamejitolea sana kujenga shule hizo lakini hazina walimu na hasa walimu wa sayansi ni tatizo sana katika shule zetu hasa za sekondari, walimu hao hawapo kabisa. Tumwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, atakapokuja kuwasilisha bajeti yake, atupe mikakati wamefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwishauliza swali hapa ndani ya Ukumbi huu na wakasema wapo mbioni kumaliza tatizo hili. Tunamwomba basi Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, atakapowasilisha bajeti yake, tuweze kuona wamefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo hilo la elimu, tuna upungufu mkubwa sana katika shule zetu wa matundu ya vyoo. Katika ziara tuliyoifanya Kamati yetu ya *LAAC*, kuna shule moja tulikuta ina wanafunzi 900, lakini ina matundu manne tu ya vyoo. Kwa kweli huo siyo uwiano mzuri. Pamoja na kutaka elimu nzuri kwa watoto wetu, lakini

afya nayo inahitajika. Kwa hiyo, tungeomba mahitaji yote muhimu yazingatiwe katika zile shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo Kamati yetu ya *LAAC* iliweza kukumbana nalo; kwa kuwa tunapeleka fedha nyingi sana katika Halmashauri zetu, tungeomba wakaguzi wa ndani waweze kuwepo katika Halmashauri zetu yaani waajiriwe. Kwa sababu wakaguzi hao wa ndani, watazisaidia sana Halmashauri na Serikali kuweza kuona zile fedha zinazotumika kule katika Halmashauri zetu, zinafanya kazi namna gani na kuweza kutoa taarifa mapema kwa Mkurugenzi kwa yale maeneo ambayo hayaendi vizuri katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee tena katika shule zetu hizo hizo. Baadhi ya shule tulizozitembelea hazina viwanja vya michezo. Hili nalo wanasema wamerudisha nyuma michezo shuleni, lakini watoto wetu hawataweza kucheza au kushiriki katika michezo kama viwanja havipo katika shule zetu. Tatizo hili limejitokeza katika shule nyingi na hasa za Jiji la Dar es Salaam na maeneo mengi ya wazi katika Miji yetu, imeyagawa kwa watu wenye uwezo wa fedha na kusababisha watoto wetu kukosa maeneo ya kuchezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili linaletwa na Idara ya Mipango Miji; wameliingiza Taifa kwenye malumbano makubwa na kuliingizia hasara kwa sababu ya tamaa yao ya kupokea rushwa na kugawa viwanja mara mbili mbili na kutoa zile *open spaces* ambazo zingesaidia watoto wetu kucheza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kabisa Wizara inayohusika wawe wakali kwa hao watu wa Mipango Miji, kwa sababu tumechoka kusikia matatizo hayo kila siku. Dar es Salaam tunasikia migogoro ya viwanja, migogoro ya ardhi. Tunaomba sasa wale waliokabidhiwa nafasi hizo waweze kusimamia kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye afya. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, amelizungumzia suala hili katika hotuba yake. Ila ningependa kusisitiza hili la vifo vya akinamama na watoto wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litawezekana tu kama vile Vituo vya Afya na Zahanati tulizonazo, zitapata wauguzi, madaktari na vifaa vya kutosha, kusogeza huduma zaidi kule vijijini ambako huduma hii haipatikani kwa urahisi. Kama tutatimiza haya yote, ninaamini tutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu naye ameweza kulisemea sana tatizo hili la akinamama na watoto. Nilishawahi kubahatika kusafiri na Mheshimiwa Rais, naye aliliongelea tatizo hili na alisema ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu. Ninaamini basi misaada tutakayopata, pamoja na fedha zetu za ndani tutakazopanga katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, akinamama hao na watoto waweze kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukadhibiti kule vijijini, lakini vifo vingine tunavisababisha na vingine tunaona vitokea huku huku Mijini. Tumesoma kwenye magazeti na kuona kwenye vyombo vya habari, wapo akinamama wajawazito, wanapokwenda kujifungua wanapokosa kuwa na fedha za *gloves*, wauguzi wanakataa kuwahudumia na kusababisha kina mama kupoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba suala hili lichukuliwe kwa umakini mkubwa kwamba, akinamama na watoto kwenye zoezi hili la kujifungua ni sehemu moja hatari sana. Ninakumbuka katika Bunge lako Tukufu hili, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, aliwahi kusema kwamba, akinamama wanapokwenda kujifungua hawahitaji kulipia, lakini wanapofika katika hospitali zetu huwa wanadaiwa fedha ili waweze kuhudumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la hatari na tunawaomba wauguzi watusaidie katika hili ili tuweze kupunguza vifo hivyo vya akinamama na watoto. Tunaomba wale wote wanaohusika kusababisha vifo kwa akinamama na watoto, wachukuliwe hatua kali ili iwe fundisho kwa wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini ugumu wa kazi zao usipoteze maisha ya binadamu wengine na watoto hao ambao hawana hatia wanaokuja duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongelee suala la viwanda, nalo pia Mheshimiwa Waziri Mkuu ameligusia katika hotuba yake. Mimi natoka katika Mkoa wa Kilimanjaro, tofauti na miaka ya nyuma; watu walikuwa wanauona Mkoa wa Kilimanjaro upo mbele kimaendeleo; lakini siku zinavyozidi kwenda, uchumi wa Kilimanjaro unazidi kushuka. Viwanda vyetu vilivyokuwa katika Mkoa wa Kilimanjaro baada ya kubinafsishwa waliovichukua viwanda vile wamevifunga, hakuna chochote kinachoendelea katika Mkoa ule wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mkuu wetu wa Mkoa, Ndugu Mohamed Babu, amejitahidi sana kufuatilia viwanda hivyo. Tumeongelea katika *RCC* lakini bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakapohitimisha hoja yake, basi atuambie vile viwanda vyetu katika Mkoa wa Kilimanjaro; wale waliovichukua kama wameshindwa kuviendeleza waturudishie. Kwa sababu uchumi wetu wa Mkoa wa Kilimanjaro unazidi kudidimia, Wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro wamekosa ajira, vijana wapo mitaani hawana kazi na kama viwanda vile vingekuwa vinafanya kazi, vingetusaidia kupunguza tatizo la ajira katika Mkoa wetu na kuongeza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Makao Makuu Dodoma; ni mara yangu ya pili katika Bunge lako Tukufu, kila ikija Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, linazungumziwa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Mheshimiwa George Simbachawene; kwamba wamesema linajadiliwa, sasa sijui kinachojadiliwa ni nini? Nakumbuka nikiwa darasa la nne, niliulizwa swali; Makao Makuu ya nchi yako wapi? Nikasema yapo Dodoma. Leo nipo ndani ya Bunge, nina mtoto yupo Kidato cha Tatu, naye anaulizwa swali hilo hilo, lakini bado hatujafikia muafaka. Tatizo ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Waziri Mkuu atakapokuwa ana-*wind up,* atuambie kwa nini hawataki kuhamia Dodoma au ni yale aliyosema aliyekuwa Mbunge wa Biharamulo, Mheshimiwa Phares Kabuye kwamba, Dodoma ni Makao Makuu ya Bunge na Makaburi ya Viongozi; kama ndivyo, basi watuambie ili Wananchi wa Dodoma walijue hilo mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zinazidi kwenda, Viongozi Dodoma hawaji, wakija ikifika Siku ya Ijumaa wanarudi Dar es Salaam, wanakuja tena Siku ya Jumatatu. Sasa ifike wakati, wananchi wajue ukweli wa jambo hili la kuhamia Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa suala la Madiwani; kilikuwa ni kilio cha muda mrefu, lakini sasa naona Waheshimiwa Wabunge wamesema na hatimaye kilio chao kimesikika.

Niwaombe Waheshimiwa Madiwani huko waliko, kwa kuwa Serikali yetu inapeleka fedha nyingi katika Halmashauri zetu, basi waweze kuisimamia ile miradi ambayo inapangwa katika Kata zao. Maana kama tukiwaachia tu Watendaji, watakaohukumiwa ni sisi wanasiasa; 2010 tunarudi mbele ya wananchi na kama hutatawaeleza nini kimefanyika katika Kata zao, basi tujue kurudi kwetu kutakuwa ni kugumu sana. Kwa hiyo, ni vizuri sisi wanasiasa; Wabunge na Madiwani, ile miradi ambayo inapangwa katika Halmashauri zetu na katika Kata zetu, tuweze kuisimamia vizuri na kama haiendi vizuri, tufikishe hoja hizo katika Halmashauri zetu ili tuweze kuzijadili kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Grace Kiwelu, pamoja na mambo mengine, umezungumzia jambo muhimu sana la kuhamia Dodoma. Nami ninatoa wito kwa Vyama vya Siasa vya *CUF, TLP, CHADEMA, NCCR* Mageuzi, pamoja na vingine, viige mfano wa CCM wa kufanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya Vyama hivyo. Moja kwa moja namwita Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mbunge wa Mchinga, Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunijalia nafasi hii. Mimi nataka kuanza na suala la maji. Tarehe 17 Julai, 2007, niliandikiwa barua hii na Waziri wa Maji, yenye Kumb. Na. BA.30/544/01, ikiniambia kwamba, Kijiji changu cha Mputwa kipatiwa shilingi 128,994,000 kwa ajili ya Skimu ya Maji ya Pampu Mputwa.

Kijiji cha Milola kitapatiwa shilingi 141,600,000 kwa ajili ya *Milola Gravity Scheme*. Vijiji vya Kiwawa, Likwaya, Namkongo, Kilolambwani, Chikanji navyo vingepata hela katika robo ya kwanza ya mwaka 2007/2008, hii ni robo ya mwisho. Barua hii kivuli chake nitakikabidhi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hatua zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipotoka na barua hii nilikwenda kutoa *photocopy* kupeleka kwa *DED* wangu, nikapita kule nikaisoma nikawa nashangiliwa. Kwa sababu wakati ule nilikuwa na mikono yote miwili salama na mimi nikawa najibu yote miwili. Nilipokwenda hii juzi baada ya kutoka hospitali, basi hata ule mkono mzima nilishindwa kuunyanyua kwa aibu. Jamani kama hawa wataalam walikuwa wanamtania Waziri; Waziri huyu hana utani na watu wa Lindi. Dada yangu aliyesaini barua hii alikuwa Mama Mwangunga na Waziri wake wakati ule alikuwa mzee wangu pale. Hawa wote wawili hawana utani na Wamwela wala Wamachinga.

Naogopa kusema walituongopea, watu wazima hawawezi kusema uongo; wanasema uongo kwa shida gani, maana mtu hukupelekwa mahakamani kwa nini useme uongo? Mimi nitaomba mtusaidie; mkienda leo Chikonji, Likwaya, Kilolambwani na Kiwawa, watu wanakunywa maji ya kwenye barabara ikinyesha mvua. Sasa hivi mvua zimesimama, wao na maji ni kama mbingu na ardhi wakikutana kiama. Hilo lilikuwa la kwanza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Kijiji cha Nanyanje kipo katika Jimbo la Mchinga. Dada yangu, Mbunge wa Viti Maalum *CUF*, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, alizungumza juzi hapa habari ya Nanyanji; ni kweli Sekondari ya Nanyanje imehamishiwa Chikonji. Mimi kama Mbunge wa Jimbo la Mchinga, sina ugomvi na wanakijiji wangu wa Kijiji cha Chikonji kuwa na sekondari hata kidogo.

Nilipopata habari hii sikukurupuka, nilikwenda kwa Mkuu wa Mkoa nikamwuliza; kumetokea nini Bwana Mack Sadick? Akaniambia kilichotokea nikaridhika naye kwamba, kwa wakati ule asingechukua hatua hiyo na hii shule maana yake ilikuwa inafungwa. Kwa jitihada zake, wiki ijayo wataalam wakaguzi wa elimu kutoka Mtwara wanakwenda tena kufanya ukaguzi wa sekondari hii mpya ili Sekondari ya Nanyanji ambayo haikufutwa usajili wake iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu si tu Mheshimiwa Mbunge aliingia kwenye Jimbo la Mchinga bila kufanya utafiti, lakini tunamvunja nguvu Mkuu wa Mkoa huyu, Mack Sadick. Ameingia Lindi kukiwa na sekondari 18, leo ninaposimama hapa tuna sekondari 96. Kwa hiyo, ningeomba sana, wanasiasa wenzangu; tunalipokuta mahali kuna tatizo, tufanye jitihada za kukutana na Watendaji wetu tujue suluhu. Mimi nilikwenda kutafuta suluhu; vijana wangu wa Nanyanje na Chikonji watasoma na wala siyo dhambi, kwa sababu hata Kilwa anakotoka Mheshimiwa Mbunge, katika kata ile ya Zinga, kuna Sekondari Zinga Kibaoni na kuna sekondari pale Migulue. Hata Nyangamala pale kuna sekondari, Mandwanga kuna sekondari na Chiuta kuna sekondari. Kwa hiyo, hakuna ubaya kuwa na sekondari Nanyanje na Chikonji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Zarafi vilevile, alizungumzia vibaya sana suala la ufuta na Mkuu wangu wa Mkoa kwamba, *Mohamed Enterprises* amekwenda anataka kununua ufuta kwa Sh. 1,800 lakini Mkuu wa Mkoa ameng'ang'ania lazima ununuliwe na Ushirika kwa Sh. 1,300. Watu wa Lindi, Mtwara na Ruvuma, tulikuwa tunamkaba koo mzee wetu pale, Mheshimiwa Wasira, juu ya ununuzi wa korosho na ufuta. Mzee akasema nitawasaidieni kama Serikali, kuhakikisha Vyama vyetu vya Ushirika vinafufuliwa. Mwaka jana kwa mara ya kwanza, hakuna korosho ambayo imelala nyumbani kwa mtu kwa sababu ya Ushirika. Kwa mara ya kwanza, mwaka jana Chama chetu cha Ushirika cha Ilulu, kilizilipa Halmashauri zake shilingi milioni 730 kutokana na ushuru wa korosho.

Kwa mara ya kwanza, Chama cha Ilulu kimelipa shilingi milioni 85 kama kodi kwa *TRA*. Haijawahi kutokea *TRA* kupata kodi ya korosho, lakini shilingi bilioni tatu zilirudishwa kutoka katika Vyama vya Ushirika kwa kukosa korosho. Mwaka huu tukasema kazi hiyo hiyo ifanyike, lakini tukautahadharisha Ushirika utangaze *tender* ili watu wengi waje. Vimejitokeza vyama vitano; vitatu vimesema tutanunua ufuta kwa shilingi 1,800 lakini kilo 3,000 tu. Lindi wastani wetu ni tani 20,000, wangenunua hizi tani 9,000 tani nyingine 11,000 zingenunuliwa na nani, tukasema mje mnunue kwenye Ushirika; ndiyo Ushirika huu ambao utatusaidia na sasa hivi unasambaza pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie ukweli; tuliambiwa kuwa hapa kuna wananchi wamezuiwa na gari lao na ufuta. Kuna mtunza hazina wa chama kimoja cha siasa pale Kilwa wa Kata ya Makangaga kwenye Kijiji cha Mageuzi, kanunua ufuta kwa *king'omba* (kikopo hivi ndiyo kilo wenyewe wanaita), kwa shilingi 350 ili msimu ukija auze kwa bei kubwa. Watu hawa 85 nashukuru wameliripoti suala hili kwa *DC* na huyu bwana hajulikani alipo. Vilevile kuna kiongozi mwingine ambaye ni Diwani kupitia chama kimoja cha siasa, yeye alinunua ufuta kwa shilingi 800 ili aje auze kwa shilingi 1,800; ana tani 6½ amezificha na mwenyewe amejificha. Naishukuru sana Serikali ya Wilaya inamtafuta, ufuta huu warejeshewe wenyewe wakauze kwa bei inayotakiwa kwenye Vyama vyetu vya Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu kuna *tendency* kwamba, Chama chetu cha Mapinduzi kinawanyanyasa wananchi kwenye elimu, kimewanyanyasa wananchi kwenye ufuta; ukweli ndiyo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni la mwisho, mimi siwezi kusema sana, nina tabia ya kuzungumza sana lakini sio leo. Basi kama nitapata nafasi nitamalizia lingine. Ninataka kuzungumzia habari ya kuwepo kwetu hapa. Waheshimiwa Mawaziri hawa na mimi nilikuwa Naibu Waziri; madereva wao wana posho kule nje hawana tabu hata kidogo. Mkuu wa Mkoa hapa wa Tanga, nimekaa naye jirani hapa dereva wake ana posho ya Serikali. Wakuu wa Mikoa waliokuja kumsikiliza Waziri Mkuu. madereva wao wana posho na wataalam wetu. Madereva wetu sisi Wabunge tuliokaa humu ndani na mimi nalisema baada ya kupata ajali, ndiyo naona kweli umuhimu wa dereva upo.

Madereva wetu mnaowaona hapa, ambao wapo hapo nje, posho yao ya kukaa Dodoma wanagawana na posho ya Mbunge. Posho ninayopata mimi Mbunge, ndiyo dereva nimgawie kwa ajili ya kula na kulala na mwanadamu yule akihitaji kupata sigara

hiyo hiyo posho yangu. Posho hiyo hiyo ndiyo anayotakiwa atume *weekend* kwa watoto wake huko nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema wakati umefika; muda mwingine mtu anakuja humu ndani anachekea hapo mlangoni baada ya kuingia, kwenye gari toka ametoka nyumbani dereva amemchukua amenuna mpaka hapa na wewe unashindwa kumkemea kwa sababu unajua kosa ni lako. Mimi ningeomba kwa kweli wakati tunasubiri sijui *Bunge Administrative Act,* kipindi hiki Mheshimiwa Waziri Mkuu, uwe msikivu sana; una huruma sana mimi nakujua, hebu tuwafikirie hawa madereva wetu; watatumaliza kwenye mikenge siyo kwa uzembe hapana mawazo; kapigiwa simu mtoto anaumwa hana cha kumpelekea dawa.

Mimi hapa kuna wapiga kura kule wananipigia simu, lakini na hapa getini nikitoka kuna wapiga kura wengine tunawakuta ambao wao ni wa kitaifa siyo wa Jimbo wanatusubiri nao. Sasa unakuta Mbunge anakuwa kama samaki vile, maana yake samaki ukimtoa baharini muda huo huo anakufa na Mbunge akitoka Bungeni muda huo huo anakufa kwa sababu ya majukumu! *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeomba sana, Waziri Mkuu wetu ni mtu mwenye huruma sana na msikivu; wakati anafikiria kupata suluhisho la kudumu kwa ajili ya madereva, basi kipindi hiki walau kumdanganyia, *General Pass* wa *US Marine Couples* alisema, ukiwa umekamatwa barabara katika uwanja wa mapambano, ukawa hujui la kufanya; dawa siyo kukaa bure. Ukikaa tu bure, unakaa mahali ambapo adui yako anakutaka ukae, ukianza kutembeatembea basi unabadilisha kanuni za mchezo, maana itabidi aanze tena kuku-*target*. Sasa kipindi hiki watu tusikae bure kusubiri wakati huo, hebu tuanzeni kulishughulikia suala la madereva ni gumu.

Kwa sababu sisi na *front bench* wote ni Wabunge, hata ninyi mnafahamu matatizo mnayopata kwa yule dereva unayemwacha nyumbani na yeye anakuwa na matatizo yale yale yanayofanana na madereva wetu, sema sisi inazidi kwa sababu tukitoka hapa inabidi tukatembelee jimboni na kule nako hali inakuwa hiyo hiyo. Unaweza ukasema si yuko jimboni bwana, lakini jimboni dereva wangu kwao Mchinga, mimi nakwenda mpaka Milola, Nangalu, huko kwingine siyo kwake na tunalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninaamini kabisa barua hii ambayo kopi yake nitaipeleka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, itashughulikiwa ili na mimi nikienda kule sasa nipokewe. Toka nilipokuwa napokewa kwenye vijiji hivi kwa wali; ukaja ugali; sasa hata madafu sipati tena. Hii ni dalili mbaya kwamba, siyo madafu; kinachofuata na kura zenyewe zitakuwa hazipatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mudhihir na ulikuwa mzungumzaji wetu wa mwisho. Niseme tu kwamba, kesho tutaendelea na majadiliano haya na Wabunge wafuatao waendelee kujiandaa; Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Mohamed

Missanga, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Aziza Ally, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe na kadhalika. Kwa hiyo, majadiliano yataendelea kesho.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa kazi zote zilizopangwa katika *Order Paper* ya leo zimekamilika na muda wetu uliobaki ni mdogo sana, hauwezi kumtosha mzungumzaji mwingine yeyote kwa jioni ya leo, basi naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.38 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 25 Juni, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*